# Nipashe

Jumatatu Septemba 16, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580024

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13



## Tucta yaanza uchokozi kikokotoo kipya cha mafao kwa wafanyakazi

UKURASA 21



# Chadema yaweka wazi hatima Lissu urais 2020

• **Yasema** mambo hadharani wakati utakapowadia, yataja vigezo na masharti...*Ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**LIPUMBA AWANOA CUF UCHAGUZI MITAA**

CHAMA cha Wananchi (CUF) kimewapa majukumu watendaji wake kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa...

**UKURASA WA 8**

**UJENZI GATI BANDARINI D'SALAAM WAKAMILIKA**

SERIKALI imesema ujenzi wa gati namba 0 katika Bandari ya Dar es Salaam umekamilika, na kwamba utakuwa na uwezo...


## Majaliwa asimamisha watumishi kisa bil. 1.3/-

UKURASA 3



Rais mstaafu Jakaya Kikwete (katikati), akishiriki matembezi ya Brazuka Marathon ya kilomita tano ya kukusanya fedha zitakazotumika kwa ajili ya watoto wenye matatizo ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Kasoro nane zaibuliwa kanuni uchaguzi mitaa

UKURASA 2


**MICHEZO** **AUSSEMS KUKOMALIA WASHAMBULIAJI SIMBA** UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Chadema yaweka wazi hatima Lissu urais 2020

**Na Enock Charles**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vincent Mashinji, amefunguka kuhusu suala la Mwanasheria Mkuu wa chama hicho, Tundu Lissu, kutajwa kuwania urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Mashinji ameweka wazi kuwa chama kinaweza kumpa nafasi hiyo Lissu iwapo ataiomba. Akizungumza na Nipashe kwenye mahojiano maalumu jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Dk. Mashinji alibainisha kuwa Chadema huwapatia nafasi za kugombea wanachama wanaoomba, iwapo hapatakuwa na mwanachama yeyote aliyeomba ni jukumu la chama kutafuta mgombea miongoni mwa wanachama wake watakaonekana kuwa na sifa hiyo.

"Akiomba anaweza kupewa kwa sababu kwa mfumo wetu wa kugombea wanapewa nafasi watu walioomba na kama tutakosa mtu aliyeomba, basi tutatafuta mtu ambaye hajaomba," alisema Dk. Mashinji.

Tetesi za Lissu kuwania nafasi ya urais katika uchaguzi wa mwaka 2020 zilianza kuzagaa katika mitandao ya kijamii, ikimuhusisha kupitia muunganiko wa vyama vya ACT-Wazalendo na Chadema.

Vilevile, kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amekuwa akimtembelea mara kwa mara Lissu aliyeko Ubelgiji anakopatiwa matibabu kwa sasa.

Lakini wawili hao walipoulizwa na baadhi ya vyombo vya habari vya kimataifa, walieleza kuwa ukaribu wao kama wanasiasa wamekuwa wakikutana na kujadili masuala ya namna ya kujenga mapambano ya kujenga Tanzania mpya ya kidemokrasia na inayojadili haki za binadamu.

Dk. Mashinji akizungumzia zaidi kuhusu mchakato wa kumpata mgombea urais ndani ya chama hicho kikuu cha upinzani nchini, alisema kupitia sekretarieti ya chama hicho, majina ya wote walioomba nafasi ya kugombea urais hufikishwa Kamati Kuu.

Alisema baada ya hapo Kamati Kuu hutoa idhini ya majina hayo kutangazwa, hivyo kutoa fursa ya kufanyiwa utafiti ili kupata jina moja litakalosimama kuwania urais.

**MAANDALIZI YA ILANI**

Kuhusu maandalizi ya ilani ya uchaguzi mkuu wa mwakani, Dk. Mashinji alisema chama hicho kimeshaanza mipango ya kukusanya taarifa mbalimbali kutoka kwa wadau ili kutengeneza ilani itakayokuja na majibu ya masuala mbalimbali ya maendeleo.

"Ni jana tu tumemaliza kuweka taratibu za namna gani tutafanya hizo document (nyaraka), ni ilani inayolenga kukuza uchumi na kuiwezesha sekta binafsi kukua," alisema Dk. Mashinji.

**UCHAGUZI WA S/MITAA**

Kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambapo upinzani umelalamikia kuwa kanuni zilizopo sio rafiki, Dk. Mashinji alisema kuwa pamoja na kuwapo kwa kanuni sizizo rafiki chama hicho hakina mpango wa kususia uchaguzi huo.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako (kushoto), akipeana mikono na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mwalimu Commercial Bank Plc, Richard Makungwa, baada ya kuhutubia kongamano la walimu lililokwenda kwa jina "Amsha Amsha na Mwalimu Bank" kwenye ukumbi wa Serengeti wilayani Kasulu mkoani Kigoma juzi. Kongamano hilo liliandaliwa na Mwalimu Commercial Bank kwa lengo la kutoa elimu ya fedha kwa walimu kutoka wilaya za mkoa huo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kasoro nane kanuni uchaguzi wa Serikali Mitaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKATI uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2019 ukitarajiwa kufanyika Novemba 24, mambo manane yamebainika kutozingatiwa katika utungaji wa kanuni zake, huku serikali ikiombwa kuangalia namna ya kuyazingatia wakati wa mchakato huo.

Upungufu huo umebainika katika uchambuzi uliofanywa na Mtandao wa Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (Tacceo) na Jukwaa la Sera (Policy Forum) kuhusu kanuni hizo.

Akitoa tamko kuhusu kanuni hizo jana jijini hapa, Mwenyekiti wa Policy Forum, Martina Kabisama, alisema asilimia 70 ya mambo waliyopendekeza kwenye kanuni hizo yamezingatiwa lakini bado kuna masuala ya msingi ambayo hayakuzingatiwa katika utungaji husika.

"Masuala mengi yamezingatiwa na kufanyiwa maboresho kama tulivyopendekeza. Policy Forum na Tacceo tunapongeza serikali kwa kuzingatia takribani asilimia 70 ya maoni na mapendekezo yetu," alisema.

Alitaja mambo hayo kuwa ni ushiriki wa watu wenye ulemavu na mwenye mahitaji maalum, sababu za kuahirisha uchaguzi, sifa za msimamizi wa uchaguzi, mkanganyiko wa majina ya kanuni, kinga kwa msimamizi wa uchaguzi, kibali cha waangalizi wa ndani wa uchaguzi, tafsiri ya mkazi na mapungufu ya kiuchapaji kwenye majedwali na fomu.

**USHIRIKI WENYE ULEMAVU**

Kabisama alisema kwa mujibu wa Kanuni za Mamlaka za Miji na Mamlaka ya Wilaya (vijiji) kifungu cha 32(1) na Mamlaka za Wilaya (vitongoji) kifungu cha 31(1) kinasema kutakuwa na sanduku maalum la kupiga kura lililotengenezwa kwa namna itakayomwezesha mpigakura kutumbukiza karatasi ya kura kwa urahisi.

"Pia kifungu cha 36(1) cha Mamlaka za Wilaya - vitongoji kinaeleza juu ya usaidizi kwa wenye mahitaji maalum katika kupiga kura," alisema.

Kwa mujibu wa Kabisama, maoni yamezingatiwa ingawa kanuni hizo hazibainishi namna ambavyo watu wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum watafikia sanduku la kupigia kura kwa urahisi.

**KUAHIRISHA UCHAGUZI**

Mwenyekiti huyo alisema kanuni hizo hazijaeleza bayana juu ya sababu za msingi ambazo zitapelekea kuahirisha kwa zoezi la uchaguzi.

"Kwa mfano, kufariki (dunia) kwa mgombea, kutokea kwa janga la asilia na kutokea kwa magonjwa ya mlipuko, hivyo ni vyema kanuni zikaweka bayana sababu za msingi za kuahirisha," alisema.

Pia alisema kwa mujibu wa kanuni hizo, vifungu vya 37 (mtaa na kijiji) na 36 (kitongoji) vinasema endapo siku ya kupiga kura kutatokea jambo lolote litakalozuia upigaji kura kuendelea kufanyika, msimamizi msaidizi wa uchaguzi baada ya kuwasiliana na msimamizi wa uchaguzi, ataahirisha uchaguzi.

**SIFA ZA MSIMAMIZI**

Mwenyekiti huyo alisema kwa mujibu wa kanuni hizo, tafsiri ya msimamizi wa uchaguzi ni mtumishi wa umma tu, jambo ambalo linamnyima nafasi raia mwingine asiye mtumishi wa umma kuwa msimamizi wa uchaguzi.

**MKANGANYIKO MAJINA YA KANUNI**

Alisema katika kanuni hizo sura ya 288, inaonyesha jina ni Kanuni za Uchaguzi kwa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji.

"Mamlaka za miji hakuna kitongoji, badala yake ingesomeka kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa kitongoji katika Mamlaka ya Miji Midogo za mwaka 2019 (Sura ya 288)," alisema.

**KINGA KWA MSIMAMIZI**

Mwenyekiti huyo alisema kwa mujibu wa kanuni hizo, kifungu cha 49 (Mtaa na Vijiji) na 46 (Kitongoji) vimempa kinga msimamizi wa uchaguzi, msimamizi msaidizi wa uchaguzi, msimamizi wa kituo, wajumbe wa kamati ya rufani au mtumishi yeyote wa umma aliyehusika na usimamizi wa uchaguzi hatawajibika kwa jinai au madai au kuchukuliwa hatua za kinidhamu au kiutawala kwa jambo lolote alilolifanya au kuacha kufanya kwa nia njema.

"Changamoto ya kifungu hiki ni uwezekano wa mhusika kutumia vibaya madaraka yake kwa kisingizio cha 'nia njema' kwa kuwawekea kinga wasimamizi wa uchaguzi, kunazuia vyombo vya kutoa haki kutimiza wajibu wake na raia yoyote kukosa haki ya kudai katika vyombo hivyo," alisema.

**KIBALI WAANGALIZI**

Alifafanua kwa mujibu wa kifungu cha 50(1)(2) cha Mamlaka za Wilaya- Vijiji na Mamlaka za Miji na kifungu cha 47(1) cha Mamlaka za Wilaya- Vitongoji, waangalizi wa ndani wa uchaguzi wataweza kuangalia uchaguzi baada ya kupata kibali kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa tu.

"Kifungu hiki kinaleta urasimu usio wa lazima wa kupata vibali hasa kwa vikundi ambavyo viko mbali na Ofisi ya Katibu Mkuu wa Wizara," alisema.

**TAFSIRI YA MKAZI**

Kabisama alisema kwa mujibu wa kanuni hizo tafsiri ya mkazi ni raia wa Tanzania anayeishi kwenye eneo la mtaa, kijiji au kitongoji ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyoko katika eneo la kijiji, mtaa au kitongoji.

"Kifungu hiki hakikutumika bayana muda wa mtu kutambuliwa kuwa mkazi wa kijiji, mtaa au kitongoji, hivyo kinaweza kutoa mwanya kwa raia yeyote mwenye nia ovu au wahamiaji haramu kujiandikisha na kupiga kura," alisema.

**UPUNGUFU KIUCHAPAJI**

Mwenyekiti huyo alisema wamebaini upungufu wa kiuchapaji kwenye majina ya kanuni ambayo pia yameathiri fomu zilizoambatanishwa na wanatambua kwamba baadhi ya fomu zitarekebishwa

INAENDELEA UK.8

TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**WUZHOU INVESTMENT** COMPANY ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SANLG YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 256 BSQ** YENYE CHASSES NO **LBSPJB56H90Z**1117 NA ENGINE NO SL **157FMI 17925328**

TAARIFA YA POLISI: **KHM/TR /RB/660 /2019**

XXXXXXXX

VYETI VIMEPOTEA



**PETER ELISA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0351/097 kilichotolewa na BAGAMOYO SEKONDARI mwaka 1988. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.119/573** kilichotolewa na KIBAHA SEKONDARI mwaka 1991.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MOR/RB/1064/08.**

115419302

# Majaliwa asimamisha watumishi kisa bil. 1.3/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewasimamisha kazi watumishi saba katika halmashauri mbili za Wilaya ya Kilombero kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha zaidi ya Sh. bilioni 1.3 za makusanyo ya mapato ya ndani.

Mbali na kuwasimamisha kazi watumishi hao, pia Waziri Mkuu ameagiza warejeshe fedha hizo ndani ya siku tatu kabla hajamaliza ziara yake ya kikazi mkoani Morogoro. Watumishi hao ni pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Ifakara, Fransis Ndulane, anayedaiwa Sh. milioni tano alizoingiziwa katika akaunti yake bila maelezo yoyote.

Waziri Mkuu aliwasimamisha kazi watumishi hao jana wakati akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero pamoja na watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara, akiwa katika siku ya pili za ziara yake ya kikazi mkoani Morogoro.

Amesema: "Mkoa mzima wa Morogoro umekuwa na tatizo la upotevu wa mapato, fedha zinakusanywa zinapita mikononi mwa watu hazifiki benki, hii ni shida, hatutavumilia."

Waziri Mkuu alisema kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kipindi cha mwaka 2016 hadi Juni 2019, katika mji wa Ifakara, makusanyo yalikuwa ni Sh. bilioni 2.7, ambapo fedha iliopelekwa benki ni Sh. bilioni 1.9, na kwamba kiasi cha Sh. milioni 727 hazijulikani zilikoenda.

Alisema katika mitambo kumi ya ukusanyaji wa mapato iliokaguliwa, imeonyesha kiasi cha Sh. milioni 348 zilizokusanywa hazikupelekwa benki, hivyo kuishia mikononi mwa watu.

Waziri Mkuu alisema katika uchunguzi huo, ilibainika fedha hizo ziliingizwa katika akaunti mbalimbali za watumishi wa halmashauri hizo kutoka kwa mtendaji wa Kata ya Viwanja 60 katika Mji wa Ifakara, Gregory Midas.

Watumishi hao ni Reina Mrema, ambaye anadaiwa kuchukua Sh. milioni 298, Haile Njitango milioni 73, Linus Mdembo kiasi cha Sh. milioni mbili kwa kushirikiana na mtendaji huyo wa kata.

Waziri Mkuu aliagiza Mkuu wa Kitengo cha Tehama katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara, John Mvanga, ambaye ndiye alibaini kuwapo kwa ubadhirifu wa fedha hizo na baadaye kusimamishwa kazi, arejeshwe kazini mara moja na asibughudhiwe.

"Mlimsimamisha kazi kwa sababu mlijua amegundua madudu yenu, lakini haisaidii, arejeshwe kazini naagiza apewe ulinzi wa kutosha."

Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, Waziri Mkuu alisema zaidi ya Sh. milioni 600 hazijulikani zilipo, huku kiasi cha Sh. milioni 98.5 zikidaiwa kuingizwa katika akaunti za watumishi wa halmashauri hiyo bila maelezo yoyote.

Majaliwa amewataja watumishi hao ni Devid Onyango aliyechukua Sh. milioni 51, Elakada Kanongole Sh. milioni 36, Fork Karunde Sh. milioni nane na Charles Chali Sh. milioni 2.5.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiongea na watumishi wa Wilaya ya Kilombero, mkoani Morogoro wakati wa ziara yake mkoani humo jana. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Steven Kebwe. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## Bunge laitaka serikali kutumia vifaa vya polisi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeitaka serikali kuvitumia vifaa vya Jeshi la Polisi ambavyo vipo kwenye makontena bandarini kama taratibu zinavyoelekeza.

Hatua hiyo imekuja baada ya wajumbe wa kamati mbili waliotuliwa na Spika wa Bunge Job Ndugai kufuatilia suala la vifaa hivyo kutokana na kuwapo kwa mjadala baadhi ya wabunge kudai kuwa vifaa hivyo havijanunuliwa na Kampuni ya Daissy General Traders iliyopewa zabuni hiyo.

Akizungumzia suala hilo mwishoni mwa wiki wakati akiahirisha Mkutano wa 16 wa Bunge, Spika Ndugai alisema wakati wa Bunge la Bajeti siku ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi liliibuliwa suala la vifaa hivyo, huku Waziri Lugola akisisitiza vifaa hivyo vipo.

"Wakati Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, anahitimisha hoja yake kulikuwa na suala la vifaa vya Jeshi la Polisi ambavyo ilikuwa inadaiwa kwamba havijanunuliwa wengine wanasema vimenunuliwa na Waziri alishuhudia hapa bungeni kuwa vifaa vipo," alisema.

Alifafanua kuwa baada ya hoja hiyo aliteua wajumbe kadhaa wa Kamati za Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na kamati ya Hesabu za Serikali (PAC), ambapo walienda wajumbe wakashuhudia makontena hayo yaliyopo bandarini yana vifaa.

Mkutano wa Bunge wa 15, sakata la vifaa hivyo liliibuliwa bungeni wakati wa Bunge la Bajeti hali iliyomlazimu Spika kuteua wajumbe wa kamati hizo kufuatilia suala hilo.

# Lipumba awapa majukumu makatibu CUF uchaguzi

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Wananchi (CUF) kimewapa majukumu watendaji wake kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu.

Watendaji hao ambao ni Makatibu wa Wilaya zote za Tanzania Bara, walipewa majukumu hayo jana, jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Taifa wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba, alipokuwa anafungua semina ya siku tatu kwa ajili ya kuwawezesha kujifunza mambo kadhaa.

Alisema jukumu la kwanza la makatibu hao ni kubainisha majukumu na wajibu wa Makatibu wa Wilaya kwa mujibu wa Katiba ya CUF kwa mujibu wa Ibara ya 71.

Prof. Lipumba alisema Katibu wa Wilaya ndiye mtendaji mkuu wa chama katika wilaya anayepaswa kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maamuzi ya vikao vya kikatiba na maelekezo ya Katiba ya Chama.

"Miongoni mwa majukumu hayo ni kutunza mali za chama, kutunza takwimu za wilaya, kata na matawi yote yaliyomo ndani ya wilaya kuhusu wanachama, wapigakura kwenye kila mtaa, kijiji, kitongoji, kata na jimbo," alisema.

Alisema semina hiyo itawawezesha makatibu kuyaelewa kadhaa ikiwamo katiba ya chama ili waelewe majukumu na wajibu wao na umuhimu wa ushirikiano na kuheshimu maamuzi ya vikao katika utendaji wa kila siku.

Mwenyekiti huyo alisema kipa kuielewa sera na itikadi ya CUF, Sera ya Haki Sawa kwa Wote na Itikadi ya Utajirisho kama ilivyofafanuliwa kwenye Utangulizi wa Katiba ya CUF kwenye Tamko la Waasisi wa Chama lililotolewa 1992 msingi wake mkuu ni tamko la Umoja wa Mataifa la mwaka 1948 kuhusu haki za binadamu.

Alisema itikadi ya utajirisho maana yake ni kutumia utajiri wa nchi kwa manufaa ya wananchi wote. "Hii ndiyo sababu tumekuwa tukipiga vita ufisadi nyakati zote kwa kuwa asili ya ufisadi ni kutumia utajiri wa nchi kwa maslahi ya mafisadi wachache," alisema na kuongeza:

"Utajirisho maana yake ni haki sawa kwa wote na neema kwa wote. Tunapozungumzia haki sawa kwa wote tunamaanisha haki ya kisiasa, haki za kiuchumi, haki za kijamii katika maisha yetu ya kila siku."

Alisema lengo la semina hiyo ni kuwaanda makatibu wa wilaya kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa, vijiji na vitongoji kwa kuangalia changamoto za kanuni na mwongozo wa uchaguzi.

Prof. Lipumba aliwatala makatibu hao kuwa makini na njama za CCM na wasimamizi wa uchaguzi huo hasa kutokana na uzoefu wa uchaguzi uliopita ambapo wasimamizi wamekuwa wanawatangaza wagombea wa CCM kuwa wamepita bila kupingwa.

"Suala la wapigakura kutakiwa kuwa na vitambulisho ndio waweze

INAENDELEA UK.8

SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS


TAIFA STARS vs SUDAN
SEPTEMBA 22, 2019 • UWANJA WA TAIFA
HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

# Bilioni 10/- kujenga hospitali ya mkoa

**Na Elisante John,** SINGIDA

UJENZI wa hospitali ya rufani ya mkoa wa Singida unaoendelea kwenye eneo la Mandewa, Manispaa ya Singida, utagharimu Sh. bilioni 10, badala ya Sh. bilioni 150, zilizokusudiwa awali kabla ya serikali kuingia madarakani mwaka 2015.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alisema hayo jana baada ya Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Deogratius Banuba, kusoma risala mbele ya Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliyekuwa mgeni rasmi kwenye makabidhiano ya gari la kubebea wagonjwa, lilitolewa Mbunge Viti Maalumu (CCM), Aysharose Mattembe.

Katika risala hiyo, Dk. Banuba ambaye ni daktari bingwa wa upasuaji mifupa, alisema kasi ya mradi huo inakabiliwa na changamoto ya fedha ili kukamilika kama ulivyokusudiwa kwenye eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 125, kutoka lile la awali dogo lililopo katikati ya mji wa Singida.

Dk. Banuba alisema licha ya fedha hizo kutumika kwa ajili ya majengo yote yenye hadhi ya hospitali ya rufani katika eneo hilo, pia zitagharamia nyumba za madaktari, vifaa tiba, ujenzi wa nyumba za wataalamu wengine wa afya, chuo cha madaktari na huduma nyinginezo za tiba.

Msaada huo kutoka kwa Mbunge Mattembe unajumuisha vitanda 16, vikiwamo saba vya kulalia wagonjwa na viwili vya wajawazito kujifungulia vikiwa na thamani ya Sh. milioni 14, na gari la kisasa la kubebea wagonjwa lenye muundo wa Hiace, lenye thamani ya Sh. milioni 21.

Akifafanua juu ya fedha hizo, Dk. Nchimbi alisema haiwezekani kiasi chote hicho kigharamie mradi huo, wakati hivi sasa serikali imeshajenga hospitali mpya mbili katika wilaya ya Mkalama na Halmashauri ya Wilaya ya Singida kwa Sh. bilioni tatu tu.

"Gharama hizi ni kubwa, tumejenga hospitali mbili kwa Sh. bilioni tatu, Sh. bilioni 1.5 Mkalama na Sh. bilioni 1.5 zingine Singida Vijijini na zote zimekamilika. Hii hospitali ya rufani tunataka itumie Sh. bilioni 10 tu," alisema.

Akizungumza na waganga, wauguzi, watumishi wa hospitali hiyo na wananchi kwa ujumla, Dk. Tulia alipongeza juhudi za Mattembe katika kuisaidia jamii ya Singida, hususan sekta ya afya.

Alisema alichokifanya Mattembe kinapaswa kupongezwa kwa kuwa fedha alizotumia kununulia vifaa hivyo angeweza kutumia kwa matumizi binafsi, lakini kutokana na upendo alio nao kwa wananchi wake, ameona vyema azielekeze kwenye huduma ya afya.

Awali Mattembe alisema kuwa amelazimika kutoa msaada huo kutokana na hospitali hiyo ya rufani kukosa gari la kubebea wagonjwa, hali iliyoathiri ufanisi wa kuwahudumia wagonjwa hasa wajawazito wanaozidiwa na uchungu wanapokwenda kujifungua.

Ujenzi wa hospitali ya rufani ya mkoa wa Singida, ulianza kutekelezwa na serikali ya awamu ya tano kwa usimamizi wa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Dk. Parseko Kone, lakini hadi sasa mradi huo mkubwa kabisa haujakamilika.



Waziri wa Madini, Doto Biteko (kushoto) na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (wa pili kushoto), wakitembelea machimbo ya madini yaliyopo wilayani Bukombe mkoani Geita mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Wafanyakazi Makumbusho wafundwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wa Makumbusho ya Taifa ya Tanzania, wametakiwa kufanyakazi kwa bidii na maarifa kwa ajili ya maendeleo ya nchi na kutimizi azma ya serikali ya kufikia uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa, Dk. Gwakisa Kamatula, aliyasema haya mwishoni mwa wiki alipokutana na watumishi wa taasisi hiyo kwa lengo la kujitambulisha na kuelezea mikakati ya kuboresha utendaji wa shughuli za kimakumbusho ili kuendana na kasi ya serikali na kusikiliza changamoto za wafanyakazi.

Dk. Kamatula aliwataka watumishi hao kufanyakazi kwa weledi kulingana na fani walizosomea na kuongeza ubunifu ili kuleta tija kwa taasisi na taifa kwa ujumla.

"Tunatakiwa kuwa wabunifu katika kazi zetu ili kuongeza thamani kwa yale tunayoyafanya," alisema.

Aliwataka watumishi wa taasisi hiyo kuhakikisha kila mmoja anatekeleza majukumu yake wakati uongozi unashughulikia changamoto zinazowakabili.

"Juhudi za makusudi zinafanyika kuhakikisha changamoto zinazolikabili shirika zinatatuliwa," alisema na kuongeza kuwa watumishi wanatakiwa kutimiza wajibu wao mahali pa kazi.

Alisema ofisi yake inafanyia kazi changamoto za vitendea kazi, maboresho ya miundombinu ya makumbusho na upungufu wa rasilimali watu katika taasisi hiyo.

Aliwataka watumishi kuzingatia sheria, taratibu na miongozo ya utumishi wa umma ili kuendana na kasi ya utekelezaji wa majukumu ya serikali.

"Mimi nitasimamia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma, hivyo sitarajii kumpendelea au kumwonea mtu yeyote kwa sababu mimi ni kiongozi ambaye natakiwa kutenda haki kwa wote," alisema Dk. Kamatula.

Meneja wa Utawala na Rasilimali Watu, Nuru Sovella, alimtambulisha Dk. Gwakisa Kamatula kama ndiye atakayekaimu nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa mpaka serikali itakapoamua vinginevyo. Hii inatokana na aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa, Prof. Audax Mabula, kutimiza miaka 60 ya utumishi wake.

# Malaria sasa kuwa historia nchini mwaka 2030

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKATI ugonjwa wa malaria ukitajwa kuongoza kwa vifo duniani, wabunge wa Tanzania walioko kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa huo, wametoa kauli ya matumaini kuwa hadi kufikia mwaka 2030 tatizo hilo litakuwa limetokomezwa kabisa.

Kauli hiyo ya kuleta matumaini ilitolewa juzi na Umoja wa Wabunge walio katika vita dhidi ya malaria na Magonjwa ya Ukanda wa Joto Yasiyopewa Kipaumbele (Tapama), kupitia Katibu wake, Dk. Raphael Chegeni, wakati akikabidhi mpango mkakati wa kutokomeza malaria nchini kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainab Chaula.

Katika semina hiyo ya siku mbili iliyofanyika mwishoni mwa wiki, iliyojumuisha wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya malaria, Dk. Chegeni alisema wameanza juhudi ya utekelezaji wa mpango wa kutokomeza malaria ifikapo mwaka 2030.

Dk. Chegeni alisema mpango mkakati huo unalenga kuwakumbusha wabunge kuwajibika katika kujua takwimu za vifo na wagonjwa walioko kwenye majimbo yao.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Tapama, Riziki Lulida, alisema wameandaa mpango mkakati huo baada ya kuona vifo vingi kwa wajawazito na watoto waliopo chini ya miaka mitano.

"Tulikaa chini tukaona hakika tunapoteza kizazi kinachotegemewa hapo baadaye hasa katika mikoa ya minne yenye mzigo mkubwa wa ugonjwa huu ambayo Kigoma, Geita, Kagera, Lindi na Mtwara," alisema Lulida.

Naye Mwenyekiti wa Marais Wastaafu na Viongozi wa Juu wa Afrika wa (Alma), Joyce Kasonabo, alisema malengo ya Alma ni kuweka kipaumbele kwa ugonjwa huo wa malaria unatokomezwa kisera na kimataifa.

Alisema ugonjwa huo hauwezi kutokomezwa na mtu mmoja mmoja, hivyo jitihada za makusudi zinahitajika.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainabu Chaula, akipokea mpango huo wa kutokomeza malaria alisema kila mmoja ana nafasi yake kuhakikisha anatokomeza ugonjwa huo.

Alisema ugonjwa huo upo na umekuwa tishio kwa kuua nguvu kazi ya taifa. Aliongeza kuwa serikali kupitia Wizara ya Afya imefanikiwa kutokomeza ugonjwa huo kutoka asilimia 14.4 mpaka asilimia 7.3.

## HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Nangoo, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, ambaye ni diwani wa kata hiyo, Mohamedi Chilumba, akizungumza na wananchi (hawapo pichani) jana, katika kikao cha mwendelezo wa ujenzi wa bweni la Shule ya Sekondari ya Nangoo, ambapo awali diwani huyo alichangia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya kuanza ujenzi huo. **PICHA, HAMISI NASIRI**

# Kanyasu afunda wazazi wahitimu la 7

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini, Constantine Kanyasu, amewahimiza wazazi wa wanafunzi waliomaliza darasa la saba mwezi huu wahakikishe hawajiingizi katika makundi yasiyofaa.

Akizungumza kwenye mahafali ya saba ya wanafunzi wa darasa la saba yaliyofanyika katika Shule ya Msingi ya Waja Springs ya mkoani Geita, Kanyasu aliwataka wazazi wawe mstari wa mbele katika malezi ya watoto wao.

Aidha, Kanyasu amewataka wanafunzi hao wakawe mfano bora katika jamii kwa kuwa kuwasaidia wazazi wao kwa kufanya kazi majumbani badala ya kuacha kazi zote zifanywe na wafanyakazi wa ndani.

Katika hatua nyingine, Kanyasu ameipongeza shule hiyo kwa kufanya vizuri katika mitihani ya Taifa na kuufanya mkoa wa Geita kuwa miongoni mwa mikoa inayokuwapo kwenye tano bora.

Pia amewataka wanafunzi hao watumie muda mwingi kujisomea vitabu vya hadithi badala ya kutumia muda mwingi kuangalia televisheni hasa vipindi visivyofaa.

Katika hatua nyingine, Kanyasu amehakikishia uongozi wa shule hiyo kutafuta ufumbuzi wa tatizo la barabara inayoelekea katika shule hiyo pamoja tatizo maji machafu wakati mvua ikinyesha. Meneja wa Shule hiyo, Chacha Wambur, aliwaasa wazazi wajiepushe kuwapatia simu watoto wao ili wasiweze kuingia katika vishawishi.

"Wazazi jiepusheni kuwapa simu zenu hawa watoto, hii mitandao ya kijamii inawapelekea watoto kuanza kuangalia mambo yasiyofaa," alisisitiza Wambura.

Aliwataka wahitimu hao waache kuzitumia simu za wazazi wao pindi wakiwa majumbani badala yake wasome vitabu kama walivyokuwa wakifundishwa shuleni.

Naye Janeth Ndibalema, mzazi wa mhitimu wa darasa la saba, alisema malezi ya watoto kwa sasa yamekuwa na changamoto nyingi kutokana na wazazi kuacha jukumu la malezi kwa wasichana wa kazi hali inayopelekea watoto wengi kuharibikiwa.

# Teknolojia mpya kuleta uhakika chakula mifugo

**Na Futuna Seleman, TANGA**

TEKNOLOJIA mpya ya kisasa ya uzalishaji wa malisho kwa ajili ya mifugo iliyofanyiwa utafiti wa kisayansi, imethibitishwa ikitumiwa kikamilifu na wafugaji nchini itamaliza changamoto ya ukosefu wa chakula cha mifugo kwa mwaka mzima na kupunguza migogoro kati yao na wafugaji.

Aidha, matumizi ya teknolojia hiyo yataongeza kasi ya uzalishaji itokanayo na bidhaa zitokanazo na mifugo ikiwamo maziwa.

Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Tanga, ambaye ni mtafiti mbobezi katika tafiti za mifugo teknolojia na usambazaji wake, Dk. Zablon Nziku, aliyasema hayo wakati wa ziara ya waandishi wa habari waliotembelea shamba la mfano la kituo hicho jijini Tanga, baada ya mafunzo ya siku mbili yaliyoandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Costech).

Ziara hiyo ya siku mbili ilitanguliwa na mafunzo yaliyowakutanisha wanahabari kutoka Tanga, Pwani na Morogoro yaliyoandaliwa na Costech, lengo kushirikiana katika kuuhabarisha umma juu ya matokeo ya utafiti nchini.

Nziku alisema shamba la mfano la uzalishaji wa malisho ya majani aina ya nyasi na mikunde kwa ajili ya mifugo litawasaidia wafugaji kununua mbegu kwa bei elekezi ya serikali ya Sh. 4,000 kwa kilo.

"Malisho ya majani hufanya mifugo kuwa na afya bora na kuongeza uzalishaji wa maziwa, wafugaji wengi wanakuja kuulizia mbegu ya malisho ya majani haya yanaleta tija sana tunaomba wengine waje hapa kituoni wanufaike nayo," alisema.

Aidha, alisema wataalamu wao hawako nyuma katika kuwasaidia wafugaji namna ya kupanda kwa ubora aina hiyo ya malisho ambayo inafaa kwa maeneo mengi yenye ukame.

Hata hivyo, alisema teknolojia hiyo itaendelea kwenye kanda nyingine nchini.

"Oda nyingi sana, wengi wameanza kulima na kupanda malisho bora na wanawauzia wengine malisho ni chanzo kikubwa cha uzalishaji," alisema.

Aliwashauri wananchi kabla ya kuanza ufugaji wahakikishe wanapata wapi malisho ya mwaka mzima.

Ofisa Utafiti Mkuu Kiongozi kutoka Costech, Dk. Bakari Msangi, alishauri watafiti kushirikiana na vyombo vya habari ili matokeo ya utafiti wao uwafikie wananchi, kwa vile Costech imekuwa ikitumia fedha nyingi kuziwezesha taasisi za utafiti kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa maabara za kisasa kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Aidha, aliwataka wanahabari nchini kujikita kwenye uandishi wa habari za utafiti ili kuielimisha jamii kuhusiana na mambo mbalimbali hususani katika kuelekea katika uchumi wa viwanda.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Taifa Stars msisubiri penalti kwa Wasudan

**BAADA** ya kufanikiwa kutinga hatua ya makundi kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar 2022, timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), itashuka tena dimbani Ijumaa wiki hii kuikaribisha Sudan.

Katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam ni ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.

Stars itashuka dimbani ikiwa na ari ya kuendelea kufanya vizuri baada ya wiki moja iliyopita kuitupa nje Burundi katika uwanja huo kwenye mechi ya kuwania kufuzu hatua ya makundi kwa ajili ya kusaka tiketi fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar 2022.

Hata hivyo, kwa Stars pia itataka kuendelea kufanya kweli katika mechi hiyo ya kuwania kufuzu michuano hiyo ya CHAN itakayofanyika mwakani nchini Cameroon, baada ya kuitoa Kenya, Harambee Stars kwenye mechi ya awali.

Kama ilivyoanzia nyumbani dhidi ya Harambee Stars, ndivyo ilivyo tena wakati huu ikiingia kambini leo kujiandaa kuivaa Sudan. Hivyo, Stars inapaswa kufanya maandalizi makubwa yatakayoiwezesha kupata ushindi mkubwa nyumbani ili kuondoa kucheza kwa presha katika mechi ya marudiano.

Hatutaki kuona tena Stars ikilazimika kucheza kwa presha kubwa katika mechi ya marudiano na kuwaweka Watanzania roho juu kama ilivyokuwa dhidi ya Harambee Stars na baadaye ilipoivaa Burundi.

Katika mechi ya Harambee Stars, Taifa Stars ililazimishwa sare tasa nyumbani kabla ya kwenda kupata matokeo kama hayo ugenini na hatimaye kuitoa kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 4-1.

Hali hiyo ilijirudia tena ilipokutana ugenini dhidi ya Burundi kwa kutoka sare ya bao 1-1 kabla ya hapa nyumbani kupata matokeo kama hayo na hatimaye kuwatupa nje Warundi hao kwa mikwaju ya penalti 3-0.

Matokeo ya mechi hizo mbili ni wazi licha ya Stars kuvuka kwa mikwaju ya penalti, ililazimika kucheza kwa presha kubwa kutokana na kushindwa kumaliza mchezo kwenye mechi ya awali.

Tunatambua wazi Sudan si timu rahisi na ni bora zaidi ya Stars hata kuliko wapinzani hao wawili ambao imewatoa, Burundi na Harambee Stars, hivyo haitakiwi kufanya makosa kwenye mechi ya awali nyumbani Ijumaa wiki hii.

Kinachotakiwa kwa Stars si tu kuhakikisha inapata matokeo nyumbani, bali pia kuwa makini kwa kwa kutokubali kuruhusu bao nyumbani huku ikihakikisha inapata ushindi wa kishindo.

Kuruhusu mpinzani wako kupata bao la ugenini kunakufanya kubeba mzigo mzito katika mechi ya marudiano, hivyo Watanzania wanachotaka kukiona si tu kushinda bali kushinda kwa kishindo na kutoruhusu nyavu kutingishwa.

Tunaamini hilo linawezekana hasa kutokana na kujenga kujiamini kwa wachezaji wa Stars katika mechi hizi mbili ilizocheza dhidi ya Harambee Stars na Burundi. Lakini pia ubora wa Stars inaouonyesha pindi inapokuwa uwanja wake wa nyumbani mbele ya mashabiki wake unazidi kutupa matumaini ya kufanya vizuri.

Hivyo, kinachotakiwa ni kuhakikisha inapata ushindi wa mabao mengi ili kutocheza kwa presha mechi ya marudiano ugenini lakini pia mashabiki wakijitokeza kwa wingi Uwanja wa Taifa Ijumaa kwenda kutimiza wajibu wao wa mchezaji wa 12 uwanjani kwa kuishangilia.

Kwa upande wa mashabiki hawana budi kushangilia mwanzo mwisho na si kusubiri hadi bao lifungwe, lakini pia kila mpinzani anapogusa mpira kumzomea jambo ambalo tunaamini litakuwa msaada mkubwa kwa Stars kuibuka na ushindi katika mechi hiyo muhimu kwao kushinda.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Yanga itafute dawa ya kutoshinda nyumbani

Na Adam Fungamwango

**NI** mechi ya pili mfululizo Yanga imeshindwa kupata ushindi nyumbani kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika.

Jumamosi iliyopita ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Zesco ya Zambia ikiwa ni baada ya mechi ya hatua za awali, kupata sare kama hiyo dhidi ya Township Rollers ya Botswana. Hata hivyo ilikwenda kushinda bao 1-0 ugenini.

Hii inaonyesha kuwa Yanga ina matatizo ya kupata ushindi ikiwa nyumbani, mbele ya mashabiki wake. Vyovyote itakavyokuwa, ishinde tena ugenini, au itolewe, lakini benchi la ufundi la Yanga linapaswa lilifanyie kazi suala hili la kushindwa kupata matokeo nyumbani.

Vinginevyo Yanga inaweza kuwa na changamoto kubwa hata kama itatinga hatua ya makundi. Kwenye hatua hiyo kunakuwa na timu ngumu, ambazo nyingi lengo lao kubwa ni kushinda nyumbani na kutafuta sare ugenini.

Kama timu haishindi nyumbani kwenye hatua ya makundi, basi kuna hatari ya kushika hata mkia. Kwenye makundi hata timu kubwa kama Al Ahly inakuwa ngumu kushinda ugenini, lakini ikitegemea zaidi kushinda nyumbani.

Tuliona msimu uliopita kwenye kundi ililokuwa klabu za Simba, AS Vita, Saoura na Al Ahly, hakuna timu yoyote iliyoshinda ugenini. Kila mtu alishinda kwake, hivyo Yanga isitegemee kuwa hata ikifanikiwa kuingia hatua ya makundi kama haikushinda nyumbani itakuwa salama.

Na kama ikitolewa na Zesco, bado Yanga itakuwa na nafasi ya kutupwa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho. Kwenye michuano hiyo, kuna mechi moja ya mchujo kabla ya kuingia kwenye makundi.

Hii yote inaonyesha kuwa Yanga bado ipo ipo sana kwenye michuano ya kimataifa, hivyo inabidi itafute dawa ya kuwa inashinda mechi zake za ugenini na kuacha kutegemea kushinda ugenini kama ilivyofanya kwa Township Rollers, kitu ambacho wakati mwingine hakiwezi kuja mara mbili au kujirudiarudia.

> **Kama timu haishindi nyumbani kwenye hatua ya makundi, basi kuna hatari ya kushika hata mkia. Kwenye makundi hata timu kubwa kama Al Ahly inakuwa ngumu kushinda ugenini, lakini ikitegemea zaidi kushinda nyumbani.**

Kinachoonekana ni kwamba, Yanga bado ina matatizo kwenye safu ya ushambuliaji, hivyo kama itafanikiwa kupita kwenye hatua ya makundi, ambapo inaruhusiwa kuongeza wachezaji, itafute mastraika au straika mmoja mwenye kiwango cha hali ya juu ambaye anaweza kuifanya iwe na uwezo wa kupata mabao ikiwa nyumbani.

Pengo la Heritier Makambo bado lipo, na sasa linaonekana dhahiri kwa mashabiki wote. Nadhani Yanga ilimuuza straika huyo bila ya kuwa kwanza imetafuta mbadala sahihi na hiki ndicho kinachowatesa. Hata huyu aliyopo sasa, David Molinga ambaye bado hajapata leseni, sidhani kama anaweza kuwa muarobaini wa timu ya Yanga kushinda mechi zake za nyumbani.

Kocha Mwinyi Zahera akumbuke kuwa kwenye michuano mikubwa kama hii ya Afrika, si tu kwamba timu inatakiwa ishinde nyumbani, lakini pia kwa mabao mengi, hivyo afanyie kazi mapungufu haya.

Katika michuano hii, Yanga imekuwa ikishinda kwa penalti na jambo ambalo ni hatari kwao kuweza kusonga mbele kama mastraika watashindwa kutumia vema nafasi wanazozipata.

Aidha, wakati huu wakijiandaa kwa mechi ya marudiano ugenini dhidi ya Zesco, wachezaji hawana budi kuandaliwa kisaikolojia zaidi ili kuweza kuihimi presha kwa wapinzani wao ambao wanajivunia rekodi ya kutopoteza hata mechi hata moja ya kimataifa wakiwa kwenye Uwanja wao wa nyumbani wa Levy Mwanawasa.

Kikubwa zaidi ni Zahera sasa kutafuta njia mbadala ya timu kupata mabao hususan kuwaandaa wachezaji wa nafasi ya kiungo na mabeki, kujaribu kupiga mashuti ya mbali, kwani ni wazi safu ya ushambuliaji inaonekana kuwa butu kwa sasa.

## BARUA & MJADALA

# Tunalihitaji daraja tulilolichangia

***Mhariri***

*MIMI ni mmoja kati ya wananchi wanaozikubali sana jitihada za Rais John Magufuli ya kuchapa kazi ili kujiletea maendeleo kama mtu mmoja mmoja, lakini na kwa ustawi wa taifa la Tanzania kwa ujumla wake.*

*Aidha, ni miongoni mwa Watanzania walio wengi ambao wanaikubali sana dhana ya wananchi kuchangia maendeleo ya eneo lao pale walipo, kwa kushiriki kwenye miradi mbalimbali ya kujitolea nguvu kazi ama kuchangia fedha.*

*Ninafanya hivyo kwa sababu michango kama hiyo huwa ina faida za moja kwa moja kwetu sisi wananchi au hata kama si ya moja kwa moja, ina faida zake kwa mgongo wa nyuma kwa maana ya ama watoto na wajukuu wetu, kama siyo kwa jirani zetu.*

*Kunapokuwa na changamoto kwa mfano ya barabara ambayo wananchi wana uwezo wa kuilima au ya daraja ambalo wananchi wanaweza kubeba mawe au kuchangia kidogo fedha ili daraja la kuwasaidia liweze kujengwa, basi mimi huwa niko mstari wa mbele kushiriki.*

*Na ndiyo maana nimeshiriki kwa mapana sana katika kutoa michango mbalimbali iliyohusu kuchangia ujenzi wa zahanati katika kijiji chetu au ujenzi wa madarasa, nikielewa fika kuwa huo ni wajibu wa msingi kufanya.*

*Hata hivyo, Mhariri ninapokuja kupinga au kutokubaliana na aina hii ya uchangiaji wa nguvu kazi ama fedha kutoka kwa mwananchi ni pale ambapo michango hiyo inapoishia hewani, bila kutekeleza kilichokusudiwa.*

*Na ndicho kilichonifanya leo hii niandike barua hii kwako Mhariri, nikiwa mkazi wa Kinondoni Mashariki, Kata ya Mabwepande, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam.*

*Mimi pamoja na wakazi wenzangu wa wa Kinondoni Mashariki, tulichangia Sh. 70,000 kila kaya kwa ajili ya ujenzi wa daraja litakalorahisisha usafiri katika eneo la Mji Mpya.*

*Sasa hadi miaka imepita, na daraja hatuoni likijengwa huku viongozi wetu, kwa maana ya mwenyekiti wetu wa mtaa pamoja na diwani wetu wa Kata ya Mabwepande, wakiwa kimya kama vile hakuna kitu kilichofanyika.*

*Mhariri, hapa ndipo ninapokuja kupingana na aina hii ya uchangiaji kwa sababu tunapochanga kwa ajili ya maendeleo yetu, inapaswa tulichochangia kionekane na si vinginevyo.*

*Ninaomba basi kupitia kwako wahusika watueleze fedha zetu zilipo kwa kuwa hatuoni daraja likijengwa na tatizo bado lipo.*

***Mkazi Kinondo Mashariki, Dar***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Tusiilazimishe TFF, Taifa Cup imepitwa na wakati




**Na Adam Fungamwango**

**WAKATI** Shirikisho la Soka nchini (TFF), likisaini mkataba wa miaka minne na Azam Media kwa ajili ya kuonyesha moja kwa moja mechi za timu ya Taifa, Taifa Stars pamoja na Kombe la Shirikisho, maarufu kama FA Cup, Rais wa Shirikisho hilo, Wallace Karia, alisema haoni sababu ya kuwapo kwa Taifa Cup.

Mashabiki wengi wa soka wa sasa hawaijui michuano hiyo, iliyokuwa maarufu na kutia fora sana enzi hizo. Taifa Cup ni michuano ya zamani ambayo ilikuwa ikizishirikisha timu za mikoa yote ya Tanzania.

Sifa ya michuano hii ilikuwa ikizalisha wachezaji wengi ambao ilikuwa si rahisi kuonekana kwa sababu za kijiografia.

Wachezaji hao walikuwa wakitoka vijijini kabisa ambapo kwa hali ya kawaida, isingewezekana kuwaona na kuwapa mafunzo kabla ya kuwa mastaa wakubwa.

Wachezaji wengi waliotokea kuwa mastaa wakubwa nchini, walitokea kwenye michuano hii kwa uchache ni Mohamed Chuma, Edibilly Lunyamila, Ahmed Amasha, Ibrahim Marekano na wengine wengi ni zao la michuano hiyo.

Urahisi wa kuonekana kwa wachezaji hao ulikuwa ni mkoa unatafuta wachezaji wenye vipaji kutoka pembe hadi pembe ya mkoa, wahusika wakifika hadi kwenye vijiji ambavyo havifikiki kwa urahisi, wanawachukua na kuunda timu ya mkoa.

Mara nyingi michuano hii ilikuwa ikifanyika Dar es Salaam. Timu zote za mikoa zilikuwa zikikutana Dar na uwanja mkubwa uliokuwa ukitumika ni Ilala ambao baadaye ukaitwa Karume.

Wachezaji waliokuwa wakionekana kuwa na vipaji vya hali ya juu na uwezo mkubwa, hawakurejea tena kwenye mikoa yao, kwani klabu za Dar es Salaam, Simba, Yanga Cosmopolitan, Sigara, Pilsner, Nyota Nyekundu, Pan Africa ziliwanyakua.

Kutokana na kumbukumbu hiyo, mashabiki wengi hasa wa kizazi cha enzi hizo walipendelea mfumo huo urudi tena, wakiwa na maana michuano hiyo irudishwe ili vipaji kama hivyo ambavyo bado vimezagaa vijijini vionekane na kuibuliwa.

Karia akasema kuwa imepitwa na wakati. Lakini kauli hiyo ikaonekana kupingwa na wadau wengi wa soka.

Kwangu mimi pia naona ni kweli imepitwa na wakati. Mfumo huo ulikuwa mzuri kipindi kile ambako nchi ilikuwa kubwa. Nina maana kuwa kulikuwa hakuna miundombinu kama vile barabara nyingi za lami, pamoja na mawasiliano ya simu, hasa za mkononi.

Ni kwamba leo hii Tanzania inafikika hadi vijijini, pia kuwapo mawasiliano kunafanya mchezaji hata akiwa kijijini watu kujua na kufika haraka kukiokoa kipaji chake.

Kwa sasa kipaji cha mchezaji ni pesa, tofauti na zamani soka lilikuwa ni la ridhaa, hivyo hakuna mtu anayeweza kukiacha kipaji kiozee kijijini na wakati anajua hata akitumia gharama zake kukipeleka mkoani au mjini ni lazima apige pesa.

Hata wazazi kwa sasa wamekuwa na mwamko, imefikia wakati kuwa hakuna mzazi anayeweza kukiacha kipaji cha soka cha mtoto wake kife kijijini, badala yake atafanya kila mbinu hata kwa kumpeleka kwa ndugu yake mjini, atafutiwe timu ili mtoto aonekane.

Michuano ya Taifa Cup ilikuwa na tija pale timu ya mkoa husika ikichezesha wachezaji waliotoka kwenye mkoa huo tu.

Lakini ilianza kupoteza maana timu za mikoa zilipoanza kuchezesha hata wachezaji ambao hawatoki kwenye mikoa hiyo.

Mbali zaidi viongozi wa timu za mikoa wakaanza sasa kutotafuta vipaji vijijini na badala yake kuchezesha mastaa.

Mfano timu ya mkoa wa Mbeya, Mapinduzi Stars inakuwa ni kombaini tu ya wachezaji wa Mbeya City na Prisons, hivyo kupoteza maana nzima ya michuano hiyo.

Timu ya Dar es Salaam Mzizima United, sasa ikawa kama Taifa Stars kwa kukusanya wachezaji mastaa kutoka Simba, Yanga, Pan Africa na nyinginezo.

Mwishoni mwa miaka ya 80' kukawa na mikakati ya kuiboresha kwa kuwapiga marufuku wachezaji wanaocheza Ligi Kuu kucheza michuano hiyo, lakini baada ya kuona labda haitokuwa na msisimko, wakaruhusu wachezaji wasiozidi watano. Na hata hivyo haikufua dafu, hadi ilipokufa kifo cha asili.

Kwa mlolongo huo wote nilioainisha hapa, hata mimi kwa sasa sioni umuhimu wa michuano hiyo, kwani kwa sasa kuna vituo vingi vya 'Akademi' tofauti na zamani, lakini pia kwa sasa ambapo teknolojia inaifanya dunia kuwa kama kiganja, sidhani kama kutakuwa na kipaji kwenye kijiji chochote nchi hii kishindwe kufahamika na kufanyiwa kazi.

Tuendelee na michuano mingine kama ya watoto na vijana na kuachana na michuano ambayo ni kweli wakati wa nyuma ilikuwa na tija, lakini kwa sasa imepitwa na wakati.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Upanuzi wa gati bandarini wakamilika

Na Enock Charles

SERIKALI imesema ujenzi wa gati namba 0 iliyopo Bandari ya Dar es Salaam jijini Dar es Salaam umekamilika, na kwamba itakuwa na uwezo wa kuhudumia magari 600,000 kwa mwaka, kutoka 150,000 ya awali.

Imesema kukamilika kwa gati hiyo kutaiwezesha Bandari ya Dar es Salaam kuongezea uwezo wa kupokea shehena ya mizigo kutoka tani milioni 17 hadi tani milioni 25 kwa mwaka, ifikapo mwaka 2021.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isaack Kamwelwe, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kufanya ziara ya ukaguzi katika gati hiyo.

Waziri Kamwelwe alisema kuboreshwa kwa miundombinu hiyo kutawezesha pia nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kupata huduma za usafiri kwa urahisi na kushiriki katika shughuli za kibiashara na kiuchumi.

"Gati hilo mnaloliona lina uwezo wa kuhudumia magari 600,000 na meli ya kwanza iliyobeba mzigo mkubwa wa magari imepokelewa juzi na kuna nyingine inakuja, kuimarika kwa miundombinu hii kutawezesha ushirikiano rahisi wa kibiashara na kiuchumi baina ya nchi wanachama wa SADC," alisema Waziri Kamwelwe.

Alisema gati hiyo imejengwa kwa miaka miwili na ina urefu wa mita 320 na upana wa mita 40, huku likiwa na uwezo wa kubeba magari 10,000 na yadi yenye uwezo wa kuegesha magari 90,000, itakuwa ikifanya kazi kwa saa 24.

Wakati huo huo, Waziri Kamwelwe alizungumzia mkutano wa mawaziri wa SADC unaotarajia kufanyika jijini Dar es Salaam, alisema serikali imeingia makubaliano na baadhi ya nchi wanachama wa SADC katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga, kwamba Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) litafanya safari zake katika nchi za Comoro, Afrika Kusini, Zambia na Zimbabwe kwa utaratibu uliokubaliwa na Mamlaka ya Anga ya nchi wanachama wa jumuiya hiyo.

Alisema katika kuboresha ushirikiano wa nchi wanachama wa SADC wamekubaliana kuwa na mpango wa pamoja wa kuwa na programu ya vipindi kitakachoitwa 'eye on SADC' kwa madhumuni ya kuhabarisha nchi wanachama kuhusu Sera, mipango na mikakati ya umoja huo, kitakachorushwa kwenye televisheni za nchi wanachama.



Meneja Mwandamizi wa Huduma za Kibenki kwa Taasisi, Dorah Monyo, akikabidhiwa tuzo na Jumuiya ya Wakorea waishio nchini, Yum Yunhwa, baada ya Benki ya NMB kudhamini tamasha la Korea 2019 lililofanyika jijini Dar es Salaam. NMB walidhamini tamasha hilo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wasimamizi ardhi waonywa kukwaza fursa za uwekezaji

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WASIMAMIZI wa masuala ya ardhi na uwekezaji wilayani Bukoba mkoani Kagera, wametakiwa kutokuwa vikwazo kwa wawekezaji wanaohitaji huduma ya kuwekeza miradi mahali popote.

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa Baraza la Biashara wilayani humo, ambaye ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Deodatus Kinawilo, alipokuwa akizindua Baraza la Wafanyabiashara wa Sekta Binafsi na Umma.

Kinawilo alisema katika wilaya hiyo kuna maeneo ya kutosha kufanya shughuli za kiuwekezaji kama viwanda, kilimo na ufugaji.

Alisema fursa zinazopatikana ni chachu kubwa na zitumike kupanua uchumi wa nchi kwa kushirikiana na wawekezaji wanaotoka ndani na nje ya mkoa na hata nje ya nchi.

Aidha, Kinawilo alisema, lengo la kufungua baraza hilo ni kuibua fursa zilizopo kwa kutumia wawekezaji na kufanya uchumi wenye uhakika kwa walio tayari kuwa waaminifu na wenye kutekeleza wajibu na kukuza kipato cha taifa.

Aliongeza kuwa tayari waraka namba 1 wa mwaka 2001ulitolewa na Rais John Magufuli wa uanzishaji mabaraza ya wilaya na mikoa yenye kujadili fursa ambazo zitasaidia uchumi kusonga mbele na kufikia dira ya Taifa kwa 2020-2025.

Ofisa Mipango, Takwinu na Ufuatiliaji, Richard Mihayo, alisema Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba imebainisha fursa zinazopatikana ambazo zinategemewa kuongeza mapato ya kiuchumi.

Mihayo alisema shughuli za usafirishaji, kilimo, ufugaji, elimu, afya na viwanda ni mambo ambayo yatafanywa kwa kuongeza thamani kupitia malighafi zitokanazo na ufugaji na kilimo kwa kuongezwa thamani.

"Kwa upande wa ufugaji, kilimo na uvuvi kuna ufugaji ambao ujenzi wa machinjio ambao utapaki nyama kuza, kuuza kwato, uuzaji wa dagaa samaki, kuku kilimo mazao ya matunda, maparachichi, chips za ndizi," alisema Mihayo.

Mwekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) mkoa wa Kagera, Faustine Mugenyi, alisema baraza hilo linaweza kuwaweka pamoja na kukubaliana na mabadiliko, na kuanza kuwekeza katika maeneo yaliyoko wazi.

## Kasoro nane kanuni uchaguzi S/Mitaa

INATOKA UK. 2

katika halmashauri husika.

Alisema fomu za matokeo hazina nafasi ya kutaja jina la kituo cha kupigia kura, fomu za uteuzi hazibainishi au kutambua watu wenye ulemavu walioonesha nia ya kugombea nafasi za uongozi, fomu za mpigakura hazina picha ya mgombea, hali hiyo inaweza kuleta ugumu wa utambuzi wa mpigakura kuchagua mgombea anayemtaka hasa kwa mpigakura asiyejua kusoma na kuandika.

**MAPENDEKEZO**

Alisema wanapendekeza waziri mwenye dhamana kuzielekeza mamlaka husika kufanya maboresho katika fomu za uteuzi, upigaji kura na matokeo ya uchaguzi kutaja jina la kituo la kupiga kura.

"Tunapendekeza wadau wa uchaguzi wa serikali za mitaa watoe msaada na ushirikiano ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanashiriki kikamilifu katika uchaguzi na sanduku la kupigia kura liwekwe mahali ambapo watu wenye mahitaji maalum wanaweza kulifikia kwa urahisi," alisema Kabisama.

Aidha, alisema wanapendekeza mamlaka za uchaguzi, msimamizi wa uchaguzi, msimamizi msaidizi wa uchaguzi na msimamizi wa kituo watoe msaada na ushirikiano ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanashiriki kikamilifu katika uchaguzi.

Pendekezo lingine ni kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (Tamisemi) kukasimu mamlaka ya kutoa vibali vya kuangalia uchaguzi na kuendesha elimu ya mpiga kura kwa msimamizi wa uchaguzi ngazi ya halmashauri.

Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa wanapendekeza pia baada ya uchaguzi, waziri mwenye dhamana azielekeze halmashauri zote nchini kuandaa na kutoa taarifa ya uchaguzi wa serikali za mitaa kwa umma ikiainisha pamoja na masuala mengine upigaji kura, matokeo, ushiriki wa makundi maalum kama vijana, wanawake na walemavu.

## Lipumba awapa majukumu makatibu

INATOKA UK. 3

kujiandikisha na hatimaye kupata fursa ya kupiga kura ni tatizo, na kwa hakika ni utaratibu unaopora haki za kisiasa kwa maana ya kupiga au kupigiwa kura," alisema.

Alisema kama Rais alionyesha wasiwasi wake juu ya usajili wa line za simu kufanyika kwa kutumia vitambulisho vya Taifa kwa kuwa havijakamilika kwa Watanzania, basi hata vitambulisho vingine vilivyotajwa kuwa vitatumika kwenye uchaguzi huu wa mitaa vinakumbana na changamoto hiyo hiyo, na kwamba kama hali ndio hiyo, basi wataoshiriki kwenye kuchagua viongozi wa serikali za mitaa watakuwa ni wachache sana.

Alisema CUF inamtaka Waziri wa Tamisemi kutoa fursa kwa wananchi kuchagua viongozi wanaowataka kwa kuondosha vikwazo vinavyotishia kupunguza idadi ya wapigakura.

Prof. Lipumba aliitaka Tamisemi kuweka orodha ya mitaa, vijiji na vitongoji kwenye tovuti yake ili kurahisisha vyama vyenye uwezo wa kuchukua taarifa hizo na kuzifanyia kazi.

HABARI MIKOANI

# Mtanzania aibuka mhitimu bora udaktari nchini Cuba

**Na Beatrice Moses**

IRENE Mageni ameng'ara kwenye matokeo ya mitihani yake ya kuhitimu masomo ya udaktari nchini Cuba na kwa miongoni mwa wachache waliotunukiwa tuzo.

Hatua hiyo imewavutia waliosoma katika Sekondari ya Wasichana Rugambwa kumwandalia hafla ya kupongeza mwishoni mwa wiki iliyopita.

Miongoni mwa wanafunzi wa taaluma hiyo 466 wageni kutoka katika mataifa mbalimbali duniani waliokuwa wanasoma, Irene ambaye Cuba tayari inamtambua kama daktari alikuwa miongoni wahitimu sita bora.

Akizungumza na gazeti la Nipashe alieleza kuwa anafurahi kwa kuwa anaamini kuwa matokeo hayo mazuri aliyoyapata katika Latin American School of Medicine yatawavutia na kuwapa chachu wanafunzi wengine hasa wa kike kusoma kwa bidii ili kutimiza ndoto zao.

"Hii ilikuwa ni kazi ya ndoto yangu, hatimaye imetimia, nakumbuka ningali mdogo, nakumbuka nilikuwa navutiwa zaidi kutazama kipindi cha afya ya jamii na msalaba mwekundu vyote vilikuwa vikirushwa ITV," alisema.

Aliishukuru serikali kutokana na ushirikiano aliokuwa akiupata kupitia Wizara ya Elimu, kwa kuwa licha ya kuwa alipata nafasi ya kwenda kusoma nchini Cuba mwaka 2012 kwa ufadhili wa taasisi ya Fidel Castro, lakini bado alilazimika kuomba mkopo wa elimu ili kufanikisha mahitaji yake muhimu.

Alisema amerejea nchini anatamani kuungana na wanataaluma wenzake katika kuhakikisha huduma za afya zinatolewa ipasavyo ili kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na jamii yenye afya kwa maendeleo ya jumla.

"Nipo kwenye mchakato wa kuhakikisha ninakamilisha taratibu za kutambulika nchini kwa kufanya mafunzo ya vitendo kwa mwaka mmoja, baada ya hapo niweze kutafuta ajira, naamini nitatumia elimu niliyoipata vyema ikiwamo kusaidia baadhi ya wanajamii kuacha kuamini masuala ya ushirikina na kutambua umuhimu wa tiba sahihi," alisema Dk. Irene.

Anabainisha kuwa amebaini kuna baadhi ya watu wamekuwa wakichelewa kwenda hospitali kutibiwa wanapougua, badala yake wamekuwa wakiamini kuwa wamerogwa, hivyo kuamua kuzunguka kwa waganga wa jadi licha ya magonjwa wanayougua wangeweza kutibiwa na kupona wangewahi kwenda kufanyiwa vipimo sahihi.

Dk. Magdalena Ngaiza mmoja wa walezi wa Taasisi ya Rugambwa Girls Foundation (RGF), ambaye ni Mhadhiri mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema ni jambo lenye kuleta furaha kujumuika kufurahia matokeo yenye thamani.

"Tumeona tunaweza kutumia muda wetu kumpongeza kwa hatua hii ya mafanikio ya kujivunia, ambayo kwa namna nyingine yanasaidia kutoa changamoto kwa stereo type, huyu ana nafasi nzuri ya kuzungumza na wasichana wengine ili kuwajenga katika ushindi," alisema Dk. Ngaiza.

Alisema RGF imekusanya wahitimu sekondari hiyo tangu mwaka 1968, ambapo pamoja na mambo mengine imekuwa ikijishughulisha katika kuhakikisha inakuwa mstari wa mbele kuhakikisha inashiriki kikamilifu katika kufanikisha vijana hasa wa kike kufanya vyema kwenye masomo yao ili kuleta chachu ya maendeleo kwenye jamii.

"Tunafurahi tunapoona watoto wetu wanafanya vizuri, huyu siyo wa kwanza wapo kadhaa wengine tayari wameajiriwa sehemu mbalimbali, lakini pia wapo wanaofanya vyema kwenye mitihani ya elimu ya msingi na sekondari," alisema.

Mama mzazi wa Irene, Dorothy Magesse ambaye ni mhitimu wa Rugambwa, alieleza kuwa anajisikia furaha kuona mtoto wake ametimiza ndogo ya kuwa daktari.

"Wazazi jukumu letu kuhakikisha tunawapa moyo watoto wetu kwa kuhakikisha tunawawezesha, tunawashauri ili kuwasaidia kufanikisha kupata elimu ili waweze kutimiza ndoto za kufanya kazi wanazozipenda, kwa kuwa watakuwa wanafanya kazi hizo kwa bidii hivyo kutakuwa na mafanikio kwa nchi na jamii," alisema.

Dorothy ambaye ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Nutrition and Social Inclusion, alisema anashukuru kwa upendo na ushirikiano baina yao ambao waliujenga na kuimarisha kupitia kundi la whatsApp.

Mwanakikundi wa RGF ,mtaalam wa masuala ya taarifa za teknolojia (IT), Leona Katakwesa, aliishauri jamii kuwa na matumizi mazuri ya mitandao.



Irene Mageni akifurahia baada ya kukabidhiwa tuzo ya kuwa mwanafunzi bora wa udaktari nchini Cuba, mwishomi mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: BEATRICE MOSES**

## Shirika, wahariri kukuza vipaji vijana

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Vijana (TAYOA), limekubaliana na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari kuibua vipaji vya vijana naa kuwahamasisha kujitegemea na kujifunza kutoka kwa wenzao waliofanikiwa katika mazingira magumu zaidi wanayoishi.

Hayo yaliafikiwa baada ya wahariri kutembelea Makao Makuu ya Shirika la TAYOA Bahari Beach Dar es Salaam, kujifunza kazi mbalimbali zinazotekelezwa na shirika hilo.

Mkurugenzi wa TAYOA, Peter Masika, alisema asilimia kubwa ya Watanzania ni vijana hivyo ni muhimu kuwapa nafasi ya kuonyesha na kuendeleza vipaji vyao ili kutengeneza ajira kwao na kwa wengine pia.

Alisema nia ya kuwapa fursa ya kuonyesha kazi zao za kiubunifu kwenye vyombo mbalimbali vya habari ni kuamsha hamasa ya vijana kupenda kujitegemea, uzalendo, maendeleo na kuongeza kasi ya mafanikio ya kuondokana na umaskini wa kipato na usio wa kipato kwa kufanya kazi kwa juhudi ili kuleta maendeleo yao na ya jamii zao kupitia Vijanatz Talent Show.

Alisema nia ya shirika hilo ni kuibua vipaji vya vijana na kuwasaidia kufikia ndoto zao kupitia teknolojia na mabadiliko ya fikra, tabia, uongozi, uzalendo, ujasiriamali ili waweze kutengeneza ajira mpya au wawe wanaajirika.

Pia alieleza kwamba kupitia Vijanatz Talent Show, TAYOA inatafuta vijana wenye vipaji vya ubunifu, mawazo yenye tija kwa Taifa na ulimwengu na sio kulenga tasnia ambazo zimezoeleka kwenye utafutaji wa vipaji hasa kwenye sanaa ya muziki na filamu.

Masika alieleza kwamba ili tuweze kuondokana na mkwamo wa kimaendeleo ni lazima sekta binafsi na ya umma tufanye kazi pamoja kuibua na kuvikuza vipaji vya ubunifu na kuvibadilisha kuwa fursa na ajira.

# JPM atoa bil. 1.5/- ujenzi hospitali rufani Kusini

**Na Hamisi Nasiri, MTWARA**

MKOA wa Mtwara umethibitisha kupokea Sh. bilioni 1.5 kutoka kwa Rais John Magufuli kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini ambayo inayojengwa mkoani Mtwara.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Mkoa huo, Gelasius Byakanwa, alipotembelea eneo la ujenzi wa hospitali Kata ya Mitengo.

Alisema serikali imetoa jumla ya fedha huzo kwa lengo la kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo ambayo itakapokamilika itahudumia mikao ya Mtwara, Lindi na Ruvuma, na kwamba hospitali hiyo itakuwa na uwezo wa kutoa huduma mbalimbali za kibingwa. Byakanwa alisema wazo la kwanza la ujenzi wa hospitali hiyo ulitokana na maamuzi yaliyotolewa na kikao cha Halmashauri Kuu (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi(CCM) mwaka 1979, ambapo yaliridhia kufanyika kwa ujenzi wa hospitali hiyo ufanyike mjini Mtwara.

Alisema serikali mkoani Mtwara na wananchi kwa ujumla wanampongeza Rais Magufuli kwa kutoa fedha hizo, na kwamba kukamilika kwa hospitali hiyo kutasaidia kuendelea kuboresha huduma za afya katika mikao ya kanda ya kusini.

Byakanwa alisema wamiliki wa eneo hilo wameshalipwa fidia zao ili kupisha ujenzi huo ambao ulianza mwaka 2009, huku jiwe la msingi la ujenzi wa hospitali hiyo liliwekwa na kiongozi wa mbio za Mwenge mwaka 2016, George Jackson Mbilinji, na kwamba baadhi ya majengo yalishajengwa katika eneo hilo tangu mwaka huo 2009.

Byakanwa alimsisitiza mkandarasi wa mradi huo ambaye ni Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuhakikisha anakamilisha ujenzi huo kwa wakati na kwa viwango kama serikali ilivyokusudia.

# Utoro wawatumbua watumishi saba

**Na Marco Maduhu, KISHAPU**

WATUMISHI saba wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga, wamesimamishwa kazi kwa madai ya utoro sugu kazini, huku wakijipatia likizo wenyewe kinyume cha taratibu za kiutumishi.

Watumishi waliosimamishwa kazi ni watendaji wa vijiji watatu, mtendaji kata mmoja, ofisa maendeleo kata mmoja, ofisa mifugo kata mmoja, pamoja na muuguzi mmoja.

Taarifa hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Kishapu, na Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Martini Ndamo, baada ya madiwani hao kujigeuza kuwa kamati, na kuazimia kuwasimamisha kazi watumishi hao, ingawa hawakutaka kuwataja majina yao.

Ndamo ambaye ni ofisa utumishi wa halmashauri hiyo, alisema Baraza hilo la Madiwani limeazimia kuwasimamisha kazi watumishi hao, kutokana na makosa ya utoro sugu kazini pamoja na kujipatia likizo kinyume cha taratibu za kiutumishi, na kusababisha wananchi kukosa huduma.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kishapu, Boniphace Butondo, alisema amechukizwa na tabia ya watumishi kutoroka kazini, na kubainisha hata kwenye kata yake ya Lagana mtendaji wa kijiji alishatoweka na hajulikani alipo bila ya kutoa taarifa.

Alisema halmashauri imeshachoka kuwa na watumishi mizigo, hivyo wataendelea kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi ambao wataendelea kuwa watoro kazini na kutowajibika ipasavyo kuwatumikia wananchi.

Pia aliwaonya watendaji wa idara ya mifugo na maendeleo ya jamii, kuwa wajitathmini kufanya kazi kwenye halmashauri hiyo, sababu wamekuwa na utovu mkubwa wa nidhamu wa kutoonekana kwenye maeneo yao ya kazi.



Meneja Ukuzaji wa Biashara Kitengo cha biashara ndogo na za kati wa Benki ya NBC, Jonathan Bitababaje, akiwasilisha mada kuhusiana na huduma za benki hiyo wakati wa kongamano la kibiashara lililoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya wateja wake wadogo na wa kati mkoani Dodoma lililofanyika jijini humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu wakulima kukosa mavuno sasa zaanikwa

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

TATIZO la baadhi ya wakulima kushindwa kutumia viuatilifu na kutumia upandaji usiozingatia utaalamu kwa mazao ya mizizi na nafaka kama maharage, mahindi na mihogo, limetajwa kuchangia asilimia kubwa ya wakulima kukosa mavuno.

Kauli hiyo ilitolewa na mratibu wa mradi wa Pata Tija Tanzania, mkoa wa Kagera, Frank Ademba, wakati wa mafunzo ya wakulima na wadau wengine wa kilimo yanayolenga kuongeza mavuno kwa wakulima na kuwezesha uzalishaji wenye tija.

Alisema mazao hayo yapo katika athari ya ushambulizi wa magonjwa kama viwavi jeshi na wadudu waharibifu ambayo humfanya mkulima kukosa uzalishaji wenye kiwango kwa ajili ya usalama wa chakula pamoja na kipato cha kuboresha maisha ya mkulima mdogo.

Alisema katika kukabiliana na changamoto za kilimo kwa mkulima mkoani humo wadau wa kilimo wameshauriana namna ya kumjengea uwezo mkulima kutoka katika kilimo cha mazoea na kufikia kilimo chenye tija.

Alisema kupitia mwongozo wa vipindi vya redio unaoandaliwa kwa msimu huu wa kilimo ambavyo vitarushwa kwa lengo la kumsaidia mkulima kujifunza na kutatua changamoto za upatikanaji wa mbegu na masoko, utawajengea uelewa.

"Mkulima atapata taarifa mbalimbali kama mbinu bora za kilimo chenye tija, usimamizi wa mazao na jinsi ya kuongeza thamani ya mazao husika, ili kupata masoko zaidi," alisema.

Alisema, mradi huo kwa mwaka 2018/2019 ulilenga kuwafikia wakulima wadogo 200,000 katika mkoa wa Kagera, na kuwa baadhi ya wakulima wameweza kufanikiwa kupitia redio kwa kuongeza uzalishaji kutoka magunia matatu katika ekari moja na kufikia magunia 20 ya uzalishaji wa mahindi.

Mratibu dawati la uzalishaji wananchi kiuchumi, Issaya Tendega, alisema ili kukamilisha mnyororo wa thamani katika kilimo, lazima mkulima apatiwe elimu ya uzalishaji kama njia ya kumsaidia kupata faida.

Tendega alisema kuwa, ili shughuli za uchumi ziendelee ushirikishwaji wa serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na kampuni unahitajika, na kuwa sekta ya kilimo inategemewa zaidi kwani ndiyo sehemu ya kumpatia kipato mwananchi wa chini na kuinua mapato ya serikali.

Mradi wa Pata Tija Tanzania uko chini ya Alliance for Green Revolution Africa (AGRA) na unatekeleza miradi miwili magharibi mwa Tanzania katika mikoa ya Kagera na Kigoma kwa kipindi cha miaka mitatu.

# Kongamano lanoa wateja wa NBC

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

BENKI ya NBC imeratibu kongamano maalum la kibiashara kwa ajili ya wateja wake wadogo na wakati jijini Dodoma ambalo pamoja na mambo mengine lililenga kuwaongezea wateja hao uelewa kuhusiana na mabadiliko ya kihuduma na fursa za kiuwezeshaji kutoka benki hiyo.

Akizungumza wakati wa kongamano hilo lililofanyika jijini humo, Meneja Ukuzaji wa Biashara Kitengo cha biashara ndogo na za kati wa Benki hiyo, Jonathan Bitababaje, alisema kufuatia uboreshwaji mkubwa wa huduma za benki hiyo ambazo zinaendana na kasi ya kiteknolojia na fursa za kiuchumi kumekuwa na hitaji kubwa kwa wateja hao kujengewa uelewa ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko hayo.

"NBC kwa sasa tumefanya mabadiliko makubwa ya kihuduma yanayoendana na kasi ya kiteknolojia na ukuaji wa uchumi na tumeona kuwa mabadiliko haya yatakuwa na tija zaidi kwa wateja wetu hasa wadogo na wakati ikiwa tu tutawajengea uelewa wa kutosha ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko haya badala ya kuwa changamoto," alibainisha.

Aidha, katika kongamano hilo la siku moja, mbali na masuala ya kibenki washiriki walipata fursa ya kusikiliza na kuchangia mada kutoka kwa wawakilishi wa taasisi nyingine ikiwamo Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) na Baraza la Uwezeshaji Wananchi (NEEC) ambao walielezea fursa mbalimbali za kibiashara ndani na nje ya nchi ikiwamo nafasi ya taasisi hizo katika kuwaunganisha wafanyabiashara na wenzao kutoka nje ya nchi.

"Kwa kushirikiana na benki ya NBC tumekuwa tukishirikiana mambo mengi yanayolenga kuwasaidia wafanyabiashara wetu na hivi karibuni tunatarajia kuwasafirisha wafanyabiashara kwenda nchini China kwa ajili ya safari ya kibiashara ya siku kumi ambapo wahusika watalipa gharama ya kiasi cha Dola za Kimarekani 2500 tu ambayo itagharamia mahitaji yao yote ya msingi ikiwamo nauli ya kwenda na kurudi, gharama za chakula na huduma nyingine ikiwamo ya wakalimani," alisema Patrick Magai, Meneja Maendeleo Viwanda kutoka TCCIA.

"Pia ipo haja kwa taasisi za fedha nchini kutambua baadhi ya changamoto zinazotukabili wateja wao kwenye biashara zetu kwa kubuni huduma zinazotambua changamoto zetu ikiwamo kuangalia namna ya kushirikiana nasi pindi tunapokabiliwa na changamoto ya ucheleweshwaji wa malipo yetu kutoka kwa wateja wetu," alisema mmoja wa wafanyabiashara hao ambaye ni mkandarasi, Dk. Steven Masangia.

# Wawili wakamatwa na mihadarati mgodini

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

JESHI la Polisi mkoa wa Manyara, linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kukutwa na kete 321 za mihadarati aina ya heroine kwenye machimbo ya madini ya tanzanite huko Mererani.

Machimbo hayo yako kwenye Mamlaka ya Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Manyara, Agostino Senga, alisema dawa hizo za kulevya zinahisiwa kuwa ni aina ya heroine.

Kamanda Senga alisema watuhumiwa hao walikamatwa Septemba 11 saa 10:00 jioni katika eneo la kitalu B (Opec) ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini ya tanzanite. Aliwataja watuhumiwa hao, kuwa ni Hussein Mbega (37), mkazi wa Soko Mjinga, Saidi Shabani (19), mkazi wa Daraja Mbili, wote wa jijini Arusha.

Alisema watu hao walikamatwa kwenye jengo ambalo halijakamilika na dawa hizo za kulevya zilikuwa zimefungwa kwenye vipakti vidogo wakisubiri wateja.

"Baada ya kupata taarifa kuwa kuna watu wanafanya biashara hiyo askari wetu walifika mara moja kwenye eneo la tukio kufanya msako wa kushtukiza na kuwakamata watu hao wakiwa na dawa hizo za kukevya," alisema Senga.

Aidha, aliwataka wananchi wote wanaofanya shughuli zao ndani ya ukuta huo kuhakikisha kuwa wanafanya biashara halali na endapo watakwenda kinyume watachukuliwa hatua za kisheria.

"Gharama kubwa zimetumika kujenga ukuta huu unaozunguka eneo linalochimbwa tanzanite, hivyo wananchi wanapaswa kufanya biashara halali kwani Jeshi la Polisi lipo makini kwa kuweka ulinzi eneo hili," alisema Senga.

Alisema watuhumiwa hao, watafikishwa mahakamani uchunguzi wa tukio hilo, utakapokamilika kwani bado wanaendelea na uchunguzi.




Ofisa Masoko wa TBL katika kiwanda cha Mwanza, Happy Conrad, akitoa elimu ya kunywa kistaarabu kwa wahudumu wa baa ya Las Vegas Bwiru jijini Mwanza, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uhamasishaji Unywaji wa Pombe Kistaarabu Duniani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kituo cha afya chakosa watumishi, vifaa tiba

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

UHABA wa wafanyakazi katika Kituo cha Afya cha Muriet kilichopo jijini Arusha, unakwamisha utoaji wa huduma.

Akisoma ripoti ya kituo hicho, mbele ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Joseph Nyamuhang, Mganga Mkuu wa Jiji la Arusha, Dk. Simon Chacha, alisema kituo hicho kinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa wafanyakazi.

Alisema kituo hicho kina jumla ya wafanyakazi 25 na mahitaji yake ni watumishi 52 hivyo kuna upungufu wa wafanyakazi 27.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema katika kituo hicho, pia wanauhitaji wa vifaa vya tiba na baadhi ya vile vilivyopo walivipata kupitia mfuko wa ndani wa jiji kwa fedha za makusanyo ya ndani na michango ya wadau waliowekeza katika mkoa wa Arusha na mchango wa Mkuu wa Mkoa, Mrisho Gambo.

Aidha, alisema ujenzi wa kituo hicho, umegharimu zaidi ya Sh. bilioni moja hadi kukamilika na katika halmashauri ilichangia Sh. milioni 359 na Serikali Kuu Sh. milioni 700.

Chacha alisema kituo hicho, kinahudumia mitaa 13 katika kata ya Murieti na nyingine za jirani, na kwamba kuna wateja takribani 50,000.

Katika maelezo yake alimweleza Katibu Mkuu kuwa kituo hicho kimekamilisha majengo ya upasuaji, maabara, jengo la mama na mtoto na jengo la kuhifadhia miili.

Katibu Mkuu wa Tamisemi, Joseph Nyamuhanga, alifurahishwa na kazi iliyofanywa kwenye kituo hicho, huku akiishukuru halmashauri kwa kununua vifaa vya utendaji kazi katika kituo hicho.

Alisema serikali itawapatia vifaa pamoja na kuleta watumishi ili waweze kufikia idadi inayoendana na mahitaji ya watumishi wanaohitajika kituoni hapo.

"Tatizo la uhaba wa wafanyakazi lipo kwenye vituo vya afya, zahanati na hospitali nyingi hapa nchini, kama serikali tutajitahidi kuongeza idadi ya watumishi wanaotakiwa, lakini napenda kuwashukuru wafanyakazi wa kituo hiki kwa kuendelea kufanya kazi kwa umahiri na kuhakikisha wagonjwa wanapata huduma ya uhakika," alisema Nyamuhanga.

Meya wa Jiji Kalist Lazaro, alimshukuru Katibu Mkuu kwa kutembelea kituo hicho, na alisema halmashauri hiyo, itakapokuwa na uwezo wa kifedha haitasubiri serikali kuu kutoa fedha za kuwahudumia wananchi bali halmashauri itachukua jukumu hilo mapema.

"Tunahitaji kufanya maendeleo kama halmashauri ili kuipunguzia serikali mzigo napenda kusema mimi na Mkurugenzi wa Jiji tutaendelea kushughulikia miradi ili kuinua maendeleo katika Mkoa wetu, " Lazaro.

## Wadau mifugo walia kukosa soko la bidhaa

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WADAU wa sekta ya mifugo, katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na Arumeru, wameitaka jamii kuthamini bidhaa zinazozalishwa nchini badala ya kupendelea zile zinazotoka nje.

Kadhalika, wameitaka kuachana na dhana potofu kuwa vitu vya nje ni bora kuliko vinavyotengenezwa hapa nchini.

Wakizungumza katika hafla ya kuwakabidhi vyeti wadau wa mifugo walioshiriki kwenye Maonyesho ya Nanenane mwaka 2019, katika banda la mifugo la halmashauri, wadau hao walisema changamoto kubwa inayowakabili wawekezaji wa mifugo ni mwitikio wa jamii kwenye matumizi ya bidhaa za ndani.

Waliwataka Watanzania kuthamini na kutumia bidhaa zinazotengenezwa na viwanda vya nyumbani, ili kuunga mkono jitihada za serikali za kufikia uchumi wa kati na wa viwanda

Mmoja wa wadau hao, Baraka Laizer, alisema wafugaji wengi wameamka na kufuga kibiashara na kutumia malighafi za mifugo, kuanzisha viwanda kama vya kuchakata ngozi, kufungasha maziwa na nyama kwa kutumia teknolojia ya gasi itokanayo na kinyesi cha ng'ombe.

Laizer alisema changamoto inayowakabili ni ushindani mkubwa wa bidhaa kutoka za nje ya nchi kutokana na dhana iliyojengeka kwenye jamii ya kutokununua vitu vinavyozalishwa nchini kwa kigezo hakuna ubora wala viwango.

Msimamizi wa kiwanda cha Uchakataji Nyama, cha Maasai Exports Butchery, Frenk Mollel, alisema kiwanda chake, huzalisha bidhaa za kimataifa, lakini bado wananchi hawazitumii hizo kwa wingi, jambo linalosababisha soko la ndani kusuasua.

"Watu kutoka mataifa ya nje wananunua ng'ombe hapa nchini, wanawasafirisha na huko wanatumia mashine kama tunazotumia lakini wakiingiza bidhaa zao hapa nchini, Watanzania wananunua bidhaa hizo, kwa wingi na kwa bei ya juu wakidhani ni bora kuliko zetu, ilhali kiwango cha ubora kinafanana na bidhaa ambazo tunazalisha hapa nchini," alisema Mollel.

# Pigeni kura ili Mlima K'njaro uwe kivutio bora duniani

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MLIMA Kilimanjaro umeingia katika shindano la kimataifa la kuwania tuzo za dunia za kivutio bora zaidi cha utalii kinachoongoza kwa mwaka 2019.

Tuzo hizo za World Travel Awards, zimeuweka mlima huo kwenye orodha ya nchi bora zenye vivutio adimu Afrika na duniani.

Jana, Kamishna Mwandamizi Msaidizi wa Uhifadhi nchini (SAC), Paschal Shelutete, aliithibitishia Nipashe kuwa kazi ya kupiga kura kwa njia ya mtandao ilianza rasmi Septemba 12 na inatarajiwa kufikia ukomo Oktoba 20 mwaka huu.

"Tunawaomba Watanzania kuupigia kwa wingi kura Mlima Kilimanjaro ambao umeingia tena katika shindano la kimataifa la kutafuta kivutio bora zaidi cha utalii kinachoongoza duniani kwa mwaka 2019. "Kura zote zinapigwa kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya worldtravelawards.com/vote kwa kusajili taarifa zako na kuingia rasmi katika mfumo wa upigaji kura."

Kura zitakazopigwa, ndizo zitakazoamua mshindi kutokana na wingi wa kura ambazo Mlima Kilimanjaro itapata.

Aidha, taarifa iliyochapishwa katika tovuti ya World Travel Awards inaonyesha kuwa utaratibu kama huo ulifanyika Mashariki ya Kati, Februari mwaka huu, wakati Ulaya pazia hilo lilifunguliwa Machi 11 mwaka huu.

Pia, zilionyesha kuwa Amerika ya Kati, Amerika ya Kusini na Asia, pazia hilo lilifunguliwa Machi 25 mwaka huu.

Itakumbukwa kuwa mwaka 2013, Mlima Kilimanjaro ulishinda tuzo ya maajabu saba ya asili ya Afrika na kuipa Tanzania heshima kubwa kutokana na kuwa na kivutio hicho cha kipekee cha utalii.

Mlima Kilimanjaro ni miongoni mwa hifadhi tano zilizopo chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), ambazo zinaoongoza nchini kwa mapato na kuziendesha hifadhi nyingine.

## 'Waliopiga' mradi wa umwagiliaji wasakwa

**Na Godfrey Mushi, SAME**

SERIKALI imetoa siku 30 kwa viongozi wa umma walioshiriki kuuhujumu mradi wa umwagiliaji wa Kalimawe, Wilaya ya Same, kuirejesha mitambo ya kufua umeme wa jua iliyoondolewa kwa mizengwe, badala ya kusubiri mkono wa dola.

Watu wanaodaiwa kuwa viongozi wa umma wakishirikiana na baadhi ya wananchi katika Kijiji cha Karamba, Kata ya Kalimawe, wanadaiwa kung'oa mitambo hiyo iliyokuwa ikitumika kusukuma maji.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alitoa maelekezo hayo, baada ya kukutana na kusikiliza kero za wakazi wa Karamba.

"Nyie viongozi wa Karamba na wengine mnaojua mmeshiriki kuukwamisha mradi huu wa umwagiliaji, rejesheni solar zilizokuwa zinatumika kusukuma mitambo ya maji. Baada ya siku 30 kupita, ntalia na nyie.

"Suala la kurejesha 'sola' hizo ni agizo la waziri, naomba sana msimchonganishe na Waziri Mkuu, serikali na wananchi wake."

Akiwa katika kijiji hicho, mkuu huyo wa wilaya aliwataka wakazi wa Karamba kuheshimu na kuendelea kushirikiana na vijiji vingine vinavyolizunguka bwawa la Kalimawe vinavyotekeleza mradi wa kuzalisha vifaranga vya samaki.

Mwaka jana, vijiji vinne viliingia makubaliano ya ubia katika uwekezaji huo na kampuni ya Norway na ile ya Mikono Tayari ya Tanzania.

Kampuni hizo ziliahidi kujenga kiwanda cha kisasa cha kusindika minofu ya samaki kwa ajili ya soko la ndani na la kimataifa.

Bwawa hilo lenye urefu wa mita 4,000 na upana wa mita 5,000 lilijengwa na Waingereza kati ya mwaka 1952 na 1959.

**"Nyie viongozi wa Karamba na wengine mnaojua mmeshiriki kuukwamisha mradi huu wa umwagiliaji, rejesheni solar zilizokuwa zinatumika kusukuma mitambo ya maji. Baada ya siku 30 kupita, ntalia na nyie.**



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Steven Ulaya, akiwakabidhi hati ya shukrani Mwenyekiti wa ECLAT Foundation, Peter Toima na Mkurugenzi wa Upendo Society, Fred Heimbach kwa kujenga na kukarabati Shule ya Msingi Lengijabe kwa Sh. milioni 102 juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Ofisa kizimbani kwa kuomba, kula 'mlungula'

**Na Paul William, MOSHI**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Kilimanjaro, imemfikisha mahakamani Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Julius Kimaro, kwa madai ya kushindwa kusimamia makusanyo ya maduhuli.

Aidha, anashtakiwa kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni 200,000.

Ofisa huyo, ndiye aliyepewa jukumu la kusimamia makusanyo ya maduhuli katika halmashauri hiyo.

Kimaro anayekabiliwa na kesi hiyo ya jinai, namba 15 ya mwaka 2019, alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, mwishoni mwa wiki.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Sophia Masati.

Kimaro anashtakiwa kwa makosa mawili ya kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni 200,000.

Akisoma hati ya mashtaka mahakamani hapo, Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Samwel Gabriel, alisema Kimaro anashtakiwa kwa makosa mawili ya kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa mfanyabiashara wa vinyago ili aweze kumpunguzia kodi aliyokuwa amekadiriwa.

Alisema mshtakiwa huyo alifanya kosa hilo kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, namba 11 ya mwaka 2007.

Akiwa kizimbani, mshtakiwa huyo alikana makosa yote na kuachiwa kwa dhamana, baada ya kukidhi vigezo vya dhamana vilivyomtaka kuwa na wadhamini wawili watakaosaini bondi ya Sh. 500,000 kila mmoja.

Kabla ya kuahirisha kesi hiyo, Hakimu Masati alisema shauri hilo litatajwa tena mahakamani hapo Oktoba 11 mwaka huu.

# Nipashe Spotika



MECHI 5 ZA KUTAZAMWA MAKUNDI UEFA 2019/20 UK. 16 & 17




## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Man City, Sergio Aguero, amekuwa mchezaji wa tatu kuweza kufunga mfululizo katika mechi tano za mwanzo za Ligi Kuu England za msimu, baada ya Jose Antonio Reyes wakati akiwa Arsenal msimu 2004-05 na Wayne Rooney alipokuwa akiichezea Manchester United msimu wa 2011-12.

## PAMBANA...

Beki wa Kushoto wa Newcastle, Jetro Williams, akihaha kumdhibiti mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, wakati wa mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi na Liver kushinda 3-1. **HABARI UK. 29**



# KWA NINI EMERY, ARSENAL WANAHITAJI MUDA ZAIDI

**LONDON,** England

ARSENAL ilikuwa na kipindi kizuri cha usajili wa dirisha la majira ya joto. Uvumi kwamba bajeti ya usajili ilikuwa ni pauni milioni 45 ulitoa ishara mbaya na mashabiki walikuwa wamesha-poteza matumaini kuelekea msimu mpya.

**Mashabiki wengi walionekana kuvurugwa na wakaona wasipopaza sauti zao inawezekana kusifanyike usajili wowote ndani ya kikosi hicho.**

Wakaanzisha kampeni ya "#WeCare DoYou" (tunajali, wewe vipi) na ikaamsha kelele nyingi.

Na wakaitisha utiaji wa saini ya kutokuwa na imani na mmiliki wa Arsenal na hiyo ni baada ya miezi 12 tu tangu kukamilisha ununuaji wa hisa nyingi zaidi za klabu hiyo na yeye kubakia kuwa ndiye mwenye maamuzi ya mwisho.

Josh Kroenke akaamua kujibu kelele za mashabiki hao watiifu wa Arsenal. Hivyo, usajili kuanza kufanyika, akanunuliwa William Saliba, Dani Ceballos na Nicolas Pepe.

Na katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili, Arsenal wakaongeza wachezaji wawili kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya ulinzi, David Luiz na Kieran Tierney. Mashabiki wa Arsenal wakaanza kuota ndoto nzuri kwamba na wao sasa watakuwa kwenye mbio bora za ushindani.

Ushindi dhidi ya Newcastle na Burnley ukafuatiwa na kipigo kutoka kwa Liverpool na baadaye sare ya 'dabi' ya watoto wa jiji moja la London, Tottenham.

Tayari mashabiki wa Arsenal wameanza kuuliza maswali kama Arsenal hii mpya inaweza kutoa ushindani unaotakiwa. Wengine wameanza kutaka kocha, Unai Emery aondoke baada ya kumlinganisha na Jurgen Klopp na Pep Guardiola.

Wengine walionyesha kuchukizwa na makosa ya mapema kutoka kwa David Luiz na kushindwa kuwa na kasi nzuri ya umaliziaji kutoka kwa Nicolas Pepe.

Uvumilivu ndio nguzo kuu katika maisha, na kwamba utakuwa muda mzuri wa Arsenal kujaribu kuona kama mradi wao mpya unahitaji uvumilivu.

Unai Emery amefanya usajili katika madirisha mawili tu ya usajili, kwa sababu Arsenal ilishindwa kufanya usajili wa kudumu wa wachezaji, kipindi cha dirisha dogo la Januari.

Klabu hiyo imeanza maisha katika kurasa mpya baada ya wachezaji wa zamani kuondoka ambao ni nahodha Laurent Koscielny, Carl Jenkinson, Nacho Monreal, Stephan Lichtsteiner, David Ospina, Mohamed Elneny na Henrikh Mkhitaryan.

Elneny, Mkhitaryan na Mustafi wameondoka kwa mkopo, lakini ni wazi kwamba watataka kubakia huko waliko moja kwa moja.

Arsenal mpya imejaa vijana, kumwondoa kwa mkopo Mkhitaryan na kumwongeza Emile Smith-Rowe kwenye kikosi cha Arsenal cha Ligi Kuu, maana yake kwa sasa Arsenal wana wachezaji wengi zaidi vijana.

Kikosi cha kwanza kitakuwa kinajumuisha wachezaji wengi vijana, kama Rob Holding, Tierney na Bellerin atakaporudi kutoka chumba cha majeruhi. Pepe ameanza kwa kuonyesha ishara nzuri ya maisha yake hapo kwenye Uwanja wa Emirates na anaonekana ataleta kitu kizuri kwenye fowadi ambacho kilikosekana tangu kuondoka kwa Alexis Sanchez, Januari mwaka 2018.

Wakimvumilia kwa muda mchache, mabao yataanza kumiminika kutoka kwa mzaliwa huyo wa Ufaransa ambaye anaichezea Ivory Coast.


Dani Ceballos tayari ameonyesha ubora wake ingawa anacheza hapo kwa mkopo wa msimu mmoja. Upatina wa David Luiz na Sokratis unaweza kuleta uimara mkubwa zaidi kwenye safu ya ulinzi msimu huu.

Huku Mesut Ozil akiwa bado hayupo, lakini Arsenal hii ya Emery inaonyesha matumaini kwamba inaweza kutoa ushindani kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa miaka michache kutoka sasa.

Ndio, si matokeo yote yamekuwa ya kuvutia hadi sasa kwenye msimu huu. Hata hivyo, timu imeonyesha kuwa na ari nzuri ya kupigana na kukomboa matokeo kama ilivyofanya kwenye mchezo dhidi ya Spurs.

Wakati Manchester United na Chelsea zikiwa zinapitia kwenye kipindi cha mpito, Arsenal ipo kwenye ubora zaidi wa kumaliza kwenye nne bora kuliko misimu mitatu iliyopita.

**JE, WAJUA?**



KIPIGO Manchester City ilichokipata dhidi ya Norwich kwenye Ligi Kuu England juzi ni cha kwanza dhidi ya timu iliyopanda daraja tangu Machi mwaka 2015 ilipochapwa na Burnley - haijawahi kufungwa katika mechi 25 dhidi ya timu kama hizo zilizopanda kabla ya juzi, ikiwamo zote 18 chini ya Pep Guardiola.

## MICHEZO



Kiungo wa Yanga, Papy Tshishimbi, akimtoka kiungo wa Zesco, Thabani Kamusoko katika Uwanja wa Taifa wakati wakitoka sare ya bao 1-1 juzi.

# SABABU 5 YANGA KUISHINDWA ZESCO

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Yanga, Jumamosi ilijikuta ikinyang'anywa tonge mdomoni kwa kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Zesco ya Zambia kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Wakati tayari baadhi ya mashabiki wakiwa wameshatoka uwanjani, wengine wakiwa kwenye vyombo vya usafiri, kiungo wa zamani wa Yanga, anayeichezea Zesco kwa sasa, Thabani Kamusoko aliachia shuti kali akiwa nje kidogo ya eneo la hatari na mpira huo ukajaa wavuni na kumuacha kipa Metacha Mnata akiruka bila mafanikio.**

Ni bao lililowanyong'onyesha wanachama, mashabiki wa Yanga na Watanzania kwa ujumla kwani tayari ilionekana kuwa Yanga ingeondoka na ushindi wa bao 1-0, kabla ya mechi ya marudiano wiki mbili zijazo nchini Zambia.

Baada ya mechi hiyo kumalizika, mashabiki wa soka nchini kila mmoja alikuwa akiongea lake kuhusiana na matokeo hayo, lakini kubwa zaidi ni kwa nini Yanga haikulinda ushindi wake.

Mwandishi wa makala haya anatoa sababu tano ambazo kwa njia moja ama nyingine zilisababisha timu hiyo kushindwa kuibuka na ushindi kwenye mechi hiyo ya mkondo wa kwanza...

### 1. MASTRAIKA KUSHINDWA KUTUMIA NAFASI

Msimu huu inaonekana Yanga ina matatizo makubwa kwenye safu ya ushambuliaji. Ingawa ina mastraika wote kutoka nje ya nchi, lakini wamekuwa wakifunga mabao kwa shida, tena kwa timu za Daraja la Kwanza au la Pili, lakini linapokuja suala la mechi dhidi ya timu za daraja la Yanga inakuwa matatizo.

Mabao mengi ya Yanga sasa yanategemea zaidi penalti, faulo au kona. Kwenye mechi dhidi ya Zesco hali ilikuwa ni ile ile. Mastraika wa Yanga wakiongozwa na Sadney Urikhob walikosa mabao ya wazi ambayo yangeweza kusababisha timu hiyo kuondoka na ushindi hata wa mabao 3-1.

### 2. VIUNGO HAWAKUWA NA MIPANGO

Wachezaji wa eneo la kiungo la Yanga hawakuwa wabunifu kiasi cha kutosha hivyo kusababisha timu kutegemea mipira mirefu kutoka kwa mabeki.

Kuna wakati iliwasumbua mno Zesco na hata kusababisha penalti, lakini walipogundua mabeki wa timu hiyo wakawa makini na mipira hiyo mirefu kiasi kwamba ikawa haina madhara tena kwao. Waliichukua kiulaini mno. Yanga haikuwa tena na mpango mbadala. Lakini kama viungo wa Yanga wangekuwa watulivu na wabunifu, wangeweza kusababisha hatari kwa pasi za mwisho.

### 3. KUPAKI BASI KULIWAMALIZA

Ilishangaza kuona Kocha Mkuu Mwinyi Zahera akionekana kuridhishwa na idadi ya bao moja na kuiacha timu yake kuanza kucheza mchezo wa kuzia zaidi kuliko kushambulia.

Ilitegemewa kuona Zesco ndiyo wangekuwa wanazuia ili kutafuta sare au kutofungwa zaidi ya bao moja kwa ajili ya kujitengenezea mazingira mazuri nyumbani, lakini badala yake Yanga ndiyo ilionekana inajilinda zaidi hususan kipindi cha pili.

Mpango mkakati wa Yanga ulitegemewa kutafuta mabao japo mawili au zaidi ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ugenini, lakini bao moja tu lilifanya hata mabadiliko ambayo kocha alikuwa akiyafanya yalionekana kabisa kuwa ni ya kuzuia zaidi kuliko kushambulia.

Hii ilisababisha Yanga kushambuliwa mfululizo dakika 15 za mwisho na kusababisha mabeki kuchoka na hatimaye kuruhusu bao dakika za mwisho kabisa. Kama Yanga ingekuwa ikishambulia kutafuta mabao, sidhani kama Zesco ingeweza kusawazisha.

### 4. WACHEZAJI KUISHIWA PUMZI MAPEMA

Baadhi ya wachezaji wa Yanga wanaonekana kuwa na tabia ya kuchoka mapema. Hata zile mbio za mwanzo zilizokuwa zikiwahenyesha mabeki wa Zesco zilikuwa zikipungua kila dakika zilivyozidi kusonga mbele.

Ilitegemewa wachezaji wa Zesco ndio waishiwe pumzi kwa sababu ya joto la Dar es Salaam, badala yake wachezaji wengi wa Yanga walionekana kuchoka na kushindwa kulinda ushindi wao.

### 5. METACHA ALIIUA YANGA KWA KUPOTEZA MUDA

Bao la kusawazisha la Zesco lilifungwa dakika ya nne na sekunde 24 za majeruhi. Mwamuzi alikuwa akifidia muda ambao kipa wa Yanga Metacha Mnata alizipoteza kiasi cha kuzawadiwa kadi ya njano.

Ilipotimu dakika ya pili ya nyongeza bila sababu yoyote Mnata alijiangusha chini, kitendo ambacho kilitafsiriwa kuwa ni kupoteza muda. Mwamuzi wa akiba alionyesha dakika nne tu za nyongeza. Na tayari zilikuwa zimekwisha. Lakini kitendo cha Mnata kuonekana kupoteza muda, kilimfanya mwamuzi kuongeza tena dakika nyingine. Kama Mnata asingepoteza muda, mechi ilikuwa imemalizika kwa dakika nne kamili za nyongeza na zisingekuwa na nyongeza zingine, hivyo bao lisingefungwa. Na hata hizo dakika nne za nyongeza zilichangiwa zaidi na kipa huyo huyo kuigiza kuumia mara kwa mara.

## NJE YA UWANJA

LIVERPOOL hadi sasa imefunga mabao 101 dhidi ya Newcastle kwenye Ligi Kuu England- ni timu ya tatu kufunga zaidi ya mabao 100 dhidi ya timu moja kwenye mechi za ligi hiyo, na ya kwanza kufanya hivyo ambayo haijawahi kufikiwa ni (Arsenal mabao 107 dhidi ya Everton) nyingine ambayo sasa imefunikwa na Liverpool ni (Manchester United mabao 100 dhidi ya Everton).






# MECHI 5 ZA KUTAZAMWA MAKUNDI UEFA 19/20

**LONDON,** England

LIGI ya Mabingwa Ulaya ni sehemu ambayo klabu kubwa za Ulaya zinakutana kwa ajlili ya kupigania zawadi kubwa kwa soka la Ulaya.

**Makocha hutumia muda wao kuziandaa timu zao, nyota wakubwa wanakuwa kwenye nafasi ya kung'ara katika hatua hiyo kubwa na mwisho wa siku timu moja inaibuka na kubeba taji hilo.**

Wakati hatua ya makundi ya michuano hiyo ikianza kesho, hapa tunaangalia mechi tano zitakazokuwa kali zaidi kwenye hatua hiyo...

### KUNDI A - PARIS SAINT GERMAIN VS REAL MADRID

Timu ambayo imeshinda mara nyingi zaidi kwenye historia ya mashindano hayo itacheza dhidi ya timu ambayo ina kila kitu. Mchezo huu kati ya PSG dhidi ya Real Madrid keshokutwa, Jumatano ni moja ya mechi inayoonekana itakuwa ngumu zaidi.

Timu zote mbili zimeimarisha vikosi vyao, kwani Real Madrid kwa sasa ina huduma ya Eden Hazard pamoja na Luka Jovic na Ferland Mendy. Cha muhimu zaidi ni kwamba, Zinedine Zidane atarudi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ambako aliweka historia ya aina yake wakati akiwa na Los Blancos hao.

Kwa upande wao PSG baada ya kushindwa kumuuza Neymar, kwenye safu yao ya ushambuliaji ameongezeka Mauro Icardi.

Na sasa itakuwa ni vita kati ya Neymar na Hazard, huku upande mwingine ukiwa ni Bale na Mbappe.

### KUNDI B - BAYERN MUNICH VS TOTTENHAM HOTSPUR

Msimu uliopita Tottenham Hotspur ilimshangaza kila mtu kwa kufika fainali ya mashindano hayo ikiwa ni mara ya kwanza katika historia yao.

Kwa bahati mbaya kikosi hicho cha Mauricio Pochettino kikafungwa na Liverpool kwenye fainali iliyopigwa jijini Madrid nchini Hispania.

Katika dirisha la usajili, Tottenham haikupumzika, wameongeza wachezaji wazuri tu. Usajili wa Tanguy Ndombele, Giovani Lo Celso na Ryan Sessegnon umekiimarisha kikosi chao.

Bayern Munich wao wamemwongeza Phillipe Coutinho ambaye amesajiliwa kwa mkopo kutoka kule Barcelona, pia wana Benjamin Pavard, Ivan Perisic na Lucas Hernandez.

### KUNDI D - ATLETICO MADRID VS JUVENTUS

Timu hizi mbili zimeonekana kuwa na ushindani mkubwa zaidi zinapokutana kwenye mashindano hayo.

Cristiano Ronaldo atakuwa anakutana na wapinzani wake wa zamani kutoka jiji la Madrid. Kwa mara ya mwisho Ronaldo kucheza na kikosi hicho cha kocha, Diego Simeone alifunga mabao matatu 'hat trick' na kuiondoa Atletico Madrid kwenye mashindano hayo.

Juventus imeimarisha kikosi chake kwa kumsajili Matthijs de Ligt.

Atletico wao wamewapoteza Antoine Greizmann, Rodri na Diego Godin, na imeanza vizuri zaidi kwenye Ligi Kuu ya Hispania msimu huu.

Usajili wao mpya ni Joao Felix na tayari ameanza kutengeneza jina lake katika jezi ya klabu hiyo.

Itakuwa vita kati ya kocha Maurizio Sarri vs Diego Simeone na Cristiano Ronaldo vs Joao Felix.

### KUNDI F - BARCELONA VS INTER MILAN

Kwa Barcelona, msimu uliopita wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hautasahaulika kabisa kwao.

Licha ya kuongoza kwa mabao 3-0 kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali dhidi ya Liverpool, wakajikuta wakitolewa kwenye mchezo wa pili kwa kipigo cha 'mbwa mwizi'.

Inaongozwa na Lionel Messi na kwa sasa ameongezwa Antoine Griezmann ambaye anaongeza nguvu kubwa kwa mabingwa hao wa Hispania.

Ingawa kuna shaka kubwa juu ya uwezo wa kocha, Ernesto Valverde kuiongoza timu hiyo kwenye mafanikio, kikosi cha Barcelona ni kizuri na ni moja ya timu inayopewa nafasi ya kulitwaa taji hilo msimu huu.

Inter Milan ni moja ya timu inayoweza kuleta changamoto kubwa zaidi kwenye michuano hiyo msimu huu.

Ujio wa kocha mpya, Antonio Conte na usajili wa washambuliaji kutoka Manchester United, Romelo Lukaku na Alexis Sanchez, Inter inaonekana kuwa tayari kwenye mbio moja kuwania taji hilo la Ulaya.

Licha ya kumpoteza Mauro Icardi, Waitaliano hao wameimarisha kikosi chao na hivyo wanakuwa na uwezo wakuisumbua Barcelona.

### KUNDI F - INTER MILAN VS BORUSSIA DORTMUND

Bila shaka yoyote, Kundi F ndilo linaloonekana kuwa "kundi la kifo". Timu zote tatu Barcelona, Inter Milan na Borussia Dortmund zina nafasi ya kusonga mbele.

Wajerumani hao wamekuwa bize wakati wa kipindi cha usajili wa majira ya joto kwa kumrudisha Mats Hummels huku wakiwaongeza Julian Brandt, Thorgan Hazard na Paco Alcacer kwenye kikosi chao.

Vijana hao wa kocha, Lucien Favre wana nafasi kubwa ya kuleta changamoto kubwa msimu huu.

### HESHIMA KUZITAJA

Kundi E - Liverpool vs Napoli

Hii ni marudio ya msimu uliopita kwenye hatua ya makundi kwa timu hizi. Liverpool ilishinda pale kwenye dimba la Anfield dhidi ya Napoli na ikaishia kwenda kulitwaa taji hilo.

### KUNDI H - CHELSEA VS AJAX

Licha ya kuwapoteza Frenkie de Jong na Matthijs de Ligt, Ajax imebaki kuwa timu ya kuvutia zaidi kwenye mashindano haya, kwani imesheheni wachezaji wengi vijana.

Kwa upande mwingine, Chelsea inarudi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa na kocha Frank Lampard na inaweza kuleta changamoto nzuri katika mashindano hayo.

## Nukuu

"Anacheza kama mtu aliyeichezea Arsenal kwa miaka mingi. Inatisha kuwa ndiyo kwanza ana miaka 20 tu, anaweza kuwa katika nafasi ya kiungo ya Arsenal kwa miaka 10 ijayo, ni mzuri katika jukumu hilo. Hata anapotoa mpira, anataka kuwa na mpira wakati wote. Kamwe hatetereki katika hilo na hilo ndilo linalotakiwa kwenye idara ya kiungo ambalo huwezi kufundishwa, huwezi kufundisha hilo," **Straika wa zamani wa Tottenham Hotspur, Darren Bent, akimzungumzia kiungo wa Arsenal, Mfaransa Matteo Guendouzi.**



"Rekodi zipo pale kwa ajili ya kuvunjwa. Natumai kuwa kasi hii, shauku na matamanio huambatana nami kila wakati na kwamba ninafikia mechi 200, ambazo ndizo lengo, unapaswa kulifanya hilo kuwa gumu, bado ninapaswa kupiku [idadi hiyo ya mechi 167] na ninatumai bado ninaweza kuichezea nchi hii kwa miaka mingi zaidi," **Nahodha wa Hispania, Sergio Ramos, baada ya kufikia rekodi ya Iker Casillas ya mechi 167 za kimataifa.**



"Nafiriki kwa sasa safu ya ushambuliaji ya England ndio inayohamasisha zaidi, ukiangalia safu ya wachezaji watatu pale mbele kwa hakika ni imara zaidi. Tuna Sancho na Hudson-Odoi ambao wanaendelea kuimarika kwa uhakika kabisa inavutia. Unahitaji wachezaji ambao wanaweza kuwa na matokeo chanya kwenye mechi, lakini pia unatakiwa kuwa na wachezaji ambao wanaingia na kusababisha madhara," **Kocha Gareth Southgate wakati walipoichapa Bulgaria 4-0 kwenye mchezo wa kufuzu Euro 2020.**






# LIGI KUU BARA KILA TIMU KIVYAKEVYAKE

Winga wa Simba na mfungaji wa bao la ushindi, Miraji Athumani akiwatoka walinzi wa Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Uhuru Ijumaa iliyopita wakati wakishinda 2-1. **PICHA: MAKTABA.**

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara imeingia kwenye raundi ya pili wiki hii, baada ya kushuhudiwa mechi kadhaa zikichezwa na kuanza kuleta msisimko.

**Baada ya mechi za raundi ya pili, ingawa baadhi ya timu hazikucheza kutokana na mechi za kimataifa, lakini mechi zilizochezwa mpaka sasa zimetengeneza rekodi na takwimu mbalimbali.**

**1. SIMBA**

Ushindi wa mabao 2-1 ilioupata Ijumaa iliyopita dhidi ya Mtibwa umeifanya timu hiyo kucheza Ligi Kuu misimu miwili mfululizo na kushinda mechi mbili za kwanza.

Ilianza ligi kwa kuichapa JKT Tanzania mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Uhuru, na mechi ya pili kwenye dimba hilo, ikafungwa Mtibwa Sugar mabao 2-1.

Msimu uliopita 2018/19, ilianza ligi kwa kuifunga Prisons bao 1-0 na mechi ya pili ikaichapa Mbeya City mabao 2-0, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Ni tofauti na msimu wa 2017/18 ambao baada ya kuichapa Ruvu Shooting mabao 7-0 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Simba ilikutana na kigingi, ilipolazimishwa sare ya bila kufungana dhidi ya Azam FC, Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

**2. YANGA**

Wakati wiki hii ikiwa haina mechi yoyote ya ligi kutokana na kucheza mechi ya kimataifa, lakini kabla ya hapo ilijikuta ikichapwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam katika mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu, Agosti 28, ikiwa imefuta rekodi yake ya kucheza mechi ya kwanza bila kupoteza kwa misimu minne mfululizo.

Mara ya mwisho Yanga kupoteza mechi yake ya kwanza kwenye ligi ilikuwa ni Septemba 20, 2014, Ligi Kuu msimu wa 2014/15, ikichapwa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro, yaliyofungwa na Mussa Hassan Mgosi na Ame Ally.

**3. AZAM FC**

Wiki hii nayo haikuwa na mechi yoyote ya ligi kutokana na kukabiliwa na mechi ya kimataifa, lakini kwenye mechi yake ya kwanza Agosti 27 iliichapa KMC bao 1-0 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam na kuendeleza rekodi yake safi ya kushinda mechi ya kwanza kwa misimu mitatu mfululizo.

Msimu ambao Azam ilishindwa kutoka na ushindi kwenye mechi ya kwanza ya Ligi Kuu, ilikuwa ni 2016/17 ilipolazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani kwake Azam Complex dhidi ya African Lyon, mechi ikichezwa Agosti 20, John Bocco akiifungia Azam huku Hood Mayanja akiisawazishia Lyon.

**4. KMC**

Kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani mjini Tanga Septemba 13, kumeifanya kufungwa mechi zote mbili mfululizo ambazo imecheza mpaka sasa na kushindwa kuendeleza au kuvunja rekodi yake ya msimu uliopita wa 2018/19 ilipocheza kwa mara ya kwanza Ligi Kuu, ambapo ilitoka sare kwenye mechi zote mbili za mwanzo.

Kwenye mechi ya kwanza Agosti 27, ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam. Msimu uliopita ilianza ligi kwa kutoka suluhu ya bila kufungana dhidi ya JKT Tanzania, na mechi ya pili ikatoka sare bao 1-1 dhidi ya Ruvu Shooting.

**5. COASTAL UNION**

Pamoja na kuifunga KMC mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Mkwakwani mjini Tanga, lakini timu ya Coastal Union imeshindwa kuifikia rekodi yake ya msimu uliopita ilipovuna ponti nne kwenye michezo miwili ya mwanzo.

Msimu huu kwenye michezo yake miwili imejipatia pointi tatu tu. Kwenye mechi ya kwanza msimu huu ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid mjini Arusha, hivyo ushindi iliyoupata Septemba 13 umeifanya kukusanya pointi mbili tu.

Msimu uliopita kwenye mechi ya kwanza ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Lipuli ya Iringa na ikashinda bao 1-0 dhidi ya Biashara United ya Mara kwenye mechi ya pili, mechi zote zikichezwa Uwanja wa Mkwakwani Tanga.

**6. MTIBWA SUGAR**

Kwa mara ya kwanza tangu kuingia kwa mfumo mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2007/08, Mtibwa Sugar inaweka rekodi ya kupoteza mechi mbili mfululizo za mwanzo.

Ni msimu 12, Mtibwa Sugar haijawahi kupoteza mechi mbili za kwanza kwenye ligi, badala yake ilikuwa ikishinda zote mbili, kufungwa moja na kutoka sare moja, au kushinda moja na kutoka sare.

Lakini msimu huu umeanza vibaya kwao, kwani Agosti 25 ilikiona cha moto kwenye Uwanja wa Samora Iringa ilipochapwa mabao 3-1 dhidi ya Lipuli, lakini pia kwenye Uwanja wa Uhuru ikajikuta ikipoteza mechi ya pili dhidi ya Simba kwa mabao 2-1.

**7. SINGIDA UNITED**

Kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Namungo FC kimeifanya timu ya Singida United kupoteza kwa mara ya kwanza mechi mbili mfululizo za mwanzo tangu ilipopanda na kuanza kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2017/18.

Agosti 24, ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Mwadui FC Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga, na Jumamosi iliyopita ikiwa Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi ilikubali kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Namungu FC.

**8. NAMUNGO FC**

Mabao 2-0 iliyoyapata dhidi ya Singida United yameifanya Namungo FC kuweka rekodi ya aina yake ya kupanda Ligi Kuu na kushinda mechi mbili mfululizo za mwanzo.

Tangu kuanza kwa mfumo mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2007/08, hakuna timu yoyote iliyopanda tu na kucheza Ligi Kuu iliyowahi kufanya hivyo.

**9. LIPULI FC**

Tangu ipande Ligi Kuu msimu wa 2017/18, timu ya Lipuli ya Iringa ndiyo kwa mara ya kwanza inashinda mechi zake mbili mfululizo za mwanzo.

Ikiwa nyumbani, Uwanja wa Samora mjini Iringa Agosti 25, Lipuli ilianza ligi kwa kuichakaza Mtibwa Sugar mabao 3-1, na ikiwa ugenini, Uwanja wa Isamuhyo jijini Dar es Salaam Jumamosi iliyopita ilichapa JKT Tanzania bao 1-0.

**10. ALLIANCE FC VS MBAO FC**

Timu hizi zimeweka rekodi ya kucheza mechi za kufungua dimba la Ligi Kuu kwa misimu miwili mfululizo.

Msimu huu zilichezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza na kutoka sare ya bao 1-1 Agosti 24, yakifungwa na Paschal Liponda kwa upande wa Mbao FC na Ibrahim Said akijifunga mwenyewe.

Msimu uliopita timu hizo zilicheza mechi ya kufungua dimba Agosti 22 kwenye uwanja huo huo wa CCM Kirumba, lakini hii Mbao FC ilishinda bao 1-0 lililofungwa na Evergetus Mujwahuzi.

**NAJUA WAJUA**



MANCHESTER United haijawahi kupoteza mechi yoyote kati 134 zilizopita za Ligi Kuu England ikiwa uwanja wa nyumbani wa Old Trafford wakati inapokuwa ya kwanza kufunga (imeshinda 123, sare 11).

SOKA

# LUKAKU ANGEISAIDIA UTD KULIKO POGBA



**LONDON,** England

MCHEZAJI wa zamani wa Arsenal, John Hartson, amesema Manchester United wamefanya makosa makubwa kumuuza Romelu Lukaku kwani mchezaji ambaye alistahili kupigwa bei ni kiungo Paul Pogba.

**Mshambuliaji huyo wa zamani wa Arsenal anaamini kwamba Pogba alitaka kuondoka na timu imegoma kumpiga bei, hivyo jambo linalotokea kwa sasa anajaribu kucheza chini ya kiwango kutokana na hasira za kushindwa kutimiza ndoto zake za kutimkia kule Real Madrid.**

Kwenye dirisha lililopita la majira ya kiangazi, Man United ilimzuia Pogba asiondoke, lakini ilikubali kumpiga bei Lukaku kwenda Inter Milan kwa ada ya pauni milioni 73.

Na tangu Lukaku atue Inter, amepotiwa kutulizana chini ya kocha Antonio Conte, akifurahia maisha yake kuliko alivyokuwa Old Trafford chini ya makocha Jose Mourinho kwanza na baadaye Ole Gunnar Solskjaer.

Na gwiji huyo raia wa Wales, Hartson anaamini mabao ya Lukaku yangekuwa kitu cha msingi zaidi kwenye kikosi cha Man United kuliko kuendelea kuwa na huduma ya ovyo kutoka kwa kiungo Pogba.

Hartson anasema: "Nadhani Man United wamejitengenezea matatizo mengi. Ningekuwa mimi ningemuuza Pogba na kumbakiza Lukaku. Walau Lukaku atakufungia mabao. Alifanya hivyo Everton kwa miaka mitatu mfululizo, amekwenda kufanya hivyo Man United," amesema gwiji huyo katika mahojiano yake na Gazeti la Daily Mail.

"Huyu Pogba, naona watu wanasema anaanza kuonyesha kitu kizuri, hali nzuri, lakini hilo lina ukweli kweli?

"Nadhani anacheza kwa asilimia 75 tu, hamsaidii McTominay, ambaye anajitahidi sana kufanya kitu.

"Dogo McTominay amekuwa akizunguka huku na kule kwenye kiungo, peke yake. Anahitaji msaada kwa mchezaji mkongwe ambaye ni Pogba, lakini yeye hana hata wasiwasi na naamini hii ni sehemu ya mgomo.

"Kosa hili naamini litawagharimu zaidi Man United, kwa sababu hadi sasa, uwapo wa Pogba kwenye kikosi hiki hauonyeshi mchango wake, wachezaji wadogo ndio wameonekana kuwa kwenye kiwango kushinda yeye."

Gwiji huyo anaamini kwamba, kubakia kwa Lukaku hapo Man United kungekuwa na mchango mkubwa zaidi kwa kikosi hicho kuliko hali ilivyo sasa.

"Mabao ya Lukaku yangekuwa kitu cha msingi zaidi kwenye kikosi cha Man United kuliko kuendelea kuwa na huduma ya ovyo kutoka kwa kiungo Pogba ambaye anacheza kama analazimishwa.

"Naamini kwamba, Pogba kwa sasa hana mapenzi kabisa ya kukaa katika kikosi cha Manchester United, anachofikiria yeye ni kutimiza ndoto na hisia zake, kuna uwezekano mkubwa zaidi akaondoka wakati wa dirisha dogo la usajili Januari."

Hata hivyo, Hartson anaona kwamba, kikosi cha Man United msimu huu kitakuwa na wakati mgumu zaidi kwenye safu ya ushambuliaji, kwa sababu muunganiko wa timu ni mdogo na anakosekana mtu wa kulazimisha mashambulizi.

"Ukiangalia namna mashambulizi ya Man Unuted yanavyotengenezwa kwa sasa, ni wazi kwamba, kuna kitu kikubwa kinakosekana - mtu wa kusukumiza mashambulizi langoni mwa timu pinzani.

"Lukaku alionyesha kuwa anaweza kulazimisha safu ya ulinzi ya timu pinzani kuhaha kwa wakati wote - ana nguvu, ana ari na pia anacheza kwa kutafuta mabao tofauti na Pogba.

"Angalia mechi ambayo Man United ilishinda, Pogba nafasi yake ilikuwa ndogo zaidi hata kwenye mchezo dhidi ya Southampton, hakuna alichokifanya, hivyo uwapo wake sidhani kama utaisaidia Man United msimu huu."

Hadi sasa Man United katika mechi zake tano ilizoshuka dimbani za Ligi Kuu, imeshinda mbili, sare mbili na kufungwa moja na ipo nje ya nne bora kwenye msimamo.

KIPA wa Leicester, Kasper Schmeichel amefungwa mabao mengi ya penalti (16) kwenye Ligi Kuu England katika mechi 176 alizocheza kuliko baba yake Peter Schmeichel aliyefungwa mabao ya penalti 15 katika mechi



NDANI YA 18

LIGI ya Mabingwa Ulaya ni sehemu ambayo klabu kubwa za Ulaya zinakutana kwa ajlili ya kupigania zawadi kubwa kwa soka la Ulaya.

Uk. 16&17

# NAFASI 3 UNITED ZA KUZIIMARISHA




ANDER HERRERA

**MANCHESTER,** England

MSIMU mpya wa Klabu ya Manchester United umeenda tofauti kwa mujibu wa mpango wao. 'Mashetani Wekundu' hao wameshindwa kuonyesha kiwango cha kuvutia na mapema tu mwanzoni mwa msimu, inaonekana itakuwa ngumu kwao kumaliza kwenye nne bora.

**Man United ilianza kwa kuonyesha hamasa kubwa kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu, baada ya kuifunga Chelsea mabao 4-0 pale Uwanja wa Old Trafford na kuonyesha kwamba, ina nguvu na itakuwa moto mkali.**

Tangu hapo mambo yameonekana kwenda tofauti kabisa na matarajio ya mashabiki wake. Sare mbili na kupoteza mchezo mmoja kati ya michezo mitatu ya mwisho inaleta ishara mbaya.

United haikujaza nafasi za wachezaji walioondoka wakati wa kipindi cha dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto na hilo tayari limeonekana kuwasumbua sasa.

Usajili wa dirisha dogo la Januari ndilo litakalofuata na hapa tunakuchambulia sehemu tatu ambazo wanatakiwa kuziimarisha kwa kufanya usajili...

**3. KIUNGO WA KATI**

Manchester United ilipoteza mchezaji muhimu wa kiungo wa kati, wakati walipomwachia Ander Herrera kuondoka na kwenda kujiunga na PSG kipindi cha majira ya joto.

Mashetani Wekundu hao walikosea kumwachia Mhispania huyo kuondoka, lakini kwa kuwa lilikuwa ni jambo lisiloepukika, United ilitakiwa haraka kuingia sokoni na kusajili mchezaji wa kuziba nafasi yake. Bahati mbaya hilo halikutokea.

Tangu kuanza kwa msimu huu, imeonekana wazi kwamba, Man United kushindwa kwao kuziba pengo hilo lilikuwa kosa kubwa. Kwa sasa wanakosa kiungo wa kati ambaye ataweza kutoa sapoti ya kuunganisha mipira ya mashambulizi.

Scott McTominay amekuwa ndio chaguo la nafasi hiyo, lakini kiungo huyo raia wa Scotland anatengeneza mashambulizi machache. Nemanja Matic ni mchezaji wa taratibu, huku Fred ndio anabakia kuwa chaguo pekee.

Fikiri kama kiungo ingekuwa inacheza kwa pamoja Herrera na Pogba au Pogba, Herrera na McTominay na hapo unaweza kuelewa nini kinachokosekana kwa United kwa sasa.

**2. WINGA YA KULIA**

Winga ya ushambuliaji ya kulia, ndio ilikuwa kama nguzo kuu ya Manchester United kwa kipindi kirefu. Hata hivyo, safari hii Man United iliamua kutosajili winga wa kulia. Matokeo yake, safu ya ushambuliaji ya Man United inategemea zaidi upande mmoja kwa sasa.

Kwa sasa United imekuwa ikitumia zaidi winga ya kushoto kwenye kuanzisha mashambulizi. Marcus Rashford amekuwa akitumika kama fowadi wa kushoto, huku Daniel James ndio amekuwa akicheza kama winga wa kulia hadi sasa.

Hata hivyo, ukiangalia kwenye mchezo dhidi ya Southampton, raia huyo wa Wales alionyesha kwamba, anaweza kuwa muhimu zaidi kwa kikosi hicho kama atatumika kama winga wa kushoto.

Kikosi hicho cha Solskjaer kwa sasa chaguo pekee la winga ya kulia kwa sasa ni James, Jesse Lingard na Juan Mata, ambapo wote wameshindwa kuonyesha kiwango cha juu.

Kukosekana kwa winga halisi wa kulia wa Manchester United, kumemwathiri kwa kiasi kikubwa mshambuliaji Aaron Wan-Bissaka. Muingereza huyo mara zote ameonekana kama fowadi aliyetengwa na hana sapoti.

Ili kuipa timu uwiano mzuri, Man United wanatakiwa kusajili winga wa kulia ambaye ataweza kuwa kichocheo kizuri cha mashambulizi.

**1. KIUNGO MSHAMBULIAJI**

Baada ya kocha Solskjaer kubadili mfumo wa 4-2-3-1 kipindi cha majira ya joto, ilikuwa ni wazi kwamba, Manchester United ilihitaji kiungo mshambuliaji haraka.

Raia huyo wa Norway amekuwa akimtumia Jesse Lingard kwenye nafasi hiyo, lakini Muingereza huyo ameshindwa kufikia kiwango. Juan Mata alitumika kwenye nafasi hiyo kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa. Bahati mbaya Mhispania huyo ameshindwa kwenda na kasi inayotakiwa.

Kikosi cha sasa cha United pia kinaonyesha ishara ya kukosa ubunifu kwenye winga zote mbili. Ukiacha Paul Pogba na Juan Mata, wachezaji wachache wamekuwa na uwezo wa kupenya safu ya ulinzi ya timu pinzani.

Tatizo hili limeonekana kuwa kubwa zaidi katika mechi za mwanzo mwa msimu na Mashetani Wekundu hapa wamekuwa hawana rekodi ya kupiga mashuti mengi langoni mwa adui. Hivyo, United wanatakiwa kununua kiungo mshambuliaji kipindi cha dirisha dogo la usajili Januari.

James Maddison aliwekwa kwenye rada za Man United kipindi cha majira ya joto na anaweza kuwa chaguo zuri zaidi la kumwongeza wakati wa usajili wa Januari.

Christian Eriksen pia anaweza kuwa suluhisho kwao kama wataweza kumshawishi na kumsajili kutoka kule Spurs na kutua hapo Manchester.

**USILOLIJUA**



WINGA wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, amezawadiwa faulo nane kutokana na kuchezewa madhambi kwenye mechi dhidi ya Spurs juzi; idadi ambayo ni kubwa zaidi kuliko mchezaji yeyote yule kwenye Ligi Kuu England tangu Novemba 2018 (Harry Kane alipochezewa faulo nane kwenye mechi ya Spurs dhidi ya Chelsea).





# DC atoa angalizo wanaobeza mgambo

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

MKUU wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, amezindua mafunzo ya mgambo wilayani humo na kuwatahadharisha wanaobeza kuwa watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Alizindua mafunzo hayo juzi katika Kata ya Chalangwa ambapo ndipo yanapofanyikia na kuwataka vijana kuyatumia mafunzo hayo kubadili tabia na kuwa wenye nidhamu na uchapakazi kwa madai kuwa vijana wa kata hiyo wamekuwa wakitajwa kuwa na tabia mbaya.

Alisema mafunzo hayo yapo kwa mujibu wa sheria na kila kijana anatakiwa kushiriki hivyo akawasisitiza washiriki kuwahamasisha wenzao ili nao washiriki kabla hawajalazimishwa kufanya hivyo.

Aliwapongeza vijana wa kike waliojitokeza kushiriki mafunzo hayo kwa maelezo kuwa wameonyesha ujasiri japo kuwa ni wachache mno ikilinganishwa na wanaume.

Alisema katika mafunzo hayo washiriki wapo 177, lakini wa kike wapo saba pekee hali ambayo inalifanya kundi hilo kuonekana kutokuwa na mwamko.

"Naombeni muwapelekee salamu wale wote ambao hawajajitokeza kwa hiyari kushiriki mafunzo haya waje washiriki kabla hawajachukuliwa hatua na kuna wale wanaobeza hiki kinachofanyika, waambieni watashughulikiwa," alisema Mahundi.

Mahundi alisisitiza kuwa mafunzo hayo mbali na kuwasaidia vijana kuwa wakakamavu lakini pia yanawasaidia kuwa wazalendo kwa taifa lao ikiwa ni pamoja na kushiriki katika kulinda amani ya nchi.

Alisisitiza kuwa mafunzo hayo hayana malipo ya aina yoyote hivyo kila mtu anayeshiriki hachangii chochote na wala hatakiwi kulipwa chochote.

**"Naombeni muwapelekee salamu wale wote ambao hawajajitokeza kwa hiyari kushiriki mafunzo haya waje washiriki kabla hawajachukuliwa hatua na kuna wale wanaobeza hiki kinachofanyika, waambieni watashughulikiwa," alisema Mahundi.**

# Tucta yafunguka mapya kikokotoo kipya cha mafao

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

UONGOZI wa Shirikisho Huru la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (Tucta), umesema upo kwenye mazungumzo na serikali kuhusu namna kikokotoo kipya cha mafao kitakavyokuwa kinatumika baada ya muda uliotolewa na Rais John Magufuli kuendelea kutumia cha zamani utakapokuwa umekwisha.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Mbeya na Rais wa Tucta, Tumaini Nyamhokya, wakati wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (Talgwu) Mkoa wa Mbeya ambao uliambatana na uchaguzi mkuu wa chama hicho.

Nyamhokya alisema awali baada ya kuona madhara ya kikokotoo kipya walianza mazungumzo na serikali kwa ajili ya kuomba kikokotoo kipya kitoe asilimia 40 badala ya 25, lakini wakati wanaendelea na mazungumzo hayo Rais Magufuli aliagiza kiendelee kutumika cha zamani.

Alisema maelekezo ya Rais ilikuwa kikokotoo kipya kianze kutumika mwaka 2023, hivyo wao wanachokifanya sasa hivi ni majadiliano na viongozi wa serikali juu ya namna bora ya utekelezaji wa kikokotoo hicho kipya.

"Tunataka tuone ni namna gani bora kikokotoo hicho kipya kitakavyotumika baada ya mwaka 2023 ili wafanyakazi wasiathirike na wala mifumo ya serikali isiathirike," alisema Nyamhokya.

Katibu wa Talgwu Mkoa wa Mbeya, Sunday Nzaligo, alisema liche ya serikali kuruhusu watumishi kuanza kupandishwa madaraja, lakini bado kuna ukakasi kwenye ngazi ya halmashauri kuhusu utekelezaji wa takwa hilo la kisheria.

Aidha, alisema wapo baadhi ya wakurugenzi watendaji wa halmashauri wamekuwa wakiwahamisha watumishi wa umma kutoka kituo kimoja cha kazi kwenda kingine bila kuwalipa stahili zao kwa mujibu wa sheria za utumishi. Alisema kitendo hicho kinawakatisha tamaa watumishi, hivyo akaiomba serikali kusimamia na kuhakikisha watumishi wanapata haki zao.

"Mheshimiwa Rais, aliagiza watumishi wanaostahili kupandishwa madaraja wapandishwe lakini bado agizo hilo halitekelezwi kama inavyotakiwa, vilevile tunaomba wakurugenzi wazingatie sheria wanapowahamisha watumishi," alisema Nzaligo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Mtinika, ambaye alihudhuria mkutano huo, aliwataka watumishi kuendelea kutimiza wajibu wao ipasavyo wakati wakiendelea kudai haki zao.

Alisema wapo baadhi ya watumishi ambao muda wote wanalalamika na kudai haki zao, lakini hawatekelezi wajibu wao, hivyo alivitaka vyama vya wafanyakazi kuendelea kuelimisha wanachama wao.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwataka wanachama wa Talgwu kuchagua viongozi waadilifu na wachapakazi ambao watasaidia kusukuma mbele maslahi ya wafanyakazi.

Aliwataka wafanyakazi hao kuwaepuka viongozi ambao wanaleta majungu na kuwachonganisha na badala yake wawachague wazalendo watakaowaunganisha hasa wakati wa kudai haki.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kulia), akikabidhi funguo za pikipiki kwa vijana wa bodaboda ambao walikabidhiwa mkopo wa pikipiki 14 na Halmashauri ya Jiji la Mbeya kama sehemu ya utekelezaji wa sheria ya kutenga asilimia 10 kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Mgogoro wa ardhi wachukua sura mpya

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MGOGORO wa ardhi kati ya wananchi wa Kijiji cha Msesule na kikundi cha wakulima wa Mahalala Group wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, umechukua sura mpya baada ya kuzuka mapigano baina yao na kusababisha wanakikundi 11 kujeruhiwa kwa mapanga.

Aidha, wananchi hao wanadaiwa kuharibu pikipiki tano za kikundi cha wakulima kwa kuzibonda bonda na silaha za jadi walizokuwa wamebeba kisha wakazitelekeza eneo la tukio.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Jerome Ngowi, alisema chanzo cha tukio hilo ni ugomvi wa kugombea shamba la umwagiliaji lenye ukubwa wa ekari 300 ambalo kila upande unadai ni mali yake.

Alisema awali shauri la shamba hilo lilikuwa katika Baraza la Ardhi na Nyumba jijini Mbeya na limemalizika hivi karibuni ambapo kikundi cha wakulima cha Mahalala kilishinda, lakini wenzao wa Mahalala wakakata rufani na kabla ya rufani hiyo haijasikilizwa ndipo vurugu zikatokea.

Kamanda Ngowi alisema baada ya kubaini kuwa kuna viashiria vya amani kutoweka, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune alisitisha shughuli zote zilizokuwa zinafanyika kwenye shamba hilo wakati wanasubiri maamuzi ya Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya.

Alisema pande zote mbili zilipuuza agizo hilo la Mkuu wa Wilaya na kila upande ukawa unataka kufanya shughuli zake hali ambayo ilizua mapigano hayo ambayo yalileta madhara kwa baadhi.

"Wanakikundi wa Mahalala waliamua kwenda kusafisha mfereji ili waendelee na kilimo cha umwagiliaji, wakati wanaendelea na kazi hiyo wenzao wa Msesula wakiwa na silaha mbalimbali za jadi waliwavamia na kuanza kwashambulia hali iliyosababisha madhara," alisema Kamanda Ngowi.

Kufuatia tukio hilo, Kamanda Ngowi alisema Jeshi la Polisi lilifanya msako mkali na kuwakamata wananchi wanane wa Kijiji cha Msesule kwa ajili ya mahojiano, huku likimtafuta Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho pamoja na mtu mwingine ambaye jina lake halikuwekwa wazi kwa ajili ya upelelezi.


Aliwataja baadhi ya waliokamatwa ni Denis Segele (36), Annold Kibodi (15), Amos Kita (56), Kapilipili Sichura (35), Kasuka Bulhama (56), Edward Mbangala (37), Nebati Tulyanje (30) na Jumanne Mashaka (52) ambao wote ni wakazi wa Kijiji cha Msesule.

Alisema majeruhi wanane walitibiwa na kuruhusiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mbarali na wengine watatu ambao walipata majeraha makubwa bado wapo katika Hospitali hiyo wakipatiwa matibabu.

Wakizungumzia tukio hilo baadhi ya wanakikundi wa Mahalala ambao wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mbarali walidai kuwa walishindwa kujitetea kwa sababu wenzao hao walikuwa hawana maelezo na walikuwa wanawashambulia.

Mmoja wa majeruhi hao, Bakari Amadi, alisema wakati wanaendelea na shughuli ya kusafisha mfereji, wenzao waliwavamia wakiwa na silaha za jadi kama mapanga, mikuki, mashoka na marungu ambapo walianza kuwashambulia.

"Mimi walinikata kichwani na wenzangu nao walikatwa maeneo mbalimbali ya miili, walikuwa wanasema mmekuja kutafuta nini huku wakati ninyi hamna mashamba lakini kwa sasa tunasubiri tujuwe haki tunaipataje," alisema Amadi.





# Waziri Mpango ataka benki zichunguzwe

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ameagiza Benki Kuu (BoT) kufanya uchunguzi wa kina wa benki na taasisi za kifedha namna zinavyotoza riba ya mikopo kwa wateja kutokana na baadhi kuweka riba kubwa mno.

Agizo hilo alilitoa juzi jijini Dodoma katika mkutano wa chama cha kuweka na kukopa cha Hazina Saccos na hafla ya kugawa hati za viwanja vya eneo la Ihumwa Ngaloni kwa wanachama hao.

Aliitaka BoT kufanya uchunguzi huo kwa kuwa baadhi ya benki na taasisi za fedha zinawaumiza wateja wao kwa kuwatoza riba kubwa kwenye mikopo wanayokopa.

"Hivi juzi nilikutana na taasisi moja ya fedha inawatoza wateja wake riba ya mkopo asilimia 35, hii si sawa. Nawataka BoT kufanya uchunguzi wa namna taasisi hizo zinavyokokotoa riba ya mikopo kwa wateja wao," alisema Dk. Mpango.

Alisema baadhi ya taasisi hizo zinawanyanyasa wananchi wanaochukua mikopo na kusababisha kushindwa kulipa kutokana na kutozwa riba kubwa.

Waziri huyo alisema lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi hawanyonywi kiuchumi na kuibiwa na taasisi hizo.

"Watu wanaofika kupata huduma wanatozwa riba kubwa na wakikwama kulipa wanawachukulia mali zao," alisema Dk. Mpango.

Akizungumza kuhusu saccoss hiyo, Dk. Mpango aliwataka viongozi wake kuendelea kujenga uaminifu wa kutunza fedha za wanachama wake, ili kuweza kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.

"Bahati nzuri na mimi ni mwanachama wenu sijasikia lolote baya kuhusu Saccos hii, kwanza wanawapongeza kwa hatua ya kuwasaidia wanachama wenu kupata viwanja vya makazi hongereni sana," alisema Waziri.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Hazina Saccos, Aliko Mwaiteleke, alisema kwa sasa kuna wanachama zaidi ya 5,600 ambao ni watumishi kutoka serikali kuu, za mitaa na taasisi za umma.

Alisema kazi kubwa ya Saccos hiyo ni kukusanya akiba za wanachama na kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili kutatua changamoto za uchumi ya wanachama wake.

Alimwomba waziri kuwaunganisha na taasisi za kifedha zenye masharti nafuu ili waweze kuviendeleza viwanja hivyo walivyokabidhiwa hati.



Ofisa Ardhi Mteule wa Jiji la Dodoma, Joseph Kamonga (kushoto), akimkabidhi Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango hati ya umiliki ardhi eneo la Ihumwa jijini Dodoma. Waziri huyo ni kati ya wanachama wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Hazina Saccos LTD waliopatiwa hati ya kumiliki ardhi na jumla ya hati 203 zilizotolewa kwa wanachama hao juzi, jijini humo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mabinti watumia mbinu batili ili kuzuia mimba

**Na Renata Msungu, DODOMA**

BAADHI ya wasichana hasa mabinti wanadaiwa kufanya mapenzi kinyume cha maumbile ili kuepukana mimba za utotoni.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya jiji la Dodoma, Sharifa Nabalang'anya, alitoa taarifa hizo mwishoni mwa wiki kwenye mdahalo ulioandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la ESAP Tanzania uliokuwa ukijadili chanzo cha mimba udogoni.

Nabalang'anya alisema ili kujiepuka kubeba mimba za utotoni watoto hao kwa sasa wanajihusisha na mapenzi kinyume cha maumbile, huku akiwataka wazazi kuwasimamia na kuwakagua watoto wao mara kwa mara.

"Wazazi wako 'busy' na shughuli zao hawajui kuwa watoto wao mara baada ya kutoka shule na siku za wikiendi huenda katika vibanda umiza kuangalia sinema tofauti tofauti ikiwamo za mapenzi na kujifunza mambo yasiyofaa ikiwamo mapenzi kinyume cha maumbile," alisema Nabalang'anya.

Alisema ni muhimu wazazi na walezi kujenga tabia ya kukaa na watoto wao na kukagua mienendo yao ya kimaisha na kuwapa elimu ya jinsia badala ya kuwaachia walimu pekee yao.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa ESAP, Joel Katala, aliiomba serikali kuitazama upya sheria ya adhabu kwa watu wanawapa mimba watoto ya kwenda jela miaka 30 kwa wazazi ambao watachangia kuwaficha watuhumiwa.

Alisema wazazi maeneo mengi wamekuwa wakiwasaidia watuhumiwa kukimbia baada ya kuhongwa fedha kidogo na baadaye kuruhusu mtuhumiwa kuendelea na maisha ya ndoa na binti aliyepewa mimba na kukatisha masomo.

"Naiomba serikali iiangalie upya sheria na itoe adhabu ya miaka thelathini kwa wazazi watakaobainika kutenda kosa la kusaidia mtuhumiwa ili kukomesha kabisa tatizo hilo," alisema Katala.

Askari kutoka dawati la jinsia la polisi Dodoma, Amina Mzee, alisema wazazi wamekuwa hawatoi ushirikiano baada ya matukio hayo kutokea.

Alisema wakati mwingine wazazi huwalazimisha watoto wao kusema kuwa hawawajui watuhumiwa hali ambayo uwapa wakati mgumu polisi.

## Wenye taaluma 'haba' pekee kuajiriwa nchini

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema wafanyakazi wa kigeni watakaofanya kazi nchini ni wale tu wenye ujuzi ambao haupatikani nchini.

Majaliwa alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua awamu ya pili ya mafunzo ya ufundi stadi kwa njia ya uanagenzi (apprenticeship) yatakayojumuisha vijana 5,875 yaliyofanyika sambamba na maadhimisho ya miaka 100 ya Shirika la Kazi Duniani (ILO).

Alisema serikali imetoa fursa ya ajira kwa wazawa kwa asilimia kubwa na kwamba wafanyakazi wa kigeni watakaoajiriwa nchini ni wale wenye ujuzi usiopatikana Tanzania.

"Hakuna sababu ya mwekezaji kuja na wafanyakazi kutoka nje wakati mna uwezo huo wa kufanya kazi viwandani," alisema Waziri Mkuu.

Alitaja mafunzo yanayotolewa kwa vijana hao kuwa ni katika fani 14 ambazo ni useremala, uashi, ufundi magari, uchorongaji wa vipuri, ufundi bomba, uchomeleaji na uungaji vyuma, ufungaji umeme wa majumbani na viwandani, ufungaji umeme jua na kuunda kompyuta.

Nyingine ni kuweka terazo na marumaru, kubuni mitindo ya mavazi na ushonaji, mapishi na usindikaji wa vyakula, ufugaji, kilimo cha matunda na mboga, kutengeneza samani kwa kutumia "aluminium" na uchapaji wa nyaraka.

Aliwataka wakuu wa mikoa kuandaa orodha ya vijana waliopata mafunzo ya ufundi stadi ili kuwaunganisha moja kwa moja na fursa pindi wawekezaji wanapokuja katika mikoa yao.

Alisema kuwa orodha hiyo itasaidia vijana kupata ajira wawekezaji wanapofika kwenye mikoa husika badala ya kuja na wafanyakazi kutoka maeneo mengine au nje ya nchi.

" Mkimaliza mafunzo yenu nendeni moja kwa moja kwa Makatibu Tawala wa Wilaya ili wawaingize kwenye orodha ya vijana wenye fani ya ufundi stadi na yeye apeleke kwa RAS (Katibu Tawala wa Mkoa) ili mkoa ujue idadi ya vijana walionao, pindi makongamano au fursa zinapotokea za uwekezaji waelezwe vijana walionao na sifa zao, hakuna sababu ya kuja na wafanyakazi kutoka nje," alisema Waziri Mkuu.



# Waziri ataka wanafunzi kutunzwa bila ubaguzi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, ameziomba taasisi za serikali na binafsi kusaidia wanafunzi waliofaulu mitihani kwa daraja la kwanza bila kujali wamesoma masomo ya kozi gani.

Akizungumza katika hafla ya utoaji zawadi kwa wanafunzi waliofaulu masomo ya sayansi, kidato cha sita kwa ngazi ya daraja la kwanza iliyoandaliwa na Benki ya Watu wa Zanzibar PBZ, alisema:

"Masomo ya sanaa nayo yana umuhimu wake katika ukuzaji wa maendeleo na sekta ya uchumi, hivyo vijana wanaosoma masomo haya wapewe kipaumbele kama wanavyopewa sayansi."

Alisema hakuna maendeleo yatakayopatikana kwa kuhusisha masomo ya sayansi pekee, na kwamba sanaa nayo ina umuhimu wake.

Waziri huyo aliuomba uongozi wa PBZ kuwajumuisha wahitimu wote watakaopata daraja la kwanza katika fani za sanaa kwenye mitihani itakayofanyika Mei mwaka mwaka 2020. Pembe alisema Wizara ya Elimu Zanzibar inafarajika kila ikishuhudia ufauli kwa masomo ya sayansi na sanaa unaongezeka kwa wanafunzi wa Zanzibar, hivyo itaendelea kuwaunga mkono kwa kila hatua hasa katika kuwapatia walimu wa masomo yote, vifaa pamoja na vitabu vya kufundishia ili kutoa hamasa kwao.

Aidha, alitoa wito kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita watakaofanya mitihani kwa mwaka 2020 kuiga na kuongeza bidii na jitihada katika masomo yao ili kupata matokeo bora kama wenzao.

Kwa upande wake Naibu Mkurugenzi PBZ Khadija Shamte Makame, aliiahidi serikali kuendelea kuwasaidia wanafunzi wanatakaofaulu.

Alisema watakaofanya vizuri kila mwaka katika ngazi ya daraja la kwanza watasaidiwa ili kuwaunga mkono wazazi kwani wengi wao ni maskini na hushindwa kuwasomesha watoto kutokana na hali ngumu za maisha.

Alisema wapo baadhi ya vijana hukatisha masomo yao baada ya kufaulu kutokana na kushindwa gharama za malipo kwa elimu ya ngazi ya juu, hivyo PBZ itaendelea kuwashika mkono.

Aidha, Mkurugenzi huyo alisema kila mwanafunzi atakabidhiwa Sh. 1,000,000 na kila alama ya daraja la kwanza aliyoipata mwanafunzi watainunua milioni moja na kuwataka wanafunzi kujiunga na miamala ya kibenki ili kurahisisha huduma za kifedha watakapokuwa chuoni.

"Lengo ni kuwapongeza vijana wa kidato cha sita waliofanya mitihani yao vizuri kwa kiwango cha 'divisheni one' ili kuongeza hamasa vijana wa sayansi kuongeza bidii," alisema Shamte.

Jumla ya wanafunzi 188 waliofaulu kwa daraja la kwanza Zanzibar na wahitimu 93 wamefaulu katika masomo ya sayansi na wahitimu 21 ni kwa fani ya biashara.



Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Hassan Khatibu Hassan (wa pili kushoto), akizungumza kabla hajapokea msaada wa mabati 140 pamoja na vifaa vingine vya kuezekea vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 8 kutoka Benki ya NBC kwa ajili ya kuezekea madarasa manne pamoja na ofisi mbili za walimu za Shule ya Maandalizi Kizimkazi, katika hafla iliyofanyika visiwani Zanzibar mwishoni mwa wiki. Wa nne kulia ni Meneja wa NBC Zanzibar, Ramadhani Lesso. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkutano viongozi wa dini kuanza Zanzibar wiki hii

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

VIONGOZI mbalimbali wa dini wanatarajia kufanya mkutano wa kimataifa mjini Zanzibar, wenye lengo la kuimarisha amani.

Akitoa taarifa ya mkutano huo, Mshauri wa Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar, Shekhe Fadhil Suleiman Soraga, alisema utashirikisha viongozi wa Kiislamu na Kikristo.

Alisema mkutano huo umelenga kuimarisha ushirikiano pamoja na kuangalia namna ya kuendeleza na kuombea amani nchini.

Aidha, alitumia fursa hiyo kuwataka waaumini wa dini ya Kiislamu kuunga mkono juhudi za viongozi wao katika kuimarisha amani na ushirikiano kwa dini nyingine hususan katika ujenzi wa taifa.

Kwa upande wake Askofu Augustine Shao kutoka Kanisa Katoliki Jimbo la Zanzibar, alisema licha ya mkutano kuwa na lego la kuhamasisha amani, lakini pia utasaidia kuitangaza Zanzibar kwa wageni watakaopata fursa ya kuhudhuria mkutano huo.

Alisema Zanzibar ni sehemu inayosifika kwa kuimarisha amani hivyo mkutano huo utasaidia kutoa mafunzo kwa wageni juu ya kutumia nafasi walizonazo katika dini na kuhamasisha waumini wao kuimarisha amani.

Askofu Shao aliwataka waumini wa dini zote kuachana na kauli mbaya zinazochafua imani nyingine ili kuendeleza ushirikiano uliopo baina ya viongozi hao katika kuunga mkono juhudi za serikali juu ya kuimarisha amani.

Mwakilishi kutoka Umoja wa Makanisa Duniani, Dk. Zacneo Motte, alisema wataendelea kushirikiana vyema na viongozi wa dini katika kuimarisha amani kwa mataifa mbalimbali.

Aliwaambia kuwa ili mataifa yaweze kufanya harakati za maendeleo ni lazima kudumisha amani hususan kwa viongozi wa serikali na wa dini.

Katika mkutano huo unaotarajiwa kufanyika Septemba 21 mwaka huu, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Mkutano huo utashirikisha viongozi wa dini kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika, Ulaya na Asia watakaowakilisha madhehebu ya Kikiristo, Waislamu, Wahindu, Wayahudi na za kimatadumi utafanyika kwa siku tatu.

## SMZ yajisifu kuanzisha SUZA

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Zanzibar, imesema kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), ni kutafsiri kwa vitendo dhamira ya kupanua elimu visiwani humo.

Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alisema na kuongeza kuwa kuanzishwa kwa SUZA ni matokeo ya kutafsiri kwa vitendo dhamira ya kupanua fursa ya elimu Zanzibar baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964.

Akizungumza katika hafla ya kusherehekea mafanikio ya SUZA, alisema kuwa Chama cha Afro Shiraz Party (ASP), kilikuwa na dira na malengo ya muda mrefu ya kuandaa rasilimali watu ya kuitumikia nchi ili kusukuma mbele maendeleo ya taifa.

Alisema malengo hayo ya kizalendo yaliyotangazwa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Mzee Abeid Amani Karume, yamefanikiwa hatua kwa hatua kutokana na dhamira ya dhati ya viongozi waliopo ambao kwa pamoja wamechukua hatua madhubuti za kuimarisha maendeleo ya elimu nchini.

Alieleza kuwa hali hiyo imechochea kuwepo kwa hatua za kuimarisha sekta ya elimu kwa kuzifungua fursa za kuanzisha vyuo vikuu Zanzibar kwani kabla ya mwaka 1998, Zanzibar haikuwa na chuo kikuu na vijana wachache waliobahatika walilazimika kusoma vyuo vikuu nje ya Zanzibar.

Alisema kuwa uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ulifanya uamuzi wa kuanzishwa kwa vyuo vikuu nchini kwa kuruhusu kuanzishwa kwa vyuo vikuu viwili vya binafsi mwaka 1998.

Rais Dk. Shein alisema kuwa kwa lengo la kutimiza matakwa ya kisheria na mamlaka aliyonayo, Rais mstaafu , Dk. Amani Abeid Karume, alizindua rasmi SUZA, mwaka 2001 na kumpongeza kwa mchango wake mkubwa alioutoa kiongozi huyo akiwa mkuu wa mwanzo wa chuo hicho.

Dk. Shein ambaye ni Mkuu wa Chuo hicho, alieleza kuwa ni dhahiri kwamba mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 18 ni ya mfano.

Makamu Mkuu wa Chuo, Dk. Zakia Mohamed Abubakar, alieleza historia ya chuo hicho na kufahamisha kuwa kamati ya watu saba iliyoundwa na aliyekuwa Rais wa Zanzibar Dk. Salmin Amor Juma mwaka 1996.

# Fedha zaidi kutengwa kuongeza kambi za JKT

**Na Boniface Gideon, TANGA**

SERIKALI imesema itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuongeza vikosi vya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), vingine ili kuhakikisha wanachukua vijana wote wanaomaliza kidato cha sita nchini.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa JKT, Brigedia Jenerali Charles Mbuge, walipokuwa akifunga mafunzo ya vijana kwa mujibu wa sheria operesheni 'Makao Makuu Dodoma' kutoka kikosi cha 838 KJ Maramba.

Mbuge alisema serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa mafunzo ya JKT kwa vijana mwaka 2016/17 iliridhia kuanzishwa kwa vikosi vipya vitano ili kuongeza uwezo wa kuchukua vijana wengi zaidi.

Jenerali Mbuge alisema serikali inaendelea na majadiliano kuhusu kuongeza muda wa mafunzo angalau yasiwe chini ya miezi sita, ambapo aliipongeza serikali kwa kuyapa kipaumbele mafunzo hayo kwa mujibu wa sheria na kujitolea.

Aliwataka vijana hao waliomaliza mafunzo kuwa tayari kulitumikia taifa lao vyema pamoja na kudumisha umoja na mshikamano wa nchi na kuepuka kuwa kichocheo cha uvunjifu wa amani ya nchi.

Alisema Taifa linahitaji ulinzi na usalama kutoka vijana waliohitimu mafunzo kwani nchi ikiwa na ulinzi na usalama hata uchumi wake huimarika na kuwataka vijana hao kuhakikisha hawayatumii mafunzo waliyoyapata katika kufanya vitendo viovu kwa jamii kwa kuwa wanapaswa kuwa mfano wa bora wa kuigwa. "Shirikisheni idara husika kufichua wahalifu na vitendo vya kiovu na kukemea watu wasiotakia mema nchi yetu kwani mafunzo mliyoyapata yamewajengea uzalendo, uhodari, na ukakamavu kwa sababu JKT inaendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazowakabili pindi mnapo kwenye mafunzo yenu," alibainisha.

Aliwataka wazazi waendelee kutoa hamasa na msukomo katika kuwahamasisha watoto wao kujiunga na mafunzo ya JKT wamalizapo kidato cha sita, kwa kuwa nchi inahitaji vijana wenye uzalendo kwa nchi yao.

"Mtambue mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa na dhumuni la waasisi wetu ni kutoa mafunzo kwa vijana waweze kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali ili kujenga taifa letu na sio kutoa ajira," alibainisha Mbuge.




Mawakala wa bima wa Kampuni ya Bima ya AAR Brokers wakiwa katika mashauriano kuhusu ustawi jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WET**

# Wananchi 15,000 Moro kunufaika maghala sita

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wananchi 15,000 wa wilaya za Kilosa na Mvomero, mkoani Morogoro watanufaika na maghala sita ya kuhifadhia nafaka yaliyojengwa na serikali kwa kushirikiana na wahisani.

Wadau hao ni Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Helvetas ambao wamekarabati na kuyajenga chini ya mradi wa kupunguza upotevu wa mpunga wakati na baada ya mavuno (Ripoma).

Maghala hayo yamegharimu Sh. milioni 508.56 (sawa na Euro 200,000) ikiwa ni sehemu ya mradi wa kuwawezesha wakulima wadogo wanawake na vijana kupunguza upotevu wa mpunga wakati na baada ya mavuno.

Ripoma ni mradi wa miaka mitatu kuanzia Julai 2017 hadi Juni 2020 wenye bajeti ya Euro 1,875,000 (sawa na Sh. bilioni 4.768), na kwamba EU imechangia asilimia 80 na Helvetas asilimia 20 ya utekelezaji wa mradi huo kwa kushirikiana na wadau wengine.

Mradi huo unalenga kushughulikia changamoto zinazokabili kilimo cha mpunga nchini husussan tija ndogo, upungufu wa mazao, upotevu mkubwa kabla na baada ya mavuno, uwezo mdogo wa utunzaji na usindikaji, vikwazo katika kupata huduma za kifedha na mikopo, kutokuwapo kwa soko la uhakika na uhusiano dhaifu katika mfumo soko.

Mradi umenufaisha kaya 3,005 kwa kupitia vikundi 101 vya wakulima wanawake na vijana katika vijiji 36, ambao wamepewa mafunzo ya kilimo bora, usimamizi wa mazao wakati na baada ya mavuno, kuweka na kukopa na kukidhi vigezo vya masoko.

Mafunzo mengine ni usimamizi na uendeshaji wa vikundi, ushirika na maghala, pia tafiti za masoko, ziara za mafunzo na kushiriki maonyesho ya kibiashara.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Stephen Kebwe, alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau hao kwa kuhakikisha wilaya zinaendelea kusaidia utekelezaji wa mradi na maofisa ugani, ikiwamo kutoa huduma bora za mafunzo kwa wakulima.

Alisema maghala hayo yatapunguza upotevu wa mpunga, ikiwamo kuwa pia vituo vya kukusanyia kwa ajili ya kuuza kwa pamoja ili kupata bei nzuri na njia rahisi ya kupata mikopo kupitia benki.

Naye Mwakilishi wa EU, Anna Costantini, alisema wakati wa uzinduzi wa mradi huo, wamechangia kukuza sekta ya mpunga Morogoro na kwamba mbegu iliyopandwa itaendelea kukua.

## Wafanyabiashara wadogo, kati wapongeza mfumo NMB

**Na Happy, SIMIYU**

WAFANYABIASHARA wa wadogo na kati katika Mkoa wa Simiyu wameipongeza Benki ya NMB kwa kuanzisha mfumo wa Klabu Biashara (NMB Business Club) ambao umewawezesha kukuza biashara zao pamoja na mitaji.

Mbali na hilo wafanyabiashara hao, wamesema kuwa mfumo huo umesaidia kwa kiwango kikubwa kuwa na mbinu mpya kila mara na kutumia teknolojia mbalimbali za ukuzaji wa biashara zao ambazo wamekuwa wakipatiwa na benki hiyo kupitia mfumo huo.

Wafanyabiashara hao ambao ni wanachama wa mfumo huo walisema hayo jana wakati wa mafunzo jinsi gani wanaweza kuendesha biashara zao kwa tija na kutokupata hasara yaliyotolewa na benki hiyo kupitia mfumo huo.

Mwenyekiti wa Business Club Mkoa, Christopher Muhama, alisema wao kama wafanyabiashara wamenufaika sana na mfumo huo ambao umewawezesha kukuza mitaji yao na kubadilika katika ufanyaji wa biashara.

Alisema tangu kuanzishwa kwa mfumo huo NMB imewawezesha kupata elimu ya biashara mara sita, ambapo hali hiyo imesababisha kupunguza wafanyabiashara ambao wamekuwa wakikimbia kwa kushindwa kurejesha mikopo.

"Tumekuwa tunafundishwa jinsi ya kufanya biashara kulingana na mazingira na wakati, matumizi mazuri ya pesa, kukuza mitaji, na mfumo huu umewawezesha wafanyabiashara ambao wanashindwa kurejesha mikopo kwenda NMB kufanya mazungumzo ya jinsi gani watarejesha badala ya kukimbia," alisema Muhama.

Mshana Mwanareguma, mmoja wa wafanyabiashara na wanachama wa mfumo huo alisema klabu hiyo, imemwezesha kukuza mtaji wake kutoka 500,000 hadi milioni 30 tangu amejiunga.

Alisema kupitia mfumo huo NMB imewawezesha kuwapa elimu ya jinsi gani wanaweza kufanyabiashara kulingana na wakati huku wakipata mbinu mpya na teknolojia mpya za kukuza biashara zao.

HABARI KIMATAIFA

## Waziri aliyeiba fedha za ebola akamatwa

**KINSHASA, Congo**

WAZIRI wa zamani wa Afya nchini Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Dk. Oly Ilunga ambaye amekuwa akituhumiwa kwa kosa la matumizi mabaya ya pesa zilizotolewa kukabiliana na ugonjwa wa ebola mashariki mwa nchi hiyo, ametiwa nguvuni.

Ilunga alikamatwa juzi akiwa jijini Kinshasa, kesi nyingine tatu za maambukizi mapya zikiripotiwa.

Msemaji wa Jeshi la Polisi jijini Kinshasa, Kanali Pierrot Rombaut Mwanamputu, alisema Dk. Ilunga amewekwa chini ya ulinzi katika kituo cha polisi na atafikishwa mahakamani kesho.

Dk. Ilunga anatuhumiwa kutumia vibaya fedha zilizotolewa na serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kukabiliana na virusi vya ebola, ambapo baadaye alijiuzulu wadhifa wake katika kile alichodai kutokubaliana na majaribio ya chanjo ya pili ya ugonjwa huo.

Wakati hayo yakiarifiwa, kesi mpya tatu za ugonjwa wa ebola zimethibitishwa kwa mujibu wa taarifa iliotolewa Ijumaa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

WHO imesema kesi mbili zimeripotiwa huko Mambasa katika Jimbo la Ituri na Beni Mashariki mwa nchi hiyo.

Eneo la kiafya la Kalunguta mjini Beni mkoa wa Kivu Kaskazini pamoja na Mandima na Mambasa katika Mkoa wa Ituri ndiyo yaliyoathiriwa zaidi na ebola.

Mbali na hayo, takwimu zinaonyesha kuwa kuanzia Septemba 9, kesi 281 zilizoshukiwa kuwa za ugonjwa wa ebola 59 zilithibitishwa na kuwekwa katika vituo 15 vilivyotengwa kutoa huduma ya ebola.

Kwa jumla tangu kuripotiwa kwa maradhi hayo mwaka mmoja uliopita, watu 2,071 wamepoteza maisha na zaidi ya 3,084 wameambukizwa.

**RFI**

**Mbali na hayo, takwimu zinaonyesha kuwa kuanzia Septemba 9, kesi 281 zilizoshukiwa kuwa za ugonjwa wa ebola 59 zilithibitishwa na kuwekwa katika vituo 15 vilivyotengwa kutoa huduma ya ebola.**

# Mugabe kuzikwa baada ya mwezi

**HARARE, Zimbabwe**

MSEMAJI wa familia ambaye ni mpwa wa Rais wa zamani wa Zimbabwe, Robert Mugabe, Leo Mugabe amesema mwili wa shujaa huyo utazikwa baada ya kipindi cha mwezi mmoja.

Awali mipango ya mazishi hayo kufanyika siku ya Jumapili ilionekana kufutiliwa mbali.

Leo alisema mwili wa Mugabe utazikwa katika makaburi ya mashujaa mjini Harare, baada ya familia kukubali.

Kwa sasa mwili wa Mugabe umehifadhiwa katika eneo alilozaliwa baada ya watu kumuaga katika Mji Mkuu wa Harare.

Viongozi wengi wa Afrika wamemsifu Mugabe kama mpiganiaji wa uhuru katika mazishi yake katika uwanja wa kitaifa mjini Harare.

Rais wa sasa wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa alimtaja Mugabe kama kiongozi aliyekuwa na maono na kusema kwamba: "Taifa letu linalia".

Uchumi wa taifa hilo upo katika hali mbaya na raia wengi wa Zimbabwe waliamua kususia sherehe hiyo kutokana na ukandamizaji uliotekelezwa na uongozi wa Mugabe.

Kupanda kwa hali ya mfumuko na ukosefu wa ajira ni baadhi ya masuala ambayo yamewafanya raia wa taifa hilo kumlaumu Mugabe.

"Tunafurahia kwamba amefariki, kwa nini nihudhurie mazishi yake? Sina mafuta, hatutaki kusikia chochote kumuhusu tena. Yeye ndio sababu ya matatizo yetu," alisema mkazi mmoja wa Harare.

Mazishi hayo yalifanyika baada ya mgogoro kati ya familia ya Mugabe na serikali kuhusu mahala atakapozikwa.

Mugabe ambaye alikuwa na umri wa miaka 95 alifariki wiki iliopita alikuwa akitibiwa nchini Singapore.

Kulikuwa na jua na raia wachache walikwenda kutoa heshima za mwisho kwa kiongozi huyo.

Viongozi wa Afrika na wa zamani na waliopo sasa waliingia katika uwanja huo kwa shangwe kubwa pamoja na viongozi waliopigania uhuru wa Bara la Afrika.

Sifa za Mugabe kama mpiganiaji uhuru zilitolewa na kila kiongozi ambaye alisimamna kuhutubia akiwamo Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta.

Rais Kenyatta alisisitiza kwamba matatizo ya Kiafrika yanahitaji suluhu ya kiafrika.

Hata hivyo, matamshi ya Rais Kenyatta yalitofautiana na maneno yaliotolewa na mwakilishi wa familia hiyo Walter Chidhakwa aliyesema kwamba: "Mugabe alikuwa na huzuni, huzuni mkubwa".

Matamashi yake yalionyesha wazi wasiwasi uliopo kati ya serikali iliopo na familia ya Mugabe.

Zaidi ya viongozi 10 wakiwamo wa zamani wa mataifa ya Afrika walihudhuria mazishi hayo, wakimsifu Mugabe kama kiongozi wa Afrika aliyeamua kutumikia maisha yake yote kwa raia wa Zimbabwe.

Baadaye raia walimzomea Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa ikionekana kuwa ni jibu la ghasia dhidi ya wageni nchini kwake.

Rais Ramaphosa alitambua kelele hizo kwa kusema: "Katika wiki mbili zilizopita, sisi Waafrika Kusini tumekuwa tukikabiliwa na wakati mgumu. Tumekuwa na vitengo vya ghasia katika baadhi ya maeneo ya Afrika Kusini...hili limesababisha kama ninavyowasikia mkisema ... vifo na majeraha miongoni mwa idadi ya watu."

Lakini alisisitiza "Sisi Waafrika Kusini hatupendi ghasia dhidi ya wageni".

**BBC**



Askari wakiwa wamebabe mwili wa aliyekuwa Rais wa Zimbabwe, Robert Mugabe. **PICHA: AFP**

# Tunisia wapiga kura kumchagua rais mpya

**TUNIS, Tunisia**

WANANCHI wa Tunisia jana walipiga kura kumchagua rais mpya wa taifa hilo.

Uchaguzi huo ulitazamiwa kuwa ni kichocheo cha kukuza demokrasia kwenye nchi hiyo iliyotumbukia kwenye matatizo ya kiuchumi na matokeo ya vurugu.

Wagombea 26 wanawania katika uchaguzi huo wa pili wa demokrasia tangu yalipofanyika mapinduzi mnamo mwaka 2011 yaliyosababisha kuondolewa madarakani kiongozi wa muda mrefu Zine El Abidine Ben Ali.

Wagombea wakuu katika uchaguzi huo pamoja na Waziri Mkuu, Youssef Chahed na Abdelfattah Morou, Naibu Mkuu wa kundi la wanaharakati wa Kiislamu la Ennahda lenye ushawishi mkubwa nchini Tunisia.

Mwingine ni mfanyabiashara maarufu, Nabil Karoui, anayemiliki kituo cha televisheni na ambaye alikamatwa mwezi uliopita kwa tuhuma za utapeli wa pesa na ukwepaji kodi.

Mahakama nchini Tunisia siku ya Ijumaa ilikataa ombi la kutaka Karoui anayezuiliwa aachiwe huru.

Wafuasi wake wanasema tuhuma hizo zinalenga kumuharibia kisiasa mgombea wao. Vile vile kwenye kinyang'anyiro hicho yupo Abdelkarim Zbidi aliyehudumu mara mbili kama waziri wa ulinzi, wakati wa utawala wa Beji Caid Essebsi na kwenye uchaguzi huu amesimama kama mgombea huru.

Jana, wagombea wawili walijitoa kwenye uchaguzi huo na kutangaza kwamba wameamua kumuunga mkono waziri huyo wa ulinzi.

Wagombea wawili wanawake kwenye kinyang'anyiro hicho ni pamoja na Waziri wa zamani wa Utalii, Salma Loumi na mwanasiasa, Abeer Mousa, ambaye ni mpambe wa kiongozi wa muda mrefu aliyeng'olewa madarakani, Zine El Abidine Ben Ali.

Uchaguzi huo wa Rais, uliopangiwa kufanyika mwezi Novemba, mwaka huu umesogezwa mapema baada ya Rais wa kwanza kuchaguliwa kidemokrasia nchini Tunisia, Beji Caid Essebsi, kufariki dunia Julai, mwaka huu, miezi mitano kabla ya kufikia mwisho wa kipindi chake.

Takriban wapigakura milioni 7.2 wamesajiliwa kushiriki katika uchaguzi huo.

Vituo vya kupigia kura vilifunguliwa saa mbili asubuhi na kuwa wazi kwa muda saa 10. Baada ya kura kuhesabiwa na iwe hakuna mshindi wa wazi basi itafanyika kura ya pili katika tarehe maalum ambayo bado haijatangazwa.

Matokeo ya awali ya uchaguzi huo yanatarajiwa kutangazwa na Tume ya Uchaguzi wiki ijayo siku ya Jumanne.

Tunisia, ndio chimbuko la harakati na maandamano ya kutetea demokrasia ya 2010 na 2011 yaliyozikumba baadhi ya nchi za Afrika Kaskazini.

Maandamano hayo ya kupinga viongozi waliosalia madarakani kwa miongo kadhaa yanachukuliwa kuwa ni mafanikio ya kidemokrasia.

DW

# Waziri amweka njiapanda mkandarasi

**Na Friday Simbaya, IRINGA**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amemtaka mkandarasi kukamilisha mradi wa kusimika transfoma mbili za vituo vidogo vya umeme katika eneo la Mtera unaotarajia kuhudumia zaidi ya vijiji 70 vya mkoa wa Iringa na Dodoma kutokana na adha kubwa inayowakabili wakazi wa maeneo hayo.

Mkandarasi anayetekeleza mradi wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Mtera, ameagizwa kumaliza kazi hiyo ifikapo Oktoba 4, mwaka huu, ili kuwezesha vijiji hivyo kupata umeme wa uhakika.

Dk. Kalemani alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika kituo hicho na kutoridhishwa na kasi ya mkandarasi, kampuni ya Sunir kutoka Iran.

"Mwaka 2017, Novemba tulimpa mkandarasi huyu kazi ambayo alipaswa kumaliza ndani ya miezi 18, lakini hajafanya kazi vizuri na kazi zinazofanyika hapa haziendani na hatua ambayo ilibidi ifikiwe kwa sasa," alisema Dk. Kalemani.

Aidha, baada ya kufika kwenye eneo la mradi huo, Dk. Kalemani alikuta vibarua wanne tu wapo kazini na mkandarasi wa kampuni hiyo kutoka nchini Iran hakuwepo eneo la kazi, hivyo kumwagiza msimamizi wa mradi huo kutoka Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kuhakikisha mkandarasi huyo anaongeza vibarua.

Pia aliagiza mkandarasi huyo kutoka Iran ahakikishe anafika nchini ndani ya siku tatu ili kuchukua hatua zitakazowesha mradi huo kutekelezwa kwa kasi.

Alisema kituo hicho kitafungwa transfoma mbili zenye uwezo wa 10MVA kila moja na fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo ni Dola za Marekani milioni 3.2.

"Transfoma hizi kwa sasa bado zipo bandarini, lakini natoa maelekezo kwa Tanesco na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kuhakikisha kuwa transfoma hizo zinatolewa bandarini ndani ya siku tano ili zifungwe na kufanya kazi," alisema Dk. Kalemani.

Alisema awali kituo cha kupoza umeme cha Mtera kilijengwa kwa ajili ya kuhudumia eneo hilo lenye mitambo ya kuzalisha umeme pekee, lakini serikali iliamua kukipanua kituo hicho ili kuweza kuhudumia pia maeneo ya vijiji vya jirani.

Katika ukaguzi huo wa kushtukiza, Waziri wa Nishati, aliambatana na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Amos Maganga.

Alisema walipotembea mradi na kusikitishwa na hali ya maendeleo ya mradi kusua na kutoa maagizo kwa mkandarasi ndani ya siku tano ameleta transfoma hizo kutoka bandarini na kuanza kuzifunga mara moja.



Daktari Bingwa wa Watoto kutoka Muhimbili, Dk. Augustine Masaswe, akiwaelezea wafanyakazi wa Tigo Tanzania kuhusu njia mbalimbali za kuzuia kuzaa watoto njiti. Zoezi hilo lilizinduliwa mwezi uliyopita na Taasisi ya Doris Mollel Foundation. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


## POST OF EXECUTIVE SECRETARY (TAOMAC)
### Location: Dar es Salaam

**TAOMAC OVERVIEW**

Tanzania Association of Oil Marketing Companies (**TAOMAC**) was registered on March, 23, 2000 under the Registrar of Societies in the Ministry of Home Affairs. Objective of TAOMAC is to be a **Service Provider's Platform** for Oil Marketing Companies (**OMCs**) that are in the business of importation, storage and distribution of petroleum white products (Diesel, Petrol, Jet A1 and Kerosene) as well as lubricants and bitumen. TAOMAC operates under a board of Governors (BOG) whose members are elected at AGM. Executive Secretary is accountable for and operates the day to day affairs of the Association and reports to the BOG and to AGM.

**ROLE AND RESPONSIBILITIES**

TAOMAC is recruiting for an **EXECUTIVE SECRETARY (E.S.) to the BOG** who shall be required to execute various roles and responsibilities including but not limited to: -

- Manage TAOMAC office on daily basis and execute routine activities.
- Plan and implement advocacy and to network closely with Prime Minister's Office, Key Stakeholder Ministries and Agents that have direct interests in the importation and marketing of petroleum products; (i.e. Finance -TRA; Infrastructure -TPA, TASAC; Trade -TBS & WAMA; Water- EWURA and Energy-PBPA).
- Address the common constraints facing the OMCs activities and assist to look for and provide solutions.
- Organise and conduct meetings of BOG, AGM, EGM and all adhoc members meetings when called to meet with Ministers, officials and or respective Agents.
- Develop and implement strategies aimed at promoting TAOMAC Vision, Mission and Goals through development of Budgeted Action Plan (BAP).
- Coordinate and actively work with Tanzania Private Sector Foundation (TPSF) in the implementation of Blue Print Action Plan (BPAP) and National Private Sector Development Policy, 2019, with objective of securing enhanced Representation of Private Sector Interests by the Government mandating individuals and enterprises joining at least ONE of private sector organisation and ultimately to secure SINGLE VOICE of Private Sector.
- Any other duties as may be assigned by the BOG from time to time.

**QUALIFICATIONS REQUIREMENTS**

- An applicant should have 10 years' experience or more, working in the Government or private sector in senior management position. Holder of a Master's Degree in Economics, or Finance, or Legal or any of the related fields.
- Must have excellent communication (oral and written) skills, presentation skills, and public speaking skills.
- Must have integrity and accountability with a proven clean track record.
- Must provide reference from previous employers.
- Previous experience within the downstream oil industry would be an added advantage.

**Mode of Application:**
All applications shall be sent to
VOUCHER NUMBER 1309
P.O. BOX 9033
DAR ES SALAAM.

xxxxxxx


# Dawa ya ukatili wanawake, watoto kifamilia yaelezwa

**Na Mwandishi Wetu, NZEGA**

IMEELEZWA kuwa uanzishwaji wa vikundi vya malezi kwa familia utasaidia kwa kiasi kikubwa kupambana na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika familia hasa kwa watoto vinavyoendelea kushamiri kila uchao.

Hayo yamebainika wakati wataalamu kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii walipokuwa wakitoa elimu ya malezi ya familia na kuratibu uanzishwaji wa vikundi vya malezi katika kata mbili za Halmashauri ya Mji wa Nzega mkoani Tabora.

Akizungumza katika Kata ya Nzega Magharibi, Mkurugenzi Msaidizi Familia kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Tausi Mwilima, alisema mwaka 2015 serikali ilikuja na kitini cha malezi kwa familia kilicholenga kutoa elimu kwa Maofisa Maendeleo ya Jamii kuanzia ngazi ya mkoa hadi kata ili wakaitoe elimu hiyo kwa jamii na kuwezesha uanzishwaji wa vikundi vya malezi vitakavyosaidia mapambano ya kuondokana na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika jamii.

Aliongeza kuwa lengo la kuanzishwa kwa vikundi vya malezi katika jamii ni kuisaidia jamii kupata elimu sahihi ya malezi ili kuondokana na vitendo vya kikatili. Tausi alisema jamii ina wajibu wa kuhakikisha kuwa watoto wanapata malezi bora ambayo yatamweka mbali na vitendo vya ukatili ambapo kwa sehemu kubwa vimekuwa vikiwaharibu watoto hasa kisaikolojia.

Aliongeza kuwa serikali katika kuhakikisha vikundi hivyo vinapata nguvu ya kutekeleza wajibu wao, inaratibu utoaji wa elimu ya malezi ya familia ambayo itawasaidia kuwapatia wazazi au walezi nyenzo muhimu za namna ya kuwapa malezi bora watoto katika jamii.

Tausi alisisitiza vikundi vya malezi kusimamia vizuri malezi bora kwa watoto na kuwezesha kuwa na taifa lenye kuwajibika katika kuwajenga watoto katika malezi.

"Vitendo vingi vya ukatili kwa watoto vinafanywa na wazazi/walezi na watu wa karibu, hivyo tunahitaji elimu ya malezi ili kuhakikisha tunatokomeza vitendo hivi," alisema Tausi.

Katibu wa kikundi cha malezi cha Happy kilichopo Kata ya Nzega Magharibi, Neema Nogigwa, alisema elimu ya malezi ya familia waliyoipata imewapa nguvu na ujasiri wa kuzifikia familia na kuzipata elimu hiyo na watoto walioathirika na vitendo vya ukatili.

Ameongeza wanaahidi kuzifikia jamii ambazo hazijapata elimu ya malezi ya familia ili kuzuia ukatili dhidi ya watoto nchini.

Naye mjumbe wa kikundi cha malezi cha Happy kilichopo Kata ya Nzega Magharibi, Salvasia Kapalata, alisema mafunzo ya elimu ya malezi waliyoyapata wataitoa kwa vikundi vingine katika maeneo yao ili kuisaidia jamii kuondokana na vitendo vya ukatili katika familia zimekuwa mara nyingi familia zimekuwa zikifanya vitendo vya ukatili bila kujua kama wanawakatili watoto.

# Biteko: Kila mmoja atimize wajibu wake

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amewataka wachimbaji wa madini nchini kutimiza wajibu wao kwa kuwa serikali imeshatimiza na inaendelea kutimiza wajibu wake kwa wachimbaji na wadau wengine katika sekta ya madini.

Alisema hayo Jumamosi mkoani Geita wakati akizungumza na wachimbaji wa madini ya ujenzi eneo la Katoro.

Akiwa njiani kuelekea Bukombe, Biteko aliongea na wachimbaji hao kwa kuwasisitiza kulipa kodi ya serikali na tozo nyingine kama sehemu ya kutimiza wajibu wao na kuunga mkono maamuzi ya Rais, John Magufuli aliyewasikiliza kiliochao, kuhusu utitiri wa kodi zilizokuwa kero kwa wachimbaji na Rais kuamua kuziondoa.

Biteko aliwaambia wachimbaji madini kote nchini kuwa, kwa sasa ni zamu yao kutimiza wajibu wao kwa kulipa kodi, kuunga mkono jitihada alizozionyesha Rais Magufuli zilizopelekea mageuzi makubwa katika sekta ya madini.

Wakati huo huo, Biteko ambaye ni Mbunge wa Bukombe ameungana na Waziri wa Nishati Dk. Medard Kalemani katika kukagua utekelezaji wa ilani ya chama tawala katika Jimbo la Bukombe katika usambazaji wa umeme kwa wananchi. Pamoja na kusikiliza kero za wana Bukombe kuhusu umeme mawaziri hao, wamejionea kusua sua kwa usambazaji wa umeme na hatua iliyofikiwa jambo lililopelekea kung'olewa kwa Meneja wa Tanesco Wilaya ya Bukombe kwa kushindwa kutekeleza wajibu wake.

"Mhe Kalemani leo mimi sina cha kuongea ujio wako wana Bukombe wanasubiri kusikia kutoka kwako umeme utawaka lini, kwani wamekuwa wakikuona kwenye vyombo vya habari mara Kilimanjaro, Songea, Tanga ukipita ukiwasha umeme Wanabukombe nao leo wanapenda wakuone ukiwasha umeme hapa kwao," alisema Biteko.

Naye Dk. Medard Kalemani alitolea majibu kero zote zilizowasilishwa na Biteko kwa niaba ya wananchi wake.

"Mhe. Waziri, kwanza nikupongeze kwa kazi kubwa na nzuri unayoifanya kwa wananchi wako. Pili, nimekuja hapa mara mbili na leo mara ya tatu maagizo niliyoyatoa awali naona hayajatekelezwa, sasa nasema hivi, Meneja wa Tanesco Wilaya ya Bukombe kuanzia sasa namfuta kazi sio meneja tena wa hapa Meneja wa Kanda tafuta kwa kumpeleka hapa lete mwingine kesho."

# Wafurahia huduma baada ya mtumishi kusimamishwa

**Na Ndalike Sonda, KAHAMA**

BAADHI ya wananchi wa Kijiji Cha Sangilwa Kata ya Mondo katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, wamesema wameanza kuitumia zahanati ya kijiji hicho kupata huduma ya matibabu baada ya halmashauri hiyo, kumsimamisha kazi mtumishi mmoja aliyekuwa anatuhumiwa kuwataka kimapenzi wagonjwa wanawake wanaokwenda kutibiwa.

Wakizungumza na Nipashe wananchi hao Anna Kulwa, Chausiku Maganga na Masanja Juma walisema kwa sasa wamekuwa na imani kubwa na huduma zinazotolewa kutokana na serikali kusikiliza kero iliyokuwa ikiwakabili wananchi wa eneo hilo, dhidi ya mtumishi huyo.

Walisema awali wagonjwa wengi hasa wanawake walianza kutembea umbali mrefu kwenda katika kata jirani ya Kagongwa na Mwendakulima ili kupata huduma ya matibabu kwa kuwa walishindwa kuwa na imani na huduma inayotolewa katika zahanati yao ya Sangilwa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sangilwa, Vincent Mayala, alisema wananchi kwa sasa hawazungumzii jambo hilo baada ya halmashauri kumsimamisha kazi mtumishi huyo, huku muuguzi wa zahanati hiyo, Jacklini John, akiwataka wananchi kuitumia zahanati hiyo.

Hivi karibuni, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Anderson Msumba, aliliambia Baraza la Madiwani kuwa wamemsimamisha kazi mtumishi wa zahanati hiyo, kwa tuhuma za kuwataka kimapenzi wanawake wanaokwenda kutibiwa.

Musumba alisema hiyo si mara ya kwanza kwa mtumushi huyo kuwa na tuhuma kama hiyo, na kuwa mara ya kwanza alituhumiwa katika Kituo cha Afya Mwendakulima na akahamishiwa katika Zahanati ya Sangilwa.

Diwani wa Mondo, Kija Peja, alipongeza halmashauri hiyo kwa hatua waliyoichukua na kuwataka wananchi kuendelea kuitumia zahanati hiyo, huku akiwataka watumishi wa zahanati hiyo kufanya kazi kwa misingi ya taaluma yao.



Mkazi wa Dar es Salaam akiwa amebeba nyasi kwa ajili ya malisho ya mifugo yake ili kutekeleza sheria inayowabana wafugaji wa mijini mifugo kutozurura ovyo mitaani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polepole aagiza mamilioni kwa vijana, wanawake

**Na Alphonce Kabilondo, GEITA**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Modest Apolinary, kutenga Sh. milioni 200 kwa ajili ya vijana zaidi ya 300 na wanawake ili waanzishe kiwanda cha kufyatua matofali na kiwanda cha kati cha kusindika matunda.

Alitoa agizo hilo wakati akizungumza na viongozi wa CCM, wakuu wa idara, wakurugenzi wa halmashauri pamoja na wakuu wa wilaya.

Alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel Luhumbi, kusimamia fedha hiyo na mchakato wa ujenzi wa kiwanda cha kufyatua matofali, na kiwanda cha kusindika matunda kwa ajili ya wanawake vyote vikamilike kufikia Desemba mwaka huu.

Polepole alisema kati ya fedha hiyo kiasi cha Sh. milioni 100 kitumike kwa ajili ya kuwajengea uwezo vijana na wanawake na kiasi cha Sh. milioni 100 kitumike kwa ajili ya kuanzisha viwanda hivyo na kununua vifaa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji Geita, na kuagiza utenge kiasi cha Sh. milioni 200…vijana hawa zaidi ya 300 pamoja na wanawake waanzishe viwanda vya kati wafyatue matofali na kusindika matunda," alisema na kuongeza:

"Mkuu wa Mkoa nakuagiza simamia mchakato ukamilike haraka kufikia mwezi Desemba mwaka huu."

Katibu huyo aliwataka viongozi wa chama hicho pamoja na wanachama kuhakikisha wanachagua na kupitisha majina ya wagombea wa nafasi za wenyeviti wa serikali za mitaa ambao ni madhubuti wasiopenda rushwa, huku akiwataka vijana wa Jumuiya ya Vijana( UVCCM) kutembea kifua mbele na kuwaonya viongozi wanaowazuia vijana wa umoja huo, kufanya kazi kwa chuki zao binafsi.

Mhandisi R Gabriel Luhumbi alimwakikishia katibu huyo kuwa ujenzi wa viwanda hivyo kwa Mji wa Geita unawezekana kutokana na Halmashauri ya Mji wa Geita kuongoza kwa ukusanyaji wa mapato nchini na kuwa na utajiri wa madini ya dhahabu.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Geita, Mhoja Mapande, alisema kashfa za EPA, Richmond na Esscrow, na ufisadi, ukosefu wa dawa ya kwenye hospitali zilisababisha kupoteza baadhi ya mitaa mwaka 2014 katika uchaguzi wa serikali na mitaa sasa mambo ni safi kwa kuwa Rais Magufuli amemaliza kero hizo.



# GUARDIOLA

## ASIFIA KIWANGO NORWICH BAADA YA KIPIGO

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amewapongeza Norwich City baada ya kuweka rekodi ya aina yake kwenye Ligi Kuu ya England ikiishushia kipigo Manchester City cha mabao 3-2.

Norwich hawakuwa na wachezaji 11 wa kikosi cha kwanza kutokana na majeruhi na hivyo kocha, Daniel Farke alilazimika kuwatumia hadi magolikipa wa akiba kwenye benchi.

Norwich City ambayo ilipanda daraja msimu huu ilisitisha nafasi ya Man City kucheza mechi 18 mfululizo bila kufungwa kwenye mchezo huo uliokuwa wa kusisimua.

Shambulio la Kenny Mclean kutoka katika kona liliwaweka kifua mbele wachezaji hao wa baada ya dakika ya 18 kabla ya kuongeza uongozi wao baada ya dakika 30 wakati walipovamia lango la Man City huku mchezaji, Todd Cantewel akifunga.

Sergio Aguero alipunguza uongozi huo wa Norwich kupitia bao la kichwa kabla ya kipindi cha kwanza kukamilika, lakini Teemu Pukki alichukua fursa ya masihara ya Nicolas Otamendi mapema katika kipindi cha pili kuongeza bao la tatu.

Hata hivyo, shambulizi la Rodri karibu na eneo la hatari zikiwa zimesalia dakika mbili liliipatia City matumaini, lakini Norwich ilihimili kishindo cha mashambulizi ya Man City na kupata ushindi wao wa pili msimu huu.

Klabu hiyo ya kocha Farke iliondoka katika mkia wa jedwali la EPL na kupanda hadi nafasi ya 12, huku City ikisalia katika nafasi ya pili, lakini wakiwa pointi tano nyuma ya viongozi wa ligi hiyo, Liverpool.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Guardiola alisema Norwich walicheza mpira mzuri na wamepata matokeo mazuri.

"Kuna wakati mambo kama haya hutokea kwenye soka - tulikuwa na nafasi ya kufunga, lakini tukashindwa, hivyo nawapongeza Norwich," alisema Guardiola.

"Ndio soka lilivyo - tulikuwa na nafasi nyingi zaidi leo (juzi), wao walikuwa na nafasi tatu na wakafunga mabao matatu.

"La kwanza ulikuwa ni uzembe wa kushindwa kujilinda, bao la pili lilikuwa ni shambulizi la kushtukiza na la tatu lilitokana na makosa yetu, lakini tunajua wapi tulipo kama timu, tunajua nini tumefanya na tunajua wapi tunakwenda.

"Nawapenda wachezaji wangu na najisikia fahari kuwa na wao kwenye timu. Hawakutengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini walipata mabao matatu - tulicheza na Bournemouth na walikuwa na nafasi nyingi kuliko Norwich walichokifanya leo (juzi), lakini tulishinda mchezo ule wa soka wakati mwingine linaweza kukufanya hivyo."

"Hata tulipokuwa nyuma kwa mabao 2-0, tulijua kwamba bado tupo mchezoni kwa sababu tunaweza kutengeneza nafasi za kufunga," aliongeza kusema Guardiola.

"Lakini bao la tatu lilituumiza kwa sababu ndio tulianza kipindi cha pili na tulikuwa pale kuhakikisha tunarudisha mabao, lakini mwisho wa siku haikutokea hivyo. Kwenye soka mara zote unatakiwa kuepuka makosa.

"Kwa uhakika wana timu nzuri pamoja na wachezaji wenye ubora, tuliwaona wakati wakiwa daraja la kwanza mwaka jana."

## MADRID SASA YAPANIA KUMNG'OA MO SALAH

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid sasa imepania kumsajili mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto kijacho.

Kwa mujibu wa Gazeti la Marca, Rais wa Real Madrid, Florentino Perez amemtambua Salah kuwa ni mchezaji wa muhimu zaidi kusajiliwa pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Wakati Madrid ikimnasa Eden Hazard dirisha lililopita la majira ya joto, ilikwama kuwachukua Paul Pogba na Neymar ambao waligomewa na timu zao.

Hata hivyo, taarifa kutoka Hispania, Perez ameanza mipango ya mwakani kuboresha kikosi hicho, ambapo kwenye rada amewaweka Kylian Mbappe na Harry Kane, huku akiamini atatua kunasa saini ya Salah mwishoni mwa msimu huu.

Imeelezwa kwamba, Perez yupo tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 187 kwa ajili ya kunasa saini ya nyota huyo wa kimataifa wa Misri kutoka pale kwenye dimba la Anfield.

Jambo hilo linadaiwa litaibua vita kali kwa sababu Liverpool haitamruhusu aondoke baada ya kiwango bora anachokionyesha, akishinda Kiatu cha Dhahabu kwenye Ligi Kuu England kwa misimu miwili mfululizo na wala hawana hofu kwa sababu katika mkataba wake bado umebakiza miaka zaidi ya mitatu.

## FATI ANA KITU CHA ZIADA - VALVERDE

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde amemwelezea Ansu Fati kama "ana kitu fulani maalumu" baada ya kinda huyo kufunga wakati wakiibuka na ushindi wa 5-2 dhidi ya Valencia Jumamosi.

Akianza kwenye kikosi cha kwanza kwa mara ya kwanza, Fati alihitaji dakika saba tu kuonyesha umuhimu wake hapo Camp Nou, akianza kwa kufunga bao la kuongoza kabla ya kumtengenezea pasi nzuri Frenkie de Jong aliyeifungia Barca bao la pili.

Fati, mwenye umri wa miaka 16 na siku 318, alikuwa mchezaji kijana zaidi kufunga bao kwenye historia ya La Liga, na mchezaji kijana zaidi kufunga na kutoa pasi ya mwisho kwenye La Liga katika karne ya 21.

Valverde alipaza sauti kwa kijana huyo ambaye hadi sasa amefunga mabao



mawili ya La Liga kwa Barca - akisifia kiwango chake na kusema ni tofauti na matarajio.

"Yeye ni mchezaji ambaye ana kitu fulani maalumu. Kwa umri wake inaonekana ana mengi zaidi akipevuka," alisema akiiambia televisheni ya Movistar.

"Kile unachokiona kwenye mazoezi unakiona hapa. Leo ilikuwa ni kitu kilichovutia zaidi, alifunga, akatoa pasi ya mwisho na akakaribia kufunga jingine."

Fati alitengeneza ushindi kwa Barca kabla ya mabao ya kipindi cha pili ya Gerard Pique na Luis Suarez aliyefunga mawili kukiwezesha kikosi hicho cha kocha Valverde kupata pointi saba kutoka mechi nne za La Liga.

Kutokana na kiwango cha Fati, Valverde akaenda mbali na kumfananisha na nyota Lionel Messi, ambaye ni majeruhi akisumbuliwa na maumivu ya kigimbi cha mguu.

"Sihofii kuhusu kumlinganisha," aliongeza.

"Mpira unakwenda kuwa mkubwa na tunatakiwa kuwa makini."

Barcelona ipo nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi ikipitwa na Atletico Madrid kwa pointi tisa, Real Madrid (nane) na Athletic Bilbao (nane).

Barcelona inarudi dimbani Jumanne katika mchezo dhidi ya Borussia Dortmund ukiwa ni wa ufunguzi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi.

HABARI MICHEZO




# VAN DIJK

## AKUNWA NA KIWANGO CHA FIRMINO

**LIVERPOOL, England**

VIRGIL van Dijk amemsifia mchezaji mwenzake wa Liverpool, Roberto Firmino kwa kiwango kizuri alichokionyesha akitokea benchi wakati wa ushindi wa Jumamosi wa 3-1 dhidi ya Newcastle United - na anajisikia vizuri zaidi kutocheza dhidi ya nyota huyo wa Brazil.

Firmino aliichezea mechi mbili nchi yake nchini Marekani wakati wa mapumziko ya mechi za kimataifa, huku Liverpool ikianza kutetea taji lake la Ligi ya Mabingwa ugenini dhidi ya Napoli wiki ijayo, kocha Jurgen Klopp aliamua kumpumzisha fowadi huyo.

Lakini majeraha ya Divock Origi katika kipindi cha kwanza yakashuhudia Firmino akiingizwa uwanjani mapema tofauti na ilivyopangwa na alionyesha umuhimu wake wakati alipocheza pasi iliyosababisha bao la pili la Sadio Mane.

Halafu akatoa pasi ya mwisho kwa Mohamed Salah aliyefunga bao la tatu zikiwa zimesalia dakika 18 na Van Dijk alifurahishwa na hilo.

"Yeye ni mchezaji muhimu zaidi kwetu," alisema Van Dijk akiiambia BT Sport. "Najua namna gani ilivyo ngumu kwa beki wakati mshambuliaji anapodondosha mpira kwenye nafasi yake.

"Anafanya maisha yanakuwa magumu kwa beki yeyote duniani, nafikiri hivyo. Yeye ni mzuri na nina furaha yupo kwenye timu yetu."

## Solskjaer: McTominay ni kiongozi mzuri Man Utd

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amemwelezea Scott McTominay kama mmoja wa viongozi wa Manchester United baada ya kiwango chake katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Leicester City Jumamosi.

United ilimaliza ukame wa kutoshinda mechi tatu kwenye Ligi Kuu shukrani kwa bao la Marcus Rashford la dakika ya nane kwa mkwaju wa penalti katika dimba la Old Trafford.

McTominay alionyesha kucheza vizuri zaidi kutokana na kukosekana kwa Paul Pogba ambaye ni majeruhi, akicheza kwa ushirikiano mzuri na James Maddison na kuisumbua mara kwa mara safu ya ulinzi ya Leicester.

"Ana imarika, si ndio?" Alisema Solskjaer akimzungumzia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

"Leo, nafikiri alikuwa bora zaidi. Alipoteza mpira mara kwa mara, kitu ambacho unakitarajia wakati akijifunza kucheza kwenye nafasi mpya ya kiungo.

"Alikwenda na kukaba, kupigania kupata mpira... kama kuna timu inataka kujaribu kujifunza kwetu sisi, yeye yupo pale kama kiongozi."



## CONTE ATAKA INTER KUIMARIKA ZAIDI

**MILAN, Italia**

ANTONIO Conte ameitaka Inter kuongeza ubunifu zaidi wa kucheza wakati walipoweza kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Udinese iliyomaliza na wachezaji 10 uwanjani juzi Jumamosi.

Inter ilijivuta hadi kileleni mwa msimamo wa Ligi ya Serie A, ikiwa pointi mbili dhidi ya Juventus, ambapo bao la kichwa la Stefano Sensi likawawezesha kupata ushindi huo.

Bao la Sensi lilifuatiwa na Rodrigo De Paul kuonyeshwa kadii nyekundu, baada ya mwamuzi kuangalia marudio, wakati Maurizio Mariani akimfanyia faulo Antonio Candreva kwa kumpiga kichwa alipokuwa hana mpira.

Romelu Lukaku alishindwa kupiga shuti lolote langoni, huku Alexis Sanchez aliingizwa kucheza kwa mara ya kwanza zikiwa zimesalia dakika 10 mpira kumalizika.

"Nawapongeza kwa sababu ulikuwa ni mchezo mgumu dhidi ya timu imara na muhimu pointi tatu tulipata. Tulistahili kuzipata, lakini itambulike kwamba Udinese walicheza vizuri na walikuwa kwenye mchezo hadi mwisho," alisema Conte akiiambia DAZN.

"Hatukuwa na ubunifu, na hatukuwa mchezoni, hivyo tunatakiwa kujiimarisha zaidi.

"Tunatakiwa kupigana. Nasoma upuuzi mwingi kwenye magazeti. Tunatakiwa kwenda njia yetu bila kufikiria kitu chochote kile. Ukweli ni kwamba hakuna kitu rahisi na hatutakichukulia kitu chochote kwa urahisi."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR LAZIMA AKUBALI KUZOMEWA PSG- TUCHEL

Haya ndio maisha, inakuwa si rahisi kwa mashabiki kukubali wakati wa soko la uhamisho, tunatakiwa kukubali tabia...

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel, amesema Neymar anapaswa kukubali kuzomewa na mashabiki baada ya kurudi dimbani kwenye ushindi dhidi ya Strasbourg.

Akicheza mchezo wake wa kwanza msimu huu kwa PSG, Neymar alicheza kwa kiwango cha kuvutia na kuifungia bao PSG iliyoibuka na ushindi wa 1-0 Jumamosi.

Lakini nyota huyo wa Brazil alijikuta kwenye wakati mgumu kwa kuzomewa na mashabiki, ambao walionekana kuwa na hasira naye hasa baada ya sakata lake la uhamisho kipindi cha majira ya joto wakati akilazimisha kutaka kurudi Barcelona.

Tuchel alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anatakiwa kukubali kuzomewa na mashabiki hao, lakini alimsifu muitikio wa Neymar.

"Haikuwa rahisi kwa sababu ni mtu makini, lakini alifanya vizuri," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Haya ndio maisha, inakuwa si rahisi kwa mashabiki kukubali wakati wa soko la uhamisho. Ndio maana tunatakiwa kukubali tabia zao. Sitaki kuhukumu tabia zao, ni kama ilivyotokea. Haikuwa rahisi.

"Anaweza kucheza vizuri, kwa kupiga chenga nyingi na kuburuzika. Anahitaji mechi kadhaa ili kuwa bora zaidi.

"Ana ubora unaomfanya aamue hatima ya mchezo. Nina furaha alionyesha hivyo katika dakika ya mwisho."

PSG inaongoza msimamo wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, kwa pointi mbili baada ya kupata ushindi wao wa nne katika mechi tano.

Watacheza na Real Madrid kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, keshokutwa Jumatano.

## KWA UFUPI

**BECKHAM AMFUATA MESSI**

NAHODHA wa zamani wa England, David Beckham amepiga hatua ya kutoa ofa kwa mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi kujiunga na klabu yake mpya inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani (MLS), Inter Miami, kwa kutuma wawakilishi wake kwenda kuzungumza na baba wa nyota huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 32. ***(Sun on Sunday)***

**BALE ATAKIWA INTER MIAMI**

KLABU ya Inter Miami ya Marekani inavutiwa kumsajili mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale, 30, kutoka Real Madrid. ***(Maxifoot - in French)***

**KROOS, POGBA KUPISHANA**

Manchester United inavutiwa kuinasa saini ya kiungo wa Real Madrid, Mjerumani Toni Kroos, 29, katika dirisha la Januari katika uhamisho utakaomhusisha Kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26. ***(Bild - in German)***

**DE GEA AJIFUNGA MINNE**

KIPA wa Hispania, David de Gea, 28, amesaini mkataba mpya wa miaka minne na Man United utakaomfanya kulipwa pauni 250,000 kwa wiki, ambao utapanda hadi kufikia pauni 350,000 kwa wiki kutegemeana na kiwango atakachokionyesha. ***(Sunday Mirror)***

**HUDSON-ODOI KUFUNGWA MINNE**

MSHAMBULIAJI wa England, Callum Hudson-Odoi, 18, atamwaga wino mkataba wa miaka mitano hapo Chelsea baada ya kurejea akitokea chumba cha majeruhi. ***(Sun on Sunday)***

**MANE, LIVER MEZANI**

Liverpool imefungua meza ya mazungumzo na mshambuliaji Msenegal Sadio Mane, 27. ***(SoccerLink, via Sport Witness)***

**ERIKSEN KUSEPA JANUARI**

KIUNGO Mdenmark Christian Eriksen, 27, anataka kuondoka Tottenham na kujiunga na Real Madrid katika dirisha la Januari. ***(Marca - in Spanish)***

**MATIC LULU VIGOGO ITALIA**

AC Milan na Inter Milan zinavutiwa kuipata huduma ya kiungo Mserbia, Nemanja Matic, 31, kutoka Manchester United katika dirisha la Januari. ***(Corriere Dello Sport - in Italian)***

**MANDZUKIC KUTIMKIA MAREKANI**

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Mcroatia Mario Mandzukic, 33, ambaye majira ya joto alihusishwa na Manchester United, anakaribia kutua Ligi Kuu ya Marekani (MLS), kuichezea LAFC. ***(Calciomercato)***

**MURIQI AIVUTIA MAN UNITED**

Manchester United ilituma mashushushu wake kwenda kumtazama straika wa Fenerbahce, Vedat Muriqi, 25, wakati wa mechi kati ya Kosovo na England wiki moja iliyopita. ***(Sunday Express)***

**ALMADA AITOSA MAN CITY**

KINDA Muargentina Thiago Almada, 18, ambaye aliivutia Manchester City, amesaini mkataba mpya wa miaka minne na Velez Sarsfield. ***(Manchester Evening News)***

**NEWCASTLE KUELEKEA SOKONI**

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce amepewa baraka zote za kusajili wachezaji wapya katika dirisha la Januari, na zaidi akitakiwa kumulika mawinga. ***(Chronicle)***



HABARI MICHEZO

# AUSSEMS KUKOMALIA WASHAMBULIAJI SIMBA

Na Somoe Ng'itu

KOCHA Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Mbelgiji Patrick Aussems, amesema ataendelea kuwanoa washambuliaji wake ili waweze kufunga mabao mengi zaidi katika mechi zinazofuata za ligi hiyo ya juu nchini.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Aussems alisema anahitaji kuona safu yake ya ushambuliaji inatumia vema nafasi za kufunga wanazozitengeneza na hatimaye kupata ushindi mnono katika kila mechi watakayocheza.

Aussems alisema kila mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ni ngumu, na ili kujiweka katika nafasi salama zaidi ni kupata mabao mengi ambayo yatawahakikishia kuondoka na pointi tatu.

"Nawapongeza kwa kucheza vizuri na kupata ushindi katika mechi mbili tulizocheza za Ligi Kuu, lakini bado hawatumii vizuri nafasi ambazo wametengeneza, katika mechi dhidi ya Mtibwa Sugar, wamepoteza nafasi kama tatu nyingine za kufunga, tunahitaji kulimaliza tatizo hili," alieleza Mbelgiji huyo.

Aliongeza kuwa anahitaji kuona hawarudii makosa katika mechi ijayo dhidi ya Kagera Sugar na kupata ushindi ili kuendelea kukaa kileleni katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 20 kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini.

Naye nahodha msaidizi wa timu hiyo, Mohammed Hussein "Zimbwe Jr" amesema kikosi chao kina kiu ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo kwa msimu mwingine wa tatu mfululizo.

"Tunajua hakuna mechi rahisi, timu zote zimejiandaa kuonyesha ushindani, kila mchezo kwetu tunauona kama fainali, naamini tutaendelea kupambana ili tutimize malengo yetu, tunaomba ushirikiano uliokuwapo, uendelee," Zimbwe Jr alisema.

Simba inaongoza ligi ikiwa na pointi sita baada ya kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya JKT Tanzania na Ijumaa ilipata ushindi wa mabao 2-1 walipoikaribisha Mtibwa Sugar kutoka Manungu, Turiani mkoani Morogoro.



Washiriki wa mbio za baiskeli mkoani Arusha wakijiandaa kuanza mbio hizo, zilizofanyika Jumamosi mkoani humo. **PICHA: ALLAN ISACK**

## Kamusoko ajipa matumaini kuitoa Yanga

Na Shufaa Lyimo

KIUNGO wa Zesco United, Thabani Kamusoko, amesema sare waliyoipata ugenini dhidi ya Yanga kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imempa matumaini ya timu yake kusonga mbele.

Akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Taifa juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1, Kamusoko alisema anashukuru kuipatia bao la kusawazisha timu yake ugenini licha mchezo kuwa na presha pamoja na ushindani mkubwa.

"Nashukuru kwa bao ambalo nimelifunga ugenini, kwangu mimi ni faida kwa sababu kila timu ilikuwa inacheza kwa ushindani mkubwa ili ishinde," alisema Kamusoko.

Vile vile alisema lengo lake ni kujipanga akishirikiana na wachezaji wenzake kuhakikisha wanashinda na kutimiza malengo yao.

"Mikakati yangu kwa sasa ni kwenda kuanza maandalizi ya mchezo ujao nikishirikiana na wachezaji wenzangu ili tusonge mbele," alisema.

Alisema hawezi kuizungumzia Yanga kutokana na kuwa tayari alishaachana nayo na kudai kuna baadhi ya wachezaji ambao hawafahamu.

"Siwezi kuizungumzia Yanga kwa sababu sasa hivi nipo Zesco kuhusu ubora wa wachezaji pia siwezi kuuzungumzia kwa sababu sijawaona wakifanya mazoezi tumekutana uwanjani," alisema.

Mchezaji huyo aliyeifungia Zesco bao la kusawazisha katika dakika za majeruhi, aliwahi kuitumikia Yanga kabla ya kuachwa na kutimkia Zambia kujiunga na 'Mafundi wa Umeme' hao.

# Kikwete aongoza Brazuka Marathon

Na Mary Geofrey

RAIS mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, ameongoza mbio za kuchangisha fedha kwa ajili ya kutibu zaidi ya watoto 500 walio chini ya miaka mitano, wanaosumbuliwa na matatizo ya moyo.

Kikwete, aliyetembea mbio za kilometa tano, aliwataka waandaaji ambao ni taasisi za benki 18 nchini, kufanya tena mwakani mbio hizo kwa lengo la kuwafikia watoto wengi zaidi.

Mbio hizo zijulikano kama, Brazuka Marathon, zilifanyika jijini Dar es Salaam jana kuanzia mtaa wa Kiungani kupitia Central, Kivukoni, Barabara ya Barack Obama, eneo la Palm Beach na Upanga kisha kurudi katika viwanja vya michezo vya Jakaya, washiriki zaidi ya 800 walikimbia kilometa 15, na kilometa 10 na kilometa tano.

"Mashindano yalikuwa mazuri kwa sababu washiriki walipata uhuru wa kuchagua kulingana na uwezo wao katika kukimbia kilometa 15, 10 na tano. Nawashauri washiriki kuandaa tena mwakani kwa sababu yanafurahisha, pia kusaidia watoto hawa wenye matatizo ya moyo," Kikwete alisema.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Juliana Shonza, alimshukuru Kikwete kwa kuendelea kuunga mkono sekta ya michezo nchini.

Naye Mratibu wa Brazuka Marathon, Nasikiwa Berya, alisema watu wengi wamejitokeza katika mbio hizo zilizokuwa na kiingilio cha Sh. 15,000, Sh. 10,000 na 5,000 na washindi walipewa medali.

Naye Katibu Mkuu wa Shirikisho la Riadha (RT), Willhem Gidabuday, aliwapongeza washiriki hao ambao wamejitokeza licha ya kwamba hakukuwa na zawadi za fedha.

## Serikali yatakiwa kumulika baiskeli

Na Allan Isack, ARUSHA

WADAU wa mbio za baiskeli mkoani Arusha, wameomba serikali kutoa kipaumbele na kuwekeza katika mchezo wa baiskeli kama wanavyofanya kwenye michezo mingine kwani mchezo huo utaongeza ajira kwa vijana na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira hapa nchini.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mashindano ya baiskeli mkoani hapa, mwandaaji wa mashindano ya baiskeli, ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Rexlec Cycling, Mchungaji Joel Saiy, ameomba serikali na jamii kuupenda mchezo huo kwani utaweza kuwa sehemu ya utatuzi wa changamoto ya ajira kwa vijana nchini.

Alisema mashindano hayo, yalikuwa ya umbali wa kilometa 80 kwa wanaume, wanawake kilometa 60 na wazee kilometa 60.

"Ukishiriki mashindano ya baiskeli unakuwa na afya nzuri, mwili unakuwa imara na haushambuliwi na magonjwa pia unatengeneza ajira," alisema.

Aidha, alisema kupitia mashindano hayo, wanawaandaa vijana kwa ajili ya kushiriki mashindano ya dunia ya baiskeli yatakayofanyika nchini Rwanda mwaka 2025.

Mwenyekiti wa Chama cha Waendesha Baiskeli Tanzania (Chabata), Salim Seif, alisema mashindano hayo, yalikuwa mazuri na washiriki walifurahishwa nayo.

# Michezo

Jumatatu Septemba 16, 2019

Nipashe




## Neymar lazima akubali kuzomewa PSG- Tuchel

HABARI UK 30

CHA KWANZA...



Kiungo wa Norwich, Kenny McLean, akiruka juu ya Rodri na kuiandikia timu yake bao la kwanza kwa kichwa wakati wakishinda 3-2 dhidi ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England, Manchester City kwenye mechi ya ligi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Carrow Road juzi. **HABARI UK. 28**

# LWANDAMINA AIONYA YANGA, ZAHERA AFURA

●●●Aeleza sababu ya kufungwa Taifa na lengo la kwenda kushinda ugenini, lakini aambiwa...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, akikasirishwa na kitendo cha safu yake ya ushambuliaji kushindwa kutumia nafasi wanazozipata dimbani, Kocha Mkuu wa Zesco, George Lwandamina, amewaonya wapinzani wao hao kwa kuwaambia watambue hawajawahi kupoteza mechi yoyote ya kimataifa kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa.

Yanga juzi ililazimishwa sare ya bao 1-1 kwenye mechi yao ya kwanza ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Taifa, hivyo inahitaji ushindi ama sare ya zaidi ya bao moja ili kuweza kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Hata hivyo, Zahera amesema anaamini timu yake itapata matokeo mazuri katika mchezo wa marudiano na kuwataka mashabiki wa timu hiyo wasiwe na wasiwasi.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo kumalizika, Zahera, alisema Yanga ina nafasi kubwa ya kusonga mbele katika mashindano hayo na wamejiandaa kwenda kupambana kwenye mchezo huo wa marudiano utakaochezwa mjini Ndola Septemba 27, mwaka huu.

Zahera alisema kikosi chake kitajipanga kwenda kucheza soka la ushindani, na wameshaufahamu ubora na udhaifu wa Zesco.

Kocha huyo aliwapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha kiwango kizuri katika kipindi cha kwanza, na kuahidi kufanyia kazi makosa waliyofanya kwenye dakika za majeruhi kabla ya mchezo wa marudiano.

"Matokeo si mabaya, tulipata bao hapa nyumbani na wao wamefanikiwa kupata, hata wasingefunga, sisi tulishajipanga kwenda kusaka bao ugenini ili tuweze kusonga mbele katika mashindano hayo, hatuna wasiwasi na mchezo huo," alisema Zahera.

Alisema pia wachezaji wake walijisahau baada ya kupata bao la kwanza na kuwafanya wapinzani wao waweze kutawala mpira na kusababisha kuwa kwenye wakati mgumu katika dakika za mwisho za kipindi cha pili.

"Lakini pia hatukuweza kutumia vema nafasi tulizozitengeneza katika kipindi cha pili, angalia kama Ngasa (Mrisho), alivyokosa nafasi," aliongeza kocha huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Naye Kocha wa Zesco, Lwandamina, alisema mechi ilikuwa na ushindani na kila upande ulicheza soka la kuburudisha.

"Bao moja la ugenini tulilopata ni muhimu sana, Yanga walicheza vema zaidi katika kipindi cha kwanza, naamini mchezo wa marudiano utakuwa mzuri, na kumbukeni Zesco haijawahi kupoteza hata mechi moja ya kimataifa kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa," Lwandamina alisema.

Bao la Yanga katika mchezo huo lilifungwa kwa njia ya penalti na Patrick Sibomana wakati kiungo wa zamani wa timu hiyo aliyewahi kuichezea Yanga, Mzimbabwe Thabani Kamusoko aliisawazishia timu yake dakika za majeruhi.

## Rekodi Azam FC Chamazi yavunjwa

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE rekodi ya Azam FC ya kushinda mechi zote ikiwa katika uwanja wake wa Chamazi tangu ianze kushiriki kwenye michuano ya kimataifa, imevunjwa rasmi na Triangle FC ya Zimbabwe baada ya jana kukubali kipigo cha bao 1-0.

Katika mechi hiyo ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho ambayo ilihudhuriwa na mashabiki wengi kila mmoja akikutana na Ice Cream ya Ukwaju getini, licha ya Azam kumiliki mpira kwa dakika zote 90, ilishindwa kuipenya ngome ya Triangle iliyokuwa ikitumia mashambulizi ya kushtukiza.

Bao la dakika ya 34 kupitia kwa Ralph Kawondera aliyeiwahi na kuunganisha krosi kutoka wingi wa kulia, ndilo lililovunja rekodi hiyo ya Azam Uwanja wa Chamazi baada ya goli hilo kudumu kwa dakika zote 90.

**Licha ya Azam kipindi cha pili kumtoa mshambuliaji Richard Djodi na kumwingiza Shabani Chilunda ambaye baadaye alimpisha Idd Kipagwile huku pia Mudathir Yahya akiingia, haikuwa rahisi kupenya lango la Triangle ambayo 'ilipaki basi' kwa dakika zote za kipindi cha pili.**

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa Azam, Etienne Ndayiragije, atapaswa kuifanyia kazi safu yake ya kiungo mchezeshaji kwani pasi zao za mwisho kwa washambuliaji zilikuwa tatizo.

Kwa matokeo hayo sasa Azam inapaswa kujipanga vilivyo ili kuweza kupindua matokeo kwenye mechi ya marudiano Septemba 28, mwaka huu na hatimaye kucheza mechi ya mchujo na moja ya timu zitakazotolewa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa, mchezo ambao utaamua hatima yake ya kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042